ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.

14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae

30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
33.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndugu Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 28 Januari, 2013

Kikao Kimeanza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika, *(Pandu Ameir Kificho)* alisoma Dua

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kuna taarifa ndogo lakini nitaitoa baadae ili wajumbe waje wafurahike wote kutokana na taarifa iliyopo. Kwa hiyo tunaendelea maswali na majibu.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 60

Hatua Zilizochukuliwa na Serikali Baada ya Vurugu Dhidi ya Wahusika

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwakuwa mara baada ya kutoweka Imamu wa taasisi ya UAMSHO katika mwezi wa Oktoba, 2012 lilitokea vurungu kubwa nchini na hatimae kusababisha Mapambano makubwa baina ya wale wanaosadikiwa ni wafuasi wa UAMSHO pamoja na vyombo vya Dola jambo ambalo lilipelekea wananchi wengi kujeruhiwa na hatimae kupelekea mauaji ya kishenzi ya Askari mmoja wa Jeshi la Polisi.

(a) Je, ni watu wangapi waliokamatwa, kuhojiwa na hatimae kufikishwa Mahakamani.
(b) Ni watu wangapi waliouwawa na Mali zenye thamani gani zimeharibiwa kwenye vurugu hizo tangu zianze hadi leo hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 60 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, katika vurugu zilizotokea mwezi wa Oktoba 2012 baada ya kutoweka Imam wa Jumuiya ya UAMSHO, Sheikh Farid Hadi watu waliokamatwa kuhusiana na kadhia hiyo ni 71 na waliofikishwa Mahakamani ambao kesi zao zinaendelea ni 17.

(b) Mhe. Spika, ni mtu mmoja ndiye aliyeuwawa katika vurugu hizo ambaye ni askari mwenye Namba F.2105 CPL Said Abdulrahman. Na mali iliyoharibiwa inakadiriwa kufikiwa thamani ya zaidi ya shilingi milioni mia tano (500, 000,000/=) ukijumuisha uharibifu wa majengo, barabara, magari na kadhalika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba kuna watu 21, walikamatwa na kupelekwa Mahakamani. Na kwa kuwa tayari watuhumiwa wameshapelekwa mahakamani. Na kwa kuwa katika vitongoji na vijiji na vijiji pamoja na miji ya Unguja katika kipindi kile ilikuwa ni jambo la kawaida kupita askari wakipiga watu, kunyanyasa na kuwatesa barabarani huku watu wengine watuhumiwa wapo Mahakamani.

(a) Ni sababu gani za msingi zilizopelekea askari kupita barabarani katika kipindi kile kupiga na kuwatesa watu wengine waliokuwepo vijijini wakati watuhumiwa wakiwa Mahakamani.

(b) Kwa kufanya hivyo Mhe. Waziri anakubaliana nami kwamba jeshi letu la polisi haliko mahiri katika kufanya kazi zake.

(c) Atakubaliana nami kwamba kitendo kile kilichofanywa na serikali cha kuwapiga na kuwatesa na kuwanyanyasa watu majumbani na mitaani ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binaadamu uliofanywa kwa makusudi na jeshi la polisi pamoja na vikosi vya SMZ.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika jeshi letu la polisi hufanya kazi kwa kuzingatia Sheria za nchi na misingi ya haki za binaadamu. Hata ukiona jeshi la polisi linafanya operesheni maalum kwa ajili ya kazi maalum inatokana na ukiukwaji wa sheria zinazofanywa na watu mbali mbali. Ama zinazoashiria uvunjifu wa amani ama zinazosababisha kuleta vurugu na kuifanya nchi iwe katika hali ya taharuki.

Mhe. Spika, nyote mnaelewa mazingira yaliyojitokeza ya watu kujiita ubaya ubaya na vikundi vyengine ambavyo kwa makusudi vilikuwa vinachungua hatua ya kupiga watu, uonea watu, kudhalilisha watu na kuwatia watu hofu, mpaka ilifika wakati mpaka wanafunga barabara.

Mhe. Spika, lazima tuone jeshi letu la polisi na vikosi vyetu vya SMZ vinapochukua hatua za kupambana na wale wote ambao wanafanya vitendo kinyume na sheria za nchi. Jeshi haliruhusiwi kabisa kumuonea mtu wala kumdhalilisha mtu. Ni pale tu linapoona vitendo vya kinyume na sheria vinakiukwa ndipo linachokua hatua.
Mhe. Spika, kama kuna mtu yeyote ameonewa kinyume cha sheria, milango ya sheria iko wazi, vyombo vya sheria vipo wazi, mtu huyu achukue hatua za kisheria kwa kufuata misingi ya sheria zilizowekwa.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri aliyejibu Mhe. Waziri naomba kuuliza kwamba mbali na wafanyabiashara na wananchi kuathirika katika tukio lile lakini yapo maeneo mengine ambayo yameathirika kwa kiasi kikubwa hususan katika majengo ya vyama vya siasa. Je, ni hatua gani zimechukuliwa ili kuwalipa fidia vyama vile.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nchi yetu inaendeshwa kwa misingi ya Katiba na Sheria, pale ambapo pametokea makosa hatua zinazochukuliwa ni

kupeleka wahusika Mahakamani na Mahakama ndiyo itakayotoa maamuzi ya mwisho. Wale ambao mali zao zilizoharibiwa wana haki kabisa kudai fidia kwa kupitia hizo hizo taratibu za sheria zilizopo.

Mhe. Spika, wananchi lazima waelewe kwamba milango ya sheria iko wazi na pale wanapoonewa au linapotokea jambo la kunyimwa haki zao basi wafate mkondo huo ili wapate haki zao.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri swali moja dogo sana la nyongeza.

Mhe. Spika, katika majibu yake ya swali la msingi alisema kwamba katika vurugu hizi kuna mtu mmoja aliuwawa ambaye ni askari polisi. Mimi nilikuwa nataka kujua Mhe. Waziri ni watu wangapi ambao wamefikishwa Mahakamani kutokana na tukio lile la mauaji.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa sasa sina usahihi wa idadi ya watu wangapi ambao wamefikishwa Mahakamani kwa tukio lile. Lakini naelewa kwamba wapo watu tayari wamepelekwa Mahakamani kwa tukio lile. Na bado uchunguzi zaidi unafanywa ili wale wote waliohusika na tukio lile waweze kufikishwa katika vyombo vya Mahakama.
Hivi sasa jeshi la polisi linafanya kila jitihada kuhakikishwa wale wote waliohusika katika kufanya vurugu, katika kuingilia kusimamisha hali ya amani na utulivu katika nchi yetu, basi wote hawa watafikishwa katika vyombo vya sheria na hatua za sheria zitachukua mkondo wake.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, swali langu lilikuwa linaulizia idadi ya watu, Mhe. Waziri amesema hajui ni watu wangapi. Bali naomba aliahidi Baraza kwamba ataleta ile idadi ya watu ambao wamefikishwa Mahakamani. Hakunijibu kasema tu kwamba hajui idadi watu ni wangapi waliopelekwa Mahakamani kuhusu suala hili. Suala langu nilikuwa nataka kujua idadi ya watu ambao wapo Mahakamani kutokana na tukio lile. Sasa sijui analiahidi nini Baraza lako kuhusu suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kurudia majibu yangu na Mheshimiwa naomba ayasikie kwa vizuri kabisa. Na haya ndio majibu yangu kwa serikali namjibu kwamba idadi halisi ya watu waliopelekwa Mahakamani siifahamu kwa sasa lakini najua kwamba kuna watu wamepelekwa Mahakamani kwa tukio lile na kesi inaendelea na uchunguzi zaidi unafanywa na wote watakaohusika watapelekwa Mahakamani.

Nam. 82

Vibali vya Ujenzi Baraza la Manispaa

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 83

Kazi za Masheha

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa

Nam. 3

Tatizo Katika Usambazaji Umeme

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Shirika la Umeme huingia mkataba na wananchi katika usambazaji na utiaji umeme katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu. Muda unaotolewa kwa shughuli za kazi hiyo ni mzuri na unajenga matumaini kwa kazi ya usambazaji wa nguzo, uwekaji wa nyaya na uingizaji wa umeme ndani ya nyumba. Lakini matokeo yake yanakatisha tamaa kwa wananchi kwani mwaka utafika bila ya mafanikio.

(a) Mhe. Waziri ahadi wanazotoa wanaohusika ni ahadi zinazotekelezwa kwa wakati wanaokubaliana.

(b) Je, hatua gani utachukua kuhakikisha kwamba ahadi hizo ziwe za kweli zisizo na usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 3 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna baadhi ya kazi zinachelewa kutekelezwa kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa shirika. Mfano ahadi huenda isitekelezeke katika kipindi kilichopangwa iwapo vifaa vya kazi hiyo vitakosekana kutokana na sababu mbali mbali na pia matukio yanayoweza kutokezea kama majanga na kadhalika.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu wizara yangu itasimamia utekelezaji wake, pamoja na usambazaji wa huduma hiyo kwa haraka ikizingatia muda anaopewa mteja na kumuondoshea usumbufu.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri katika kulijibu swali hili, lakini Mhe. Spika, bado swali hili majibu yake hayaridhishi. Kwa sababu swali hili ni la muda mrefu na haya ni ya kawaida katika shirika la umeme katika kuwasambazia wananchi umeme majumbani na baada ya kupoekea fedha kwa wananchi muda unakuwa ni mrefu. Lakini haya ndiyo yanakuwa majibu ya kila siku.

Naomba kumuuliza hasa tatizo ni nini? Tatizo ni vifaa haviji kwa wakati au vifaa vinakuwepo lakini ni uzembe wa watendaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba kuna sababu tufouti zinazoweza kujitokeza, hususani wakati mwengine shirika linakuwa halina vifaa na wakati mwengine tunapoagizishia vifaa huwa havitoshelezi, kwa hiyo tunakuwa tunawaungia wale waliokuwa wametangulia na vinapomaliza inabidi wale wengine tuwape muda na vitapofika tena inabidi tuwafungie laini zao. Kwa hizo hizo ndio sababu zinazosababisha. Lakini nimuahidi Mheshimiwa Mwakilishi kwamba shirika langu sasa hivi litajipanga vizuri zaidi ili tuhakikishe kwamba shughuli zote tunazifanya kwa wakati uliopangwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, binaadamu akiuguwa huwa anakimbilia hospital, na umeme ukileta matatizo dawa yake ni vipuri, hivi sasa kuna tatizo kubwa la nguzo katika wizara yako. Ikiwemo wananchi wa Jambiani kulipa gharama ya milioni moja laki moja karibu mwezi mzima mpaka muda huu hakuna kinachoendelea mpaka muda huu. Je, unawambia nini wananchi wa Jimbo la Muyuni Shehia ya Jambiani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kwali kwamba sasa hivi tuna matatizo ya nguzo mbovu ndani ya Zanzibar ambazo haziko Jambiani tu, bali zipo takriban maeneo mengi sana ya Zanzibar. Lakini nimthibitishie Mhe. Mwakilishi kwamba kama nilivyoeleza tunajipanga na tutajitahidi kuyaondoa makero haya. Naamini kwamba linapotokea tatizo kama hili la kuanguka kwa nguzo kutokana na uchakavu basi haliathiri mteja tu isipokuwa linaathiri mpaka shirika la umeme kwa sababu linaingiza hasara kubwa baada ya kutokea kile ambacho kinatokea.

Kwa hivyo nimuombe Mhe. Mwakilishi astahamili tunajipanga na tutajitahidi kuwayaweka sawa haya masuala.

Nam. 58

Tathmini ya Mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza:-

Pamoja na kuwa wizara hii imeshaamua kutowaajiri tena waalimu wa masomo ya "Art" hasa yale ya Dini ya Kiislam na Kiarabu, lakini hivi sasa wako waalimu wengi ambao wameshaajiriwa na wako katika vyuo mbali mbali vya elimu ya juu, lakini hawapatiwi mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Zanzibar na ile ya Tanzania.

(a) Je, katika mwaka huu wa 2012/13 ni wanafunzi wangapi waliomba mikopo Bodi ya Mikopo ya Zanzibar na wangapi waliopata mikopo hiyo.

(b) Wangapi waliomba Bodi ya Mikopo ya Tanzania na wangapi waliopata.

(c) Je, mikopo katika Bodi ya Mikopo ya Tanzania inatolewa kwa uwiano gani baina ya Bara na Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 lenye kifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inatoa mikopo kwa waombaji wa mafunzo ya elimu ya juu kwa kufuata vigezo vya maeneo ambayo yamepewa kipaumbele na Tume ya

Mipango ya Zanzibar. Vipaumbele hivyo vimezingatia mahitaji ya nchi katika sekta ya umma na sekta binafsi. Pia, vipaumbele vinaweza kubadilika badilika kila mwaka kutegemea mahitaji ya soko la ajira. Ni kweli, kwa hivi sasa wapo wahitimu wengi wa ualimu wa masomo ya Dini na Kiarabu ambao hawajapata ajira kutokana na masomo hayo kuwa walimu wengi maskulini. Pia ni kweli wapo walimu wengi wa masomo hayo walioyoko vyuoni ambao wameshaajiriwa na baadhi yao wameomba mikopo katika Bodi ya Mikopo ya Zanzibar. Pia, ni muhimu kuzingatia kuwa Bodi ya Mikopo inawajibu kuangalia mahitaji ya wafanyakazi wote na wa sekta zote na wala sio kwa sekta ya elimu pekee yake.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

(a) Kwa mwaka 2012/2013, Bodi ya Mikopo ilipokea maombi 3020, na jumla ya maombi yaliyokubaliwa ni 800. Kati ya maombi yaliokubaliwa maombi 86 ni ya walimu wanaochukua masomo ya masomo ya Kiswahili/Kiarabu, 69 Kiarabu/Dini ya Kiislamu, 18 Kiswahili/Kiarabu na 4 Kiingereza/Kiarabu. Walimu hao ambao wameajiriwa ni 177.

(b) Kuhusu waombaji waliowasilisha maombi yao kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Tanzania, wizara yangu haina kumbukumbu za idadi yao kwani maombi yao

yanawasilishwa moja kwa moja kwa chombo hicho na hayana ulazima wa kupitishwa katika wizara yetu.

(c) Mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Tanzania haina kigezo cha uwiano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar. Utaratibu wao ni kutoa mikopo kwa mujibu wa sifa za mwombaji na maeneo ya kipaumbele ambayo wameweka. Nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya mwalimu Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza kama ifuatavyo lenye vifungu (a) na (b).
Katika maelezo ya msingi ya Mhe. Mwakilishi alihusisha walimu wa masomo ya Art. Hivi karibuni ulitupa taarifa kwamba Zanzibar ilitakiwa kupeleka walimu 50 nchini Libya wenye fani ya Kiswahili. Lakini kutokana na kwamba serikali imelipuuzia somo la Art na kulifanya kama si somo muhimu, tumekosa kuwapeleka wataalamu hao nchi za nje ili kupata ajira na kuongeza kipato kwa Wazanzibari.

(a) Je, utaratibu wa Serikali wa kudharau masomo ya Art kwa maana ya Kiswahili na Kiarabu si mnarejesha nyuma katika maendeleo ya Zanzibar katika ulimwengu huu wa Kiswahili.

(b) Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba Bodi ya Mikopo Tanzania hutoa mikopo yake kutokana na vipaumbele vya Taifa, wakati anajua kwamba vipaumbele vya Tanzania Bara ni tofauti na vya Zanzibar. Kama kigezo ni hicho si kuwawafanya Wazanzibari wakose haki yao ya msingi ya mfuko huo wa taifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, anasema katika suala lake kwamba Libya walikuwa na mahitaji ya walimu 50 ambao walitaka wapelekwe lakini Wizara ya Elimu kutokana na hawakuwa na walimu hao au wanafunzi hao, hawakupelekwa. Hili Mheshimiwa mimi sina hakika nalo na ndio kwanza namsikia Mhe. Hija Hassan Hija, kwa hivyo siwezi kulijibu kama lipo basi nitalileta kwa maandishi na nitamuelewesha.

Mhe. Spika, la muhimu ninachotaka kusema ni kwamba hatuna tatizo la walimu wa Art, ndio maana Afrika Mashariki imeanzisha Kitovu cha Elimu ya Kiswahili na tumepewa heshma ya Zanzibar kuwa na kitengo hichi cha Kiswahili kwa Afrika Mashariki nzima, sisi ndio ambao tutaongoza hichi.

Kwa hivyo ni dhahiri kuwa hatuna hilo tatizo. Lakini nataka nikatae maneno ya kaka yangú Mhe. Hija Hassan Hija kusema vipaumbele vya Zanzibar na Bara kwamba vipo tofauti. Mheshimiwa vipa umbele vya mikopo havina tofauti kati ya Zanzibar na Bara. Vyote viko sawa sawa, vile ambavyo tunavihitaji na wenzetu Bara ndivyo wanavyovihitaji ndio mahitaji ya sasa kwa Tanzania Mheshimiwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto, karibuni tulikwenda katika Tume hizi bodi za Mikopo za Bara na Zanzibar na tulikwenda kuhoji hizi habari za vipaumbele, yule anayeongoza Bodi ya Mikopo ya Zanzibar akatueleza vyake na huyu wa Bara akatueleza vyake, ikawa ni tofauti.

Leo Mhe. Waziri anatwambia kwamba vipeumbele ni sawa sawa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Yupi tumuamini baina ya yeyé na hizi bodi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, siwezi kudanganya Baraza la Wawakilishi, najua linaheshima yake na wote waliokuwepo hapa ni wawakilishi wa wananchi, wameletwa hapa kwa ajili ya kusimamia wananchi wao. Bahati nzuri na mimi pia Mhe. Spika, mmenipeleka Bungeni kwenda kuwakilisha Baraza la Wawakilishi na ni Mjumbe katika Kamati hiyo ambayo anasema. Navijua uzuri vipaumbele ambavyo wanavilenga wenzetu Bara na vile vile navijua vipeumbele ambavyo tunavyosisi katika Wizara ya Elimu. Kwa ushahidi nitawaletea makabrasha yangu ya Kamati niyalete hapa Mheshimiwa ili waje wajiridhishe kuwa vipaumbele walivyonavyo wenzetu wa Bara ndivyo vipaumbele ambavyo vinakwenda sambamba na vipaumbele ambavyo tunavyo Zanzibar. Mhe. Spika, mahitaji kwa sasa dunia nzima ni sayansi.

Nam. 89

Ujenzi wa Barabara za Jimbo la Muyuni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Miongoni mwa kazi za Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni kusimamia ujenzi na matengenezo ya barabara zote nchini, lakini kwa muda mrefu Barabara za jimbo la Muyuni zimetupwa na Wizara hii.

(a) Je, serikali inaweza kuwaeleza wananchi wa jimbo la muyuni ni lini barabara zao zitajengwa.

(b) Je, serikali haioni kutojengwa barabara hizo, ambazo zinapitia katika maeneo ya ukanda wa utalii ni kudumaza maendeleo ya wananchi pamoja na sekta ya utalii katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake nambari 89 lenye vifungu a na b kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Pamoja na kwamba Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni hajazitaja barabara anazozilalamikia. Hata hivyo, napenda kumkumbusha Mhe. Mwakilishi kwamba jimbo la Muyuni ni miongoni mwa majimbo yenye mtandao mzuri wa barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hizo ni pamoja na ile iliyotoka Kitogani hadi Paje, nyengine iliyotoka Muyuni hadi Makunduchi, nyengine Makunduchi hadi Paje, Paje hadi Michamvi. Barabara ya Makunduchi – Paje, Paje – Michamvi ni barabara ambazo ziko katika ukanda wa utalii ambazo kwa kiasi kikubwa zinachochea maendeleo hayo nchini mwetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

(a) Barabara za Jimbo la Muyuni zimejengwa na zitaendelea kutunzwa ili kuimarika zaidi kama nilivyozieleza hapo juu katika mtandao mzuri wa barabara za lami jimboni Muyuni.

(b) Serikali imeshajenga barabara zote kubwa katika Jimbo la Muyuni. Hivyo kama kuna maeneo ya ndani yanahitaji huduma hiyo namuomba Mhe. Mjumbe awasiliane na halamashauri husika na wizara yetu iko tayari kutoa kila aina ya ushirikiano katika kufanikisha suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa wananchi wa Jambiani wa Jimbo la Muyuni sawa sawa na wananchi wa Ndijani kumetumika vigezo gani baraba ya Ndijani Jimbo la Chwaka ambao mwakilishi wao wale wakajengewa wakati wale wananchi wa Jambiani ambako ndiko kunakotoka pesa za sehemu kubwa ya utalii kigezo gani.

Vile vile unaweza kunambia barabara ya Ndijani shilingi ngapi zimetumika kujengwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika utoaji wake wa huduma haina upendeleo. Tumeeleza katika majibu mama kwamba Jimbo la Muyuni maeneo ambayo anayalalamikia Mhe. Mwakilishi hakuyataja moja kwa moja. Kwa hivyo, sisi kama wizara na kama serikali tumeeleza jitihada za serikali katika ujenzi wa barabara za lami hasa katika Jimbo la Muyuni kiujumla. Nina hakika kwamba kigezo kilichotumika kuwajengewa watu wa Ndijani ilikuwa ni kuona kwamba wananchi hawa wana usumbufu na eneo lao barabara yao kubwa yenye urefu takriban kilomita tisa ilikuwa haipitiki na serikali kwa kutambua tu kwamba haina upendeleo katika kutoa huduma hiyo ndio ikaona iwasaidie, kama vile ilivyoanza mwanzo kuwasaidia watu wa Muyuni kuwawekea barabara ya lami na watu wa Ndijani nao wana haki ya kupata huduma hiyo ya kujengewa barabara.

Lakini gharama kiasi gani zimetumika katika ujenzi naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwa maandishi.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, kwa kuwa kamati yangu ya PAC katika kazi zake za kawaida iliwahi kupita Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupata ufafanuzi wa suala hili, na kwa kuwa juzi tulikuwa na mswada wa ZBC na pia tulipata ufafanuzi mzuri naomba suala hili kuliondoa.

Nam. 80

Kuimarisha Shughuli za Utangazaji

(Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kabla ya kuliondosha swali langu naomba niishukuru Wizara ya Afya kwa utekelezaji wake kuziba mashimo yale yaliyokuwa mbele ya ICU na vile vile kuendeleza milango hiyo ikabaki kazi ndogo.

Vile vile Mhe. Spika, naomba uniruhusu kusema machache. Mhe. Spika, nisionekane mimi naisakama sana Wizara ya Afya nasema hapa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu cha 88 c , vile vile na Kanuni za Baraza la Wawakilishi ukurasa wa 34(1)(2) na hiki hata Mhe. Rais mwenyewe alipelekea mapema katika Wizara kutangazwa akataja Wizara ya Afya hakutaja kwa kuwa imeanzia *alphabe*t ya A kuona umuhimu wa Wizara ya Afya na vile vile ni mjumbe mimi katika Kamati uliyonipeleka ya Wanawake, Watoto na Ustawi wa Jamii. Sasa unapoliona ovu Mhe. Spika, unaambiwa utumie mdomo, wako, mkono wako na imani ya mwisho kulichukia. Mhe. Spika, kama nitayaona pale itabidi niyalete hapa vyengine vyote itabidi Kamati Mhe. Spika, mimi niondoshwe niweke pengine ni imani ya mwisho ya dini yetu ya Kiislam.

Mimi sina ugomvi na Dr. Sira ninacholeta hapa kuja kuwatetea wananchi, wajumbe wako wengi wanafikiri mimi ninamsakama Dr. Sira. Mimi sina kinyongo naye na niko tayari kushirikiana naye. Bi Mgeni shahidi wa suala hilo.

Nam. 109

Matengenezo ya Vyoo na Sakafu ICU

(Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Mhe. Spika: Mhe. Jaku tunakushukuru kwa kuonesha usafi wa nia yako lakini pia suali namba 109 limeondolewa.

Waheshimiwa wajumbe kabla ya kuendelea sasa naomba nitoe ile taarifa ambayo niliahidi nitaitoa baadae, Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kwamba siku ya Alhamis wiki iliyopita nilipokuwa natoa taarifa kuhusu kutakuwa na michezo 2, mchezo wa netball uliofanyika Gymkhana na mchezo wa mpira uliofanyika Amani, niliahidi kwamba timu zetu zitaleta ushindi mnono. Msije mkauliza kama na mimi nimo katika kamati ya Ufundi hapana, isipokuwa tunajua kwa juhudi za wanamichezo wangu zilivyo ushindi utakuja na hasa kwa upande wa mpira wa miguu tuna golikipa makini sana. Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambaye hauachii mpira hata siku moja umponyoke uingie kwenye nyavu. Kwa hivyo baada ya kazi nzuri iliyofanyika siku hiyo naomba sasa nitoe taarifa ya michezo yote hiyo miwili.

Waheshimiwa Wajumbe itakumbukwa kwamba, juzi tu siku ya Jumamosi tulikuwa na mechi ya kirafiki kati ya Baraza la Wawakilishi Sports Club na Bima ya Afya ya Dar es Salaam kwa michezo miwili tofauti. Matokeo ya michezo hiyo ni kama ifuatavyo:

Kwa mchezo wa football uliofanyika Amani matokeo ya mchezo huo yalikuwa, Baraza la Wawakilishi Sports Club imefunga 1 zito mwanana na Bima ya Afya haikupata kitu. Bao hilo zuri lilifungwa na mchezaji mahiri sana Mhe. Ussi Jecha Simai. Na kwa mchezo uliofanyika Gymkhana mapema siku hiyo, timu yetu ya Baraza la Wawakilishi ilipata magoli 39 na Bima ya Afya wakapata 19 tumekuwa mbele kwa magoli 20 kwa upande wa netball. Nataka nitoe hongera kwa upande wa wachezaji na wapenzi wote wa mpira wa Baraza la Wawakilishi na nikuombeni basi Waheshimiwa wanamichezo tuendelee kushiriki kwenye michezo na ni njia mojawapo ya kuimarisha afya zetu, umoja na urafiki. Waheshimiwa wajumbe naomba tupongeze ushindi mkubwa huo. Ahsanteni sana.

HOJA ZA KAMATI

Ripoti Maalum ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) juu ya Uchunguzi wa Utendaji wa Shirika la Umeme, Zanzibar

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa kabla hatujaanza majadiliano juu ya hoja hii ambayo iliungwa mkono siku ya Alkhamis naomba kwanza nitoe maelezo kidogo ili tujue namna gani tutaendelea na shughuli yetu hii na kiasi cha muda ambao tumebakia nao. Shughuli hii Waheshimiwa Wajumbe ilipangiwa siku mbili za kazi na kwa bahati nzuri ripoti yenyewe ni refu, muwasilishaji Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Omar Ali Shehe peke yake alitumia muda kama wa saa tatu na dakika arubaini na tano. Sasa hiyo ilikuwa muda wote wa siku ile na nyongeza yake juu.

Na ninashukuru tulitoa muda tukajisomee ili kujipanga vizuri ili leo tukianza kuchangia tuweze kuchangia tukienda *point* kwa *point* bila ya kuchukua muda mkubwa. Na nataka muelewe kwamba shughuli hii ilivyo imalizike kesho kipindi cha asubuhi kwa hivyo tujipange hivyo kwa sababu kesho hiyo hiyo kipindi cha jioni baada ya shughuli zitakazopangwa kwa kikao cha kesho ikiwa ni pamoja na ripoti ya serikali kuhusu Baraza la Manispaa na miswada kusomwa kwa mara ya kwanza, baadae tutamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atoe hotuba ya ufungaji wa shughuli zetu za mkutano huu. Hivyo niwaombe pale itakapofikia kwamba muda hautoshi nikielewa kwamba mtajipanga vizuri ili utoshe, itabidi hatimae tuwaombe nyinyi Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane kuongeza muda ilimradi ripoti hii ichangiwe vizuri kwa muda wa kutosha na hatimaye kuacha majibu kwa utekelezaji wake.

Basi baada ya hayo Waheshimiwa wajumbe tuanze majadiliano kwa kumkaribisha Mhe. Ali Salum Haji, na baadae Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa dhati kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia ripoti ya Kamati ya Kuchunguza Shirika la Umeme la ZECO. Kwanza kabisa nichukue fursa hii adhimu kuishukuru kamati kwa namna ilivyofanya kazi kwa umakini kabisa na kubaini mapungufu yanayoonekana katika ripoti yao.

Baada ya kuishukuru Kamati Mhe. Spika, mimi naomba nichangie katika maeneo mawili matatu. Na zaidi niende katika ukurasa wa 7 katika (8) uwepo wa makundi ya *state fuel* na ZECO. Lakini katika suala hilo hilo limejitokeza katika ukurasa wa 8 kifungu cha 8 wafanyakazi kutoridhika na *management* ya Shirika.

Mhe. Spika, niseme tu, kutokana na maelezo haya yaliyoonekana hapa na kama utaiangalia ripoti hii kwa umakini kabisa na ukifuatilia hali halisi ya maeneo mbali mbali basi tayari panaonekana kwamba hata katika shirika lenyewe kuna matatizo baina ya *management* na watendaji wa kawaida. Na hili Mhe. Spika, inapelekea kutofanya kazi kwa ufanisi, inapelekea kufanya kazi katika njia ya kutopendana na kutafautiana, lawama zilizokuwa hazina msingi.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwamba kwa sababu pamoja na matatizo ambayo yameelezwa ndani ya ripoti hii, lakini pia tukiri kwamba lina jitihada za kutosha katika kuleta ufanisi wa kuwapatia wananchi wake mahitaji ya umeme. Ni shirika ambalo kwa kweli kama utaliangalia lina kazi nzito, mambo yake magumu na niseme ambazo watu wengi hawapendi kufanya kazi. Kwa sababu hiyo Mhe. Spika, ninafikiri kama tungekuwa tunajaribu kufanya takwimu wa taasisi za serikali ambazo zinapoteza wafanyakazi wake kwa wingi sana au zilizokuwa na watendaji walemavu sana basi ninafirikiri kwa tathmini za haraka haraka Shirika la Umeme linaongoza. Hii inatokana na hali halisi ya kazi zenyewe, suala la umeme ni zito linahitaji umakini katika utendaji wake wa kazi na si kazi ambazo za kukurupuka ambazo mara nyingi unapofanya hivyo inapelekea watendaji kuathirika kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Spika, hii nasema kwamba sio kama hakuna tatizo matatizo yapo lakini nasema kwamba moja katika kitu ambacho nimekiangalia kwa makini zaidi nimeona hii athari ambayo wao wenyewe Kamati wameiona ya ukurasa wa 7, na wa 8 basi inaonekana kwamba ni moja katika mambo ambayo yamepelekea kutofanya kazi kwa ufanisi sana.

Mhe. Spika, katika hili mimi ninafikiri kuna haja nzima Mhe. Spika, ya kutafuta mbinu mbadala ya kuondosha zile kasoro ambazo zimejitokeza katika maeneo mbali mbali. Kasoro nyingi sana na ukiangalia mimi kwa kweli zinanipa tabu katika kuangalia. Kwa sababu kitu ambacho Mhe. Spika, kinanipa tabu ni kimoja tu, ni kile kitu ambacho tuangalie ukurasa wa 16 naomba ninukuu Mhe. Spika, kidogo. Bwana Mohammed Habib Suleiman wa Kigongo (Wambaa) hapa pana utata kwamba taarifa zake anasema yeye mwenyewe kauli yake amelipa milioni nane, lakini risiti aliyoandikiwa ni ya 167,320. Sasa mimi kinanipa utata Mhe. Spika, hivyo kweli katika taratibu za serikali kipi kinakuwa sahihi maneno au document ambayo ipo kwa yule muhusika. Mhe.Spika, ndio nikasema kwamba hii inanipa mashaka kabisa ile kauli ya sintafahamu ya kutokwenda sambamba kwa vizuri ule ukurasa wa 7 na 8 ya kuwa kuna tofauti baina ya *management* na watendaji.

Hii mimi ninaweza kusema Mhe. Spika, inaleta utata kutaka kuwaharibia baadhi ya watu kwa kitu kama hiki. Kwa kweli hii haiingii akilini. Mimi nikalipe pesa milioni tatu kwenye dirisha halafu nipewe risiti kwa mfano ya shilingi laki moja niondoke nayo pasipo kulalamika, pasipokutaka hatua za sheria zinakwendaje, Mhe. Spika, kidogo hapa ninapata kigugumizi. Na hii Mhe. Spika, ukiangalia iko katika maeneo mengi sana. Unakuta mtu analalamika anakwambia mimi nimelipa pesa hizi lakini risiti nimepewa hii, amefanya hatua gani au amekwenda kulalamika wapi hakuna, alikuwa anasubiri labda kamati teule ipite ndipo atoe maelezo yake. Naweza kusema inawezekana lipo na inawezekana halipo kwa sababu tunacho kama sisi ni *evidence* ya kitu chenyewe kilipo na risiti ndio inaonesha hiyo hali halisi.

Mhe. Spika, kwa kuendelea kuna suala jengine la Misali. Mhe. Spika, suala hili linanipa mashaka zaidi kwa sababu kama hii ambayo nimeielezea mwanzo Mhe. Spika, kwamba kunatokezea tatizo, lakini kunapotokezea tatizo taarifa juu ya tatizo lile huikuti. Kwa sababu Mhe. Spika, suala la Misali sijui kama tunaweza tukailaumu *management* moja kwa moja. Kwa sababu taarifa zake zinaeleza kwamba huyu mtu ameungiwa umeme, lakini umeme wenyewe hakuungiwa kwa utaratibu. Sasa mimi nilikuwa nataka kujua kwamba kama kuna *document* ambayo imeonekana ya huyu mtu ambaye hakufuata taratibu katika kulalamika katika taasisi. Sasa nasema kwamba ndio haya mashaka napata makubwa sana kwamba, yale yote ukiyaangalia

kwamba hukuti kama kuna barua ya malalamiko kwa yule mtu ambaye alipata tatizo ili kujua ile hali halisi ilivyo.

Mhe. Spika, nasema kwamba mimi naamini kwamba matatizo yapo lakini matatizo yapo sikatai moja kwa moja lakini matatizo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka. Na niseme kwamba taarifa imetusaidia vya kutosha, taarifa imetusaidia kwa sababu itatoa taaluma kwa wananchi wetu katika kufahamu taratibu za kisheria. Kwa sababu Mhe. Spika, kuna baadhi ya matatizo wananchi wanajitakia wao wenyewe, kwa sababu sheria za kuunga umeme shirikani zipo, utaratibu Mhe. Spika, upo sasa inakuwaje kuwatumia wale wajanja wao wenyewe Shirika la Umeme wanawajua wanawaita vishoka. Unamtafuta mtu wa kawaida mtaani unafanya mazungumzo naye halafu yeye ndio atumie utaratibu wa kuwatafuta wale watendaji wasio waaminifu katika kuungia umeme.

Sasa nasema imetusaidia hii taarifa kujua zile njia ambazo watu wanazitumia ili wananchi wetu basi wafuate zile taratibu ambazo zinastahiki. Mhe. Spika, mimi nilipongeze Shirika la Umeme hili suala wenyewe wameliona kwa kipindi kirefu na wamelibaini na wameamua kulifanyia kazi kabisa. Na kama utafuatilia shirika la umeme kuna suala ambalo wameliweka sasa hivi wa kufanya msako wa nyumba kwa nyumba wenyewe wanaita umeme day, kuwabaini wale watu ambao hawafuati taratibu za Shirika la Umeme na kuwatumia wale watu wanaoitwa ni vishoka.

Mhe. Spika, bado Kamati ninaipongeza kwa sababu imetusaidia mambo mengi sana na imeona mambo mengi ambayo kuna haja ya kuyafanyia kazi. Na niseme pia Mhe. Spika, katika hili wale ambao wameguswa kwa namna moja au namna nyengine baada ya serikali kukaa na kuangalia kubaini ukweli wa hali yenyewe basi niiombe serikali kuchukua hatua za haraka ili kuweka nidhamu bora katika shirika hili.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba kukaa kitako.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa fursa ya kuchangia maneno mawili matatu, kuweza kuwa pamoja siku hii ya leo na kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu kutupa afya ili kuweza kuendelea kufanya hivyo.

Pili nichukue fursa hii kuwashukuru Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Kamati yake nzima kwa kufanya kazi nzito na muhimu kwa taifa letu hili la Zanzibar katika kuhakikisha kwamba tunataka kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yetu.

Lakini tatu nichukue fursa hii kuwashukuru Wawakilishi wote ndani ya Baraza hili katika kutumikia wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika mambo yetu tunayojiwekea.

Mhe. Spika, mimi kwa kuanzia kutoa mchango ndani ya ripoti hii mimi sitokwenda kifungu baada ya kifungu, katika buku letu hili tulikuwa tumekabidhiwa tokea majuzi. Nimesikiliza kwa makini Mwenyekiti alipokuwa akiwasilisha hoja na maelekezo ya buku hili nimekwenda *page* baada ya *page* kuangalia kwa umakini vile vile na napenda kuthibitisha kwamba nakubaliana na maelekezo ambayo yamo katika buku hili.

Mhe. Spika, pamoja na makubaliano ambayo nakubaliana ambayo yameandikwa ndani ya buku hili lakini ningeliomba basi ripoti hii ambayo imewasilishwa hii ni ripoti imetengenezwa na wanadamu na imefuatiliwa na wanadamu vile vile. Lakini bado ninasisitiza kwamba uhuru ule wa wananchi au watendaji ambao wamezungumzwa katika buku hili kwa namna moja au nyengine napenda taratibu za kisheria ziweze kuchukua mkondo wake. Haidhuru kwamba kuna watu wameguswa moja kwa moja katika buku hili, na kuna watu wanaguswa kwa mujibu wa sheria na uwajibikaji kwa mujibu wa nafasi zao, tungelipenda Jeshi la Polisi na vyombo vyengine vinavyohusika kuchukua tahadhari na kwenda kufanya kazi kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka na kila ambaye ameguswa na tuhuma na hili liweze kuthibitisha liwe kosa kwa upande wake na aweze kutiwa katika hatia kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, ninazungumza haya kwa sababu ninafahamu kwamba Zanzibar inafuata utawala bora, katika nchi yetu ndio maana ninasisitiza kusema kwamba, pamoja na maelekezo ambayo yametoka humu ni vizuri kuangalia sheria zaidi.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia kifungu cha tano tu kifungu cha 1. 4.0 Hadidu Rejea. Kwa hadidu rejea hizi 6 ambazo zimeainishwa humu Mhe. Spika, ni kweli naweza kukubaliana na wana kamati kwamba kweli Shirika la Umeme kuna matatizo. Lakini matatizo yaliyokuwepo tunahitaji sana yathibitike kwa mujibu wa sheria isiwe taarifa hii ndio moja kwa moja inakuja kufunga wale wahusika tayari tukawahukumu kwamba tayari wana makosa kutokana na taarifa ambazo zimeletwa katika *document* hii naomba sana. Naomba taratibu za kisheria zifuatwe ili kuhakikisha kwamba anayetiwa hatiani ni yule ambaye baadae serikali isije ikapata matatizo na kupata hasara katika namna ya kuja kutafutana kulipana madeni yasiyokuwa na msingi wowote.

Mhe. Spika, mimi nimesikitishwa sana kuona kwamba katika Shirika la Umeme tufika pahala tukaona kwamba kuna watu ambao si waaminifu wameweza kwenda kuwaungia watu umeme na kuweza kupotea mabilioni ya mapesa, hili ni tatizo kubwa sana Mhe. Spika. Sasa naomba basi kosa ambapo litakuwa limethibitika ningeomba hatua za kisheria zichukuliwe juu ya wale wote ambao walikuwa wanahusika na suala hili. Wala sisemi kwa kitendo cha kuweza kuwachukulia hatua watu hawa kama labda watu hawa, kwamba tumewakosesha au tumewaelekeza sisi waweze kwamba labda wametumwa na vyama vyao waweze kufanya vitu kama hivi hapana, Niseme kwamba ilani ya Chama cha Mapinduzi haimuelekezi mtu kwenda kuiba, kwenda kufanya mambo yasiyokuwa na maana na kufanya mambo ambayo hayana msingi. Ilani ya Chama cha Mapinduzi na katiba zake zinaelekeza kwa umakini mno na kwa umahiri wa hali ya juu kabisa juu ya namna viongozi ambao wanapewa madaraka namna ya kuyatumia madaraka yale.

Katika viapo vyetu vya uaminifu ndani ya Chama chetu cha Mapinduzi Mhe. Spika, kuna maeneo yanasema kwamba sitotoa wala kupokea rushwa, rushwa ni adui wa haki. Lakini vile vile sitotumia cheo changu nilichopewa kwa manufaa yangu binafsi au kujilimbikizia mali. Haya ni mambo ambayo ni miongozo ndani ya Chama chetu cha Mapinduzi. Kwa msingi huo basi mimi ningeliona ni jambo la msingi sheria kuchukua mkondo wake wala masuala haya yasihusishwe kabisa na masuala ya siasa. Wale watendaji ambao wanahusika na kadhia hii ndio wawajibishwe kwa mujibu wa sheria. Ni juzi tu tulifanya mabadiliko ya uongozi mkubwa katika maeneo ya serikali katika Wizara hii. Inawezekana kama ilitokana na matatizo ya hapa na pale

katika kusimamia na kuendeleza maendeleo katika Wizara hii. Lakini bado nimeendelea kufadhaishwa na kusikitishwa kwamba kuna taarifa nyengine katika buku hili zingali ni *latest* kabisa bado zinaendelea.

Sasa inaonekana hii inatufahamisha kwamba hakuna kitu chochote kitakachowafika hata ikiwa wamefanya nini. Ningeomba sana wakati wa kukaa kustahmiliana, kuvumiliana, kuona kwamba huyu ni ndugu yangu, huyu ni shemegi yangu, huyu ni kaka yangu umepita sasa. Ni wakati sasa umefika kuhakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake na wazanzibari wanabadilika kama ambavyo Mhe. Rais anatwambia siku hadi siku tuachane na ile biashara ya *business as usual* twende katika mtandao wa kuona kwamba tunafanya vizuri kwa maslahi ya nchi yetu. Zanzibar ni yetu sote tukiiharibu tutaharibikiwa sote, lakini tukiitengeneza tutatengenezewa sote. Kwa msingi huo Mhe. Spika, ningeliomba sana hatua za kisheria zichukuliwe tena kwa umakini tena kwa haraka. Tuondokane na taratibu za kusema subiri, subiri, subiri. Kila tukiendelea kusubiri katika mambo yetu tunazidi kuharibikiwa, twendeni kwa mujibu wa alama za wakati zilivyo kwa sasa, bila ya kuwa makini mambo yatazidi kuharibika.

Baaada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kwa niaba yangu, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kikwajuni naomba kuwasilisha na naunga mkono maelezo haya. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja hii muhimu sana iliyo mbele yetu. Mhe. Spika, leo sauti yangu kama unavyoisikia haiko sawa na ingekuwa ni hoja za mchezo mchezo tu ningekaa kitako nikawaachia wenzangu wachangie, lakini ni hoja iliyo muhimu ina umuhimu wa aina yake. Kwa hivyo, na mimi nitumie nafasi hii kutoa mchango wangu juu ya kamati hii tuliyoipa kazi, Kamati ya PAC.

Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nikichangia Mswada unaohusu Vyombo vya Habari nilieleza masikitiko yangu juu ya kutokuwepo kwa rafiki yangu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo; kwamba ametuletea kazi yake lakini matokeo yake mwenyewe akawa hayupo, lakini na leo naona kama ni sura ile ile kwamba tunajadili hoja muhimu inayohusu chombo muhimu lakini waziri anayehusika na chombo hiki naye hayupo. Kweli Mhe. Spika, tunakuwa tunasikitika sana. Kwa sababu hapa tutayazungumza mambo mengi ya msingi ambayo Mhe. Waziri anayehusika na chombo hiki anatakiwa ayachukue na akaweze kuyafanyia kazi. Sasa haya mambo ya kukaimu tu katika mambo muhimu kama haya kwa kweli sisi yanatupa mashaka makubwa, yanatupa mashaka hata katika utendaji wetu wa serikali.

Mhe. Spika, mimi kwanza niipongeze sana Kamati ya PAC kwa kufanya kazi nzuri, wamefanya kazi tuliyowatuma, kazi hii Mhe. Spika, ni sisi tuliowatuma katika chombo chako. Tuliwaambia nendeni kalichunguzeni Shirika hili la Umma, Shirika la Umeme na Mhe. Spika, ukatoa hadidu rejea ya kwenda kufanyiwa kazi na ukatuuliza katika chombo hiki na tukaziunga mkono hadidurejea zile kwa hivyo, imepata ridhaa na Baraka zote za chombo hiki cha wananchi. Leo tunashukuru sana kazi hii ngumu wenzetu hawa wameikamilisha na wametuwasilishia mbele yetu ili tuijadili na baadae tutoe maoni yetu. Kwa hivyo, mimi naipongeza sana kamati hii iliyofanya kazi hii ya umma.

Mhe. Spika, pia nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, Mhe. Omar Ali Shehe. Mhe. Spika, kazi ya uwenyekiti katika kamati hizi hasa Kamati Teule ni kazi ngumu. Mimi katika kamati Mhe. Spika, uliyoiunda ya kuchunguza Baraza la Manispaa wenzangu walinipa nafasi ya kuwa mwenyekiti wa kamati ile, nilikataa sana wakati waliponiteuwa, lakini hatimaye ikabidi nikubali. Kwa sababu walinambia lazima uwe mwenyekiti wa kamati hii. Kwa hivyo, suala la kuwa mwenyekiti katika kamati teule si jambo la mchezo, kwa sababu jambo hili kwanza linakuwa la Baraza zima, baadae linakuwa la kamati, lakini hatimaye linaishia la mwenyekiti. Watu wote sasa wanakunyooshea mwenyekiti kama vile yale uliyoandika pale yote umekaa nyumbani kwako ukayaandika ukatuletea, kumbe kwanza ni maamuzi ya Baraza na yanapigiwa kura lakini na kamati ina kaa na kufanya kazi hatimaye pale mwenyekiti anaunganisha na kuwasilisha kwa niaba ya wenzake. Kwa hivyo, nakupongeza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti nakupongeza kwa sababu hii ni kamati yako ya pili, umefanya kazi katika kamati yako ya kwanza na nikadhani kamati hii utakataa, lakini kwa ujasiri na uhodari wako ukakubali kubeba tena mzigo huu. Nakuomba uendelee kubeba mizigo hii ya wananchi ili tuone serikali yetu na chombo hiki kinakwenda vizuri.

Mhe. Spika, mimi baada ya kumsikia mwenyekiti nilikuwa makini alipokuwa akiwasilisha muhtasari kwa sababu ule ni muhtasari tu wa ripoti ile nilikuwa makini. Lakini pia tumepata wenyewe vitabu vyenyewe nafasi ya kupitia katika hadidurejea mbali mbali hadidurejea sita. Jambo lililonisikitisha na ninalolilalamikia sana juu ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, jambo hili kwa kweli limenisikitisha sana, kwamba chombo hiki cha umma ambacho kimewekwa kwa ajili ya kuchunguza matumizi ya serikali, kudhibiti fedha za umma kipo lakini leo kamati kama hii ambayo imeundwa na watu ambao si wataalamu ni wanasiasa wanakwenda kuchunguza katika taasisi kama hii ya umma na kugundua madudu ya mamilioni ya pesa.

Kwa kweli Mhe. Spika, inasikitisha sana, nimuombe waziri anayesimamia ofisi hii ya CAG awe makini na chombo hiki kwa kweli tumeshaanza kuwa na mashaka makubwa kwamba madudu yaliyogundulika na kamati hii ya waheshimiwa ambayo haina wataalamu imeweza kugundua mambo mengi ya msingi tukaacha PAC hatujaona chochote katika jambo hili kwa kweli inasikitisha na wanatutia mashaka. Afisi hii inatupa mashaka makubwa katika kudhibiti mali za wananchi, katika kudhibiti mali za umma. Wamekuwa wakituletea ripoti hapa za kubabaisha babaisha tu hapa kila mwaka wanambabaisha Rais.

Kwa sababu ripoti zile wanazotuletea hapa wanazipeleka kwa Rais, Rais anaangalia, anatazama, anatuletea tunaona vishilingi vile na visenti senti lakini kumbe kuna mamilioni ya pesa yanapotea. Kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha na tunailaumu sana Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutokufanya kazi zake, hawako makini katika kusimamia mali za umma. Mhe. Spika, hili mimi limenisikitisha sana na tuwaombe sana hawa wafanye wajibu wao na kwa sababu kufanya hivi wanakuwa wanatutia mashaka.

Mhe. Spika, ripoti hii imeeleza mambo mengi na nikianza kulichukua moja moja huu muda wako wote unaweza ukamalizika, lakini nitaeleza tu baadhi ya maeneo ambayo wameyazungumzia, wameyafanyia uchunguzi na kuyatolea maelezo katika ripoti hii.

Mhe. Spika, katika hadidurejea ya kwanza kuna fedha hizi zilizolipwa na mmiliki wa Hoteli ya Pemba Mesali, Ndugu Amani Ibrahim Makungu shilingi 37,720,000 fedha ambazo kwenye shirika hazikwenda kama zilivyolipwa. Zimelipwa shilingi milioni mbili sijui kitu kama hicho, ina maana shilingi 35 milioni watu wamekunywa. Hii ni hatari Mheshimiwa na fedha hizi zilikuwa zinatiririshwa katika *account* binafsi ya mfanyakazi wa shirika. Shirika hili tutalimaliza, nchi hii tutaimaliza kuitafuna wananchi wanahangaika, vijisenti vyao wanahangaika kwenda kulipa umeme, gharama za umeme zimekuwa juu, zimekuwa kubwa huku visingizio vikiwa kwamba gharama za uendeshaji kubwa kumbe gharama zenyewe za uendeshaji ni watu kujichukulia fedha wakaingiza mifukoni mwao, hii ni hatari Mhe. Spika, na hili halikubaliki fedha hizi lazima zirejeshwe katika shirika, wale wote waliohusika na wizi huu fedha hizi wazirejeshe na tupate taarifa juu ya kurejeshwa kwake.

Jengine Mhe. Spika, suala la kuungiwa umeme katika maeneo mbali mbali. Hili nalo ni kadhia kubwa, mahoteli ya wawekezaji tunajua Mhe. Spika, ni mahoteli ambayo yapo hapa kwa ajili ya kunyanyua uchumi wan chi yetu katika maeneo mbali mbali na katika nyanja mbali mbali. Leo inasikitisha kwamba kuna mlolongo wa mahoteli hapa wanaungiwa umeme bure bure tu hakuna stakabadhi hakuna utaratibu hakuna fomu zinazotolewa, mtu anaungiwa umeme maeneo makubwa halipi hivi sisi tutegemee nini katika shirika hili.

Kwa kweli jambo hili linasikitisha mno kwamba mahoteli wanaungiwa umeme bure na hatusemi kwamba wanaungiwa umeme bure, bure kwa maana fedha hizi haziingia katika shirika, fedha zile ambazo zinastahiki kuingia katika shirika zinaingia mifukoni kwa watu huku kukiwa na uongozi wa shirika Meneja yupo, *Management* ipo, Bodi ya Shirika ipo fedha mamilioni kwa mamilioni yanaingia katika mifuko ya watu.

Hili halikubaliki Mhe. Spika, kabisa kabisa na hili ni shirika moja tu ambalo tumelifanyia kazi, lakini hebu tujiulize mashirika haya yako mangapi Mhe. Spika, taasisi hizi ziko ngapi, hivi leo kama Baraza lako tukufu likaamua kwenda katika taasisi hadi taasisi tutagundua madudu mangapi, halafu leo tunalia umasikini lazima tutakuwa masikini sisi wa kudumu na kama tutaendelea kuvumiliana na kustahamiliana na kuwa na mihali juu ya mambo haya *Wallahi* Mhe. Spika, hatufiki paala. Tumekuwa na tabia ya mambo haya kuyanasibisha na vyama vyetu vya siasa.

Mwenzangu katangulia kusema hapa kwamba sisi Chama chetu cha Mapinduzi bwana katiba yake iko wazi, ilani yake iko wazi. Chama cha Mapinduzi kinapingana na yote haya yaliyofanyika, haya si watu wema hawa sio waaminifu kwa nchi hii. Kwa hivyo, tusiyanasibishe masuala haya na vyama vyetu vya siasa anayefanya mambo haya ni uroho wake.

Mimi Mhe Spika, sijakaa hata siku moja katika vikao vyetu vya Chama cha Mapinduzi tukipewa ripoti ya matumizi na mapato ya chama yakionesha kwamba pesa hizi katoa Bwana fulani au zimetoka kwenye shirika fulani kwa ajili ya kuimarisha kampuni, hilo sijaliona, hivyo naamini kama mwenzangu aliyetangulia kusema. Kwa hivyo, naamini kwamba fedha hizi ambazo hawa watu wasiokuwa waaminifu wanaingiza mifukoni mwao wanakula wenyewe. Mhe. Spika, huwezi kunasibisha na masuala haya ya wizi na ubadhirifu wa mali ya umma ukayanasibisha na vyama vyetu vya siasa. Chama kinahimiza uaminifu, kinahimiza uadilifu na uajibikaji katika nchi hii.

Mhe. Spika, nilipokuwa nikipitia ripoti hii niliona jina moja nilishituka, Shumbana Amani Karume, mwanzo nilijiuliza huyu Shumbana ndiye huyu mtoto wa Rais wetu Mstaafu au ni mwengine, ambaye ripoti inamuonesha kwamba, ameungiwa nguzo 31 na *transformer* katika nyumba yake, eneo kubwa na hakuna malipo yoyote yaliyokuwa yamefanywa. Mhe. Spika, hili ni jambo la kusikitisha ni aibu, hatuwezi kutumia madaraka yetu namna hii.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kuvutiwa umeme katika eneo la Paje navusha njia kutoka nguzo hii mpaka nguzo hii na *transformer* ni nguzo moja tu, nikawaambia watu wa Shirika la Umeme waniletee hesabu. Hesabu waliyoniletea ilikuwa ni shilingi 32 milioni, nguzo moja haitimii vizuri, shilingi 32 milioni. Leo kuna nguzo 31, moja mpaka 31 hakuna malipo *free of charge* na *transformer* juu kwa kweli inasikitisha na jambo hili lazima tulipige vita. Haiwezekani kwamba, watu wanatumia madaraka katika kuitafuna hii nchi, huwezi kutumia madaraka kwa kutafuna nchi huku wananchi wetu wakiwa wanyonge wanahangaika na fedha za umeme.

Sisi wawakilishi tunapiga kelele juu ya kupanda kwa gharama za umeme, wataalamu wa umeme wanatwambia umeme umekuwa ghali haulipiki, tumekuwa na madeni makubwa TANESCO kwa sababu ya mambo kama haya tunaambiwa hatuna uwezo wa kulipa kumbe tuna uwezo wa kuchukua fedha tukaingiza mtu katia mfukoni mwake. Tuna uwezo wa kuwaungia umeme watu bure.

The Residence Hotel imeungiwa umeme nguzo sijui ngapi la kusikitisha Mhe. Spika, kwa mujibu wa sheria ya ZECO mamlaka ya kuunga umeme hapa ni yao, leo inasikitisha Kampuni imetokea Tanzania Bara imekuja kuunga umeme hapa na kampuni inaulizwa juu ya jambo lile wanasema sisi hatujui. Hivi kweli Mhe. Spika, unaamini kwamba Shirika la Umeme halijui kama kuna kampuni imetoka Bara imekuja kuunga umeme hapa, kweli shirika halina habari. Lazima waliohusika wote wawajibike na fedha zilizopotezwa zote katika mahoteli lazima zilipwe na sheria lazima ichukue mkondo wake.

Mhe. Spika, meneja wa shirika hili hana uwezo wa kuongoza hili shirika, sikubaliani kwamba mambo haya yanafanyika na yeye yupo. Shirika hili liko chini ya uwezo wake, chini ya milki yake. Humu Mhe. Spika, mna mambo mengi hatuwezi kuyamaliza.

Internal Auditor Pemba anatoa ushauri kwa Meneja juu ya udhibiti wa fedha namna ya kukagua fedha, *internal auditor* anahamishwa kutoka Pemba analetwa Makao Makuu ili aachane kabisa na kuingilia mambo ya fedha, leo *Internal Auditor* hayupo Pemba watu wanakula fedha.

Mhe. Spika, katika eneo ambalo linatumika kwa fedha za umma ni Kisiwa cha Pemba, kule kumekuwa ndio kichaka cha wizi wa fedha za umma. Nakumbuka wakati wa ripoti ile ya mishahara hewa basi mishahara hewa ilikuwa inatolewa zaidi Pemba, watu wanapitia Pemba wanaona labda wale wamejitenga hakuna udhibiti. Pemba lazima kuangaliwe sana na ndugu zangu Wapemba lazima muwe makini sana, watu wanatoka hapa wanapitishia pesa Pemba wanachukulia huko halafu majanga yale yanakuangukieni wao wanakula nchi, hii inasikitisha.

Jengine Mhe. Spika, linalosikitisha *account* moja ya Pemba kila siku inaingiziwa shilingi milioni mbili, kila siku pesa zinazokusanywa za kodi inaingiziwa shilingi milioni mbili kwenye *account* moja, ambapo fedha zile zinachukuliwa zinaambiwa ni za matumizi ya kawaida ya kila siku.

Wanakuja watu kuuliza sasa hizi pesa mmepewa kwa ajili ya matumizi ya kila siku sasa hebu tupeni huo mtiririko wa matumizi yenyewe hakuna mtiririko wowote. Kwa sababu pesa zinaingizwa, zinatolewa watu wanagawana; zinachukuliwa zinaingizwa watu wanagawana shilingi milioni mbili kwa mwaka kiasi gani, ni pesa za umma za wavuja jasho hao tunaowalipisha umeme kwa bei ya juu.

Kwa kweli Mhe. Spika, bei ya umeme ni kali sana. Sisi Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi tunashukuru serikali inatulipia umeme, lakini wananchi kule watalipiwa na nani, wale walala hoi kule watalipiwa na nani na sisi tukimaliza kazi hii tukitoka tukienda ng'ambo tutalipiwa na nani umeme. Mimi naamini Mhe. Spika, kwa hesabu hizi ambazo wenzetu hawa wamezigundua au wizi huu ambao wameugundua kuna pesa nyingi sana zinapotea pale ambazo pengine hata bei hii ya umeme tunaolipa sasa hivi isingefika katu. Wanatwambiwa watatuongezea bei ya umeme kwa *installment,* kila mwaka asilimia fulani tutaongeza hatujafika kule tunakokwenda halafu huku pesa wanaingiza mifukoni mwao hili halikubaliki. Tuitake serikali kabisa ichukue hatua juu ya wote waliohusika katika kadhia hii.

Serikali imekuwa na tabia ya kutwambia sisi washauri, nyinyi Baraza maana yake washauri, hebu watueleze wapi palipoandikwa kwamba Baraza hili ni Baraza la Ushauri. Serikali itwambie katiba hii hapa tunayo, ni wapi tulipoandikiwa sisi Baraza la Wawakilishi ni Baraza la Ushauri, sisi sio Baraza la Ushauri hili ni Baraza la Maamuzi, hiki ni chombo cha maamuzi kwa wananchi na maamuzi yanayotoka hapa serikali ina wajibu wa kuyatekeleza kwa mujbu wa katiba.*(Makofi)*

Kwa hivyo, tunataka mambo haya yachukuliwe hatua. Mimi nakubaliana na ripoti hii iliyoandikwa na hatua zichukuliwe na wale waliochukua fedha za umma wazirejeshe haraka na wakiwa hawakurejesha fedha hizi wachukuliwe hatua za kupelekwa Mahkamani.

Mhe. Spika, namalizia nisichukue muda wako mwingi, ripoti hii imejaa mambo mengi, lakini namalizia suala la majenereta ambalo katika hadidurejea tuliyowapa kamati ilikuwemo suala la majenereta 32. Hii inasikitisha sana Mhe. Spika, inasikitisha kuona wenzetu wafadhili Norway, Sweden na Uingereza wameweza kutuonea huruma wakatusaidia fedha zaidi ya shilingi milioni moja na laki mbili kwa ajili ya kuondokana na kadhia ya kuzimika kwa umeme katika nchi hii, tukaweza kwenda kununua majenereta ili tuondokane na matatizo. Inasikitisha sana kwamba majenereta yale yaliyonunuliwa sasa hivi hayana manufaa yoyote kwa wananchi, hili linasikitisha sana.

Mhe. Spika, majenereta yale ingekuwa yana manufaa basi hata hii kadhia ya kuzimiwa umeme kwa masaa isingekuwepo kabisa, wala machungu haya ya kuzimiwa umeme wananchi wasingeyapata kama fedha zile tulizopewa na wahisani tungezitumia kwa uaminifu. Lakini kinachoonekana ni kwamba hakukuwa na uaminifu katika kuzitumia fedha zile, hakukuwa na uadilifu.

Ripoti hapa inasema kwamba, majenereta yale hayakununuliwa kwa mujibu wa taratibu tulizokuwa tumejiwekea, nchi hii Mhe. Spika ina taratibu zake za matumizi, ina taratibu zake za manunuzi, ina taratibu za kila kitu na unapokiuka taratibu za manunuzi maana yake wewe una lako, kwa nini ukiuke utaratibu wa manunuzi na utaratibu unaujua. Ni kwamba unapotaka

kununua kitu ufanye utaratibu huu na huu mpaka kile kitu kinapatikana leo kumekuwa na lugha za kubabaisha tu hapa huyu anasema hivi, huyu anasema hivi, haieleweki Mhe. Spika.

Majenereta yako pale tuyafanyie nini yale, pesa zimepotea, watu wameingiza pesa mfukoni leo shirika linafika pahala linapigwa adhabu ya shilingi 31 milioni kwa kutokuwajibika vizuri kwa uzembe tu, hizi fedha zimelipwa kwa uzembe tu na mimi nina wasi wasi sijui kama hakukuwa na njama juu ya kuzipata hizi pesa, huwezi kusimamia jambo katika utaratibu kama huu unatia mkataba na mtu mwengine unakwenda kumpa mtu mwengine, ukisha unamrudia huyu, huyu anashtaki anakupiga faini unaharakisha kulipa. Pesa hizi shilingi 31 milioni wamegawana Mhe. Spika, na hizi lazima zilipwe.

Mimi nadhani Mhe. Spika, wanafikiri tunapozungumzia shirika labda wanafikiri zile pesa ni mali yao, zile ni pesa za umma tunalipa sisi, wananchi wanalipa umeme, hizi ni pesa za umma. Shilingi milioni 31 milioni ambazo Bodi iliyokuwa ikisimamia imesababisha hata kama sio Wajumbe wa Bodi walipe pesa hizo, hata kama muda wao ushamalizika walipe, Bodi ile iliyokuwa ikiongozwa na Moh'd Hashim ilipe.

Leo mwenyekiti wa bodi tumekupa zamana ya kuongoza ZRB Bodi ya Mapato ambayo ni kiungo halafu unakwenda unapewa na umeneja unapewa na dhamana ya kwamba wewe ndio mwenyekiti wa bodi ya Shirika la Umeme halafu kule unafanya mambo haya huku unafanya nini, hii dhamana uliyopewa ya kukusanya fedha unafanya nini. Tutaunda kamati kuchunguza ZRB, tutaleta hoja ya kuichunguza ZRB kwa sababu tumeshakuwa na mashaka na hata kama mtu hayupo atawajibika na sheria itachukua mkondo wake, haiwezekani tupelekwe katika njia hii na katika utaratibu huu.

Mhe. Spika, mimi nina mengi ya kusema ripoti hii imejaa mambo mengi, na sauti yangu kama unavyoisikia inazidi kwenda chini. Lakini ninachosema nakubaliana na hoja hii na niwaombe wenzangu wakubaliane na hii. Kwa hivyo, humu kwa mujibu wa ripoti iliyoandikwa kwamba Waheshimiwa Wajumbe au Baraza hili limeombwa na kamati kwamba tuitake serikali itekeleze haya.

Mimi natofautiana na wenzangu waliotangulia, ripoti hii ikafanyiwe kazi wala haina haja tena ya kupelekwa kwenye vyombo vyengine, anayetakiwa kushtakiwa apelekwe Mahkamani atakwenda kujitetea Mahkamani. Narudia, uchunguzi tayari umeshafanywa na chombo hiki kwa hivyo, hakuna haja tena ya uchunguzi mwengine, aliyeambiwa ashtakiwe apelekwe Mahkamani kama utetezi atakwenda kuupata Mahkamani. Kitendo hiki cha kuambiwa maana yake sisi serikali tuchunguze kwanza ni cha kubabaisha. Tumeona ripoti ya kwanza hapa, haikuwa na jawabu nzuri, wananchi wanailalamikia. (Makofi).

Hii ripoti kila aliyeguswa wa kushtakiwa ashitakiwe na wakulipa alipe, kama utetezi ataufanya Mahakamani katika vyombo vya sheria, kwa sababu ripoti hii huwezi tena ukaiundia kamati nyengine. Kama walikuwa na uwezo wa kuunda kamati wao wangeunda kuchunguza lile shirika. Hii ni ripoti lililokuwepo hivi sasa ni utekelezaji ni agizo.(Makofi).

Mhe. Spika, mimi nilikuwa ni mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza Baraza la Manispaa. Wananchi walikuwa wananiuliza, kuna kipindi fulani walinitaka nihojiane nao kupitia

Televisheni Zanzibar. Nikawaeleza masuala yote waliyokuwa wakiniuliza wale wananchi kwa njia ya simu.

Wananiambia mbona inaonekana hakuna hatua zozote zinazochukuliwa juu ya ripoti zenu, nyinyi kama Baraza la Wananchi muna *role* gani katika hizo ripoti, mbona inaonekana hamna munatumia pesa nyingi munachunguza mukipeleka pale serikalini mambo yanakwisha tu, watu wote kila mmoja alikuwa ananiuliza kuhusu hoja hiyo.

Nikawaambia sisi kama Baraza la Wawakilishi tuna *role* ya Kikatiba, Makamu wa Pili wa Rais, Mawaziri, kwa pamoja watawajibika katika chombo hiki na hiyo ni Katiba ndio iliyoelekeza. Hapa ndipo Katiba ilipotupa mamlaka, mawaziri wote wa serikali chini ya Makamu wa Pili wa Rais watawajibika hapa. Nini maana ya kuwajibika. Maana yake kuwajibika ni kutekeleza yale yanayoamuliwa hapa na kama hutowajibika, maana yake unatakiwa uajibishwe. (Makofi).

Kwa hivyo tunasema kwamba ripoti hii ikafanyiwe kazi, tunataka baada ya miezi mitatu iliyotolewa serikali ituletee utekelezaji wa yale yaliyoelezwa wa kupelekwa Mahakamani tuambiwe wameshapelekwa Mahakamani, kama wa kutoka akatoke Mahakamani, wakulipa tuambiwe amelipa kama hajalipa apelekwe Mahakamani, maana ni wizi wa mali ya umma na wale wote waliohusika kwa namna moja au nyengine katika kadhia hii ni lazima serikali ichukue nafasi yake kuona kwamba vyombo hivi vinafanyakazi kwa manufaa ya wananchi, sio vyombo hivi vinafanyakazi kwa ajili ya kuiingiza fedha mfukoni. (Makofi).

Mhe. Spika, naunga mkono hoja na mimi nakubaliana nayo asilimia mia kwa mia na nawaomba sana Waheshimiwa wenzangu kuwaambia kwamba ripoti hii ni yetu, chombo hiki tumekiunda wenyewe, shirika hili ni la umma linahudumia kila mtu, shirika hili ni muhimu, umeme ni muhimu sote tunaujua umuhimu wa umeme, tumeshazimikiwa hapa umeme miezi mitatu hatuna umeme, kwa hivyo tutaka shirika hili lifanyiwe marekebisho makubwa ili liwe ni tumaini kwa wananchi wa Zanzibar.

Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana. Nimeona bora nichukue fursa hii ili kuondosha wasi wasi kwamba Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji, na Nishati kuwa hayupo labda kwamba amedharau kikao hichi laa.

Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban hayupo nchini, yupo Ethiopia ameungana na ujumbe wa Mhe. Rais Kikwete katika kuwasilisha ripoti ya Tanzania kwenye ile kazi ya APRM. Ameungana na ujumbe ule lakini sasa kutokuwepo kwake haina maana kwamba wizara haipo, haina maana kwamba serikali haipo, tuna utaratibu wetu wa serikali akiondoka waziri mmoja anakaimu mwengine.

Mhe. Waziri Mohamed Aboud Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiye Kaimu Waziri na Naibu Waziri yupo. Kwa hivyo Mhe. Spika, na ruhusa maaluma kaomba kwako mwenyewe binafsi na serikalini.

Kwa hivyo naomba ifahamike kwamba kuondoka kwake sio kama hayupo kienyeji, kaondoka kwake rasmi na serikali ipo na wizara ipo, tupo tayari kupokea michango.

Ahsante sana Mhe. Spika. (Makofi).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu kutokana na hii ripoti iliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia fursa hii baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii. Pili niipongeze hii Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya. Na katika hili Mhe. Spika, nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikukupongeza wewe kuwa makini katika kuteuwa hii Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC).

Kwa kweli ulikuwa makini katika kuteuwa na kwa kweli kazi waliyoifanya hii kamati ni kazi nzuri sana na imetupa muongozo Mhe. Spika. Imetupa muongozo na kutupa taaluma Waheshimiwa Wawakilishi kwamba kazi yetu sisi sio tu kupitisha bajeti ya serikali na mishahara ya watumishi, aah! ni pamoja na kuangalia matumizi mazuri ya fedha za walipa kodi wa nchi hii.

Kwa vile ripoti hii Mhe. Spika, imeweka bayana jinsi ya ubadhirifu wa fedha za wavuja jasho wa nchi hii zinavyomumunywamumunywa na hawa mchwa. Kwa hivyo Mhe. Spika, naipongeza kamati kwa kazi nzuri kwa vile wametuwekea bayana ubadhirifu wa fedha zetu, hivyo hongereni sana.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii vile vile kabla sijaingia kwenye hoja, kuungana na Mhe. Salmin nimpongeze sana kwa mchango wake ambaye ni mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi. Kwa kweli ingelikuwa hakuna demokrasia humu kwenye Baraza tungesema mchango wake unatosha. Maana yote kayamaliza yeye Mhe. Salmin Awadh Salmin lakini kwa vile imekuwa ni sababu tumekuwa na demokrasia ya kutosha na kila mtu ana uwezo wa kutoa mawazo yake basi na sisi tunatia nyama tu, lakini Mhe. Salmin mambo haya ameyamaliza kabisa na ndio maana Chama cha Mapinduzi wakampa unadhimu, na wala wasiwe na wasi wasi wakiwa wana tatizo la Katibu Mkuu pia ana uwezo wa kazi hiyo (Makofi).

Mhe. Spika, sasa niende kwenye hoja Shirika hili la Umeme (ZECO) ni shirika la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Linaendeshwa kwa fedha za walipa jasho wa nchi hii na dhamira kubwa ni kutoa huduma kwa walipa kodi, sambamba na kuipatia mapato serikali yetu.

La kusikitisha Mhe. Spika, shirika hili limekuwa ni Muumiani. Kwa mujibu wa ripoti hii ni Muumiani. Muumiani ni wale wanaonyonya damu lakini hawa wanafyoza fedha zetu kwa maslahi yao binafsi na sio kwa maslahi ya umma.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huu naungana na ripoti hii asilimia mia kwa mia kwamba yeyote ambaye amehusika na ubadhirifu wa fedha hizi za walipa kodi, basi vyombo vya sheria vichukue hatua. (Makofi).

Mhe. Spika, ukenda katika ukurasa wa 15 wa ripoti hii utaona dhahiri kwamba shirika hili haliwatendei haki Wazanzibari wote, linawabagua. Kwa mujibu juzi tulivyoelezwa hapa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni kwamba katika jambo ambalo linalohimizwa katika nchi hii ni umoja na SMZ haina ubaguzi. Alitetea sana Mhe. Waziri na mimi nakubaliana na yeye.

Lakini la kusikitisha hawa wenzetu wanakwenda kinyume na msimamo wa serikali yetu. Kwa mfano tuangalie ukurasa wa 15 wa hii ripoti. Mhe. Spika, kwenye ukurasa huu, kuna mama mmoja anaitwa Zuhura Nassor, yeye aliuziwa umeme kwa masafa ya nguzo moja na *loophole* kwa shilingi milioni moja laki mbili na thalathini na sita elfu, mia saba na arobaini na saba na senti mbili.

Masafa hayo hayo, aliungiwa bwana mmoja wa Chokocho Ali Mohamed Sadi kwa shilingi laki nne na arobaini na nne elfu kwa masafa hayo hayo, nguzo moja na *loophole*.

Sasa mbona wapo *bias* kiasi hiki, mbona wanawabagua walipa kodi wa nchi hii kiasi hiki. Huu ni udhaifu mmoja na kwa vyovyote wote hawa Mhe. Spika, hawasaidii serikali. Hivyo na pesa hizi hatujui hii tofauti iliopo kwamba inaingia serikalini au inamung'unyuliwa mung'unyuliwa kama vile mchwa anavyomung'unya kigogo.

Mhe. Spika, sisi hapa tuna utaratibu kwamba serikali yetu inawasomesha vijana wetu au wananchi wetu wanasoma kupitia Bodi hizi za mikopo ya Zanzibar na Bodi ya Mikopo ya Tanzania Bara. Fedha zile zinachukuliwa kwa kukopwa. Kwa hivyo kila Mzanzibari ananufaika na pesa anayoikopa katika Bodi ya Mkopo kwa sababu akimaliza fedha ile inazungumza ni rotating fund.

La kusikitisha Mhe. Spika, shirika kwa mujibu wa ripoti hii imemuagharimia mama mmoja *pound* elfu tatu na mia sita kwa kozi ya *Advance Diploma* ambayo inapatikana hata hapa SUZA na kwengine hapa nchini inapatikana. Sasa haya sio matumizi mazuri ya walipa kodi na fedha ile ni kwamba hairudi. Sasa Mhe. Spika, mimi naomba hizi *pound* elfu tatu mia sita, huyu jamaa zirudi hizi na hatua nyengine zichukuliwe za kisheria dhidi yake.

Mhe. Spika, kuna fedha ambayo kama mwenzangu aliyoitaja hapa aliyotoa Bwana Makungu pale pamoja na Munawar House. Bwana Makungu alilipa elfu thalathini na saba T. Shillings. Risiti ikaandikwa chini ya milioni tatu. Munawar na yeye akalipa fedha karibu milioni kumi na sita, lakini risiti ikaandikwa hivyo hivyo milioni moja na kidogo.

Kwa hivyo kuna kama milioni arobaini za hawa tu wafanyabiashara wawili tu hao zilizoingia katika mfuko wa watu binafsi. Mhe. Spika, huku ni kuwaibia. Hawa hawatofautiani na mtu anayevunja benki. Kuzichukua pesa za walipa kodi karibu milioni arobaini kwa watu wawili tu ukazitia mfukoni mwako na kuinyima serikali mapato, huu ni uhaini. Naomba Mhe. Spika, niungane na mheshimiwa mwenzangu kwamba hawa wachukuliwe hatua na hizi fedha zirudi.

Mhe. Spika, la kusikitisha zaidi ni kwamba kuna hii kampuni inayoitwa GECO. GECO imeelezwa sana katika ukurasa wa 52 hapo kwamba inafanya kazi ya kuunganisha umeme katika minara ya simu. Hii kazi ingefanywa vizuri na ZECO lakini nakwambia hawa jamaa zetu wa shirika, nimeiona humu kwenye taarifa kuna wafanyakazi wana hisa. Sasa inaonekana hizo kazi zote kwamba kazi za ZECO zenye maslahi wanaziingiza kwenye kampuni yao binafsi ili kujikupatia mali ambazo ni fedha zetu. Hawa Mhe. Spika, si waajiri waaminifu hata chembe kwamba wamejiingiza kwenye GECO, fedha za mabilioni kwa sababu kuna minara karibu arobaini na sita ile serikali ingeweza ku-connect ile karibu milioni mia mbili, kwa sababu ni milioni mia moja na thamanini kazi walizozifanya katika kujenga minara GECO, leo zimeingia katika GECO pesa hazikuja serikalini.

Mhe. Spika, hawa wanaturudisha nyuma, milioni mia mbili hizi zingeingia serikalini zikawagusa walipa kodi wa nchi hii, ninakuhakikishia tungeweza kuwafundisha walimu wa sayansi ya diploma na digrii hapa na halafu wale Wanigeria tungewarudisha kwao, tusingekuwa na haja ya kuwaagizia Wanigeria hapa.

Hawa wanaturudisha nyuma katika kila upande. Leo hii hatuna walimu wa sayansi, vijana wapo hatuwasomeshi kwa sababu hatuna fedha. Leo milioni mia mbili hizi zinachukuliwa na GECO tu. Huu ni wizi Mhe. Spika, na hawa lazima kwa mujibu wa ripoti hii basi sheria ichukue mkondo wake. (Makofi).

Tena namuomba sana Mhe. Rais, nina imani sana na yeye na serikali yake na ni mtii wa serikali yake. Hawa watu wa ZECO hawana shukurani Mhe. Spika, kama kuna watumishi wanaopata mishahara mikubwa katika nchi hii na wao wamo, lakini matokeo yake wanatuibia namna hii. Sasa hii ripoti imeshapatikana Rais aisome.

Nashukuru juzi wakati anatoa hotuba ya Baraza la Iddi Mhe. Rais alisema kwamba alipokuwa akizungumzia wale wanaohatarisha wanaojaribu kufanya matendo ya kuhatarisha amani, alisema naomba nimnukuu kidogo.

“Kwamba ukimya wa serikali kwa kipindi kirefu sio kushindwa”. Alisema hayo katika Baraza la Iddi Rais wetu kwamba ukimya wa serikali katika kipindi kirefu katika kuwashughulikia hawa watu wanaohatarisha amani sio serikali kushindwa, serikali ina uwezo na itawadhibiti na baada ya muda kweli serikali ilifanya kazi.

Sasa namuomba kwa Mhe.Rais na yeye kwa sababu taarifa hii ipo na naamini vyombo vitapeleka kwake, basi ukimya wa serikali katika kushughulikia wizi na wanaomumunya mali ya nchi hii basi isiwe ishindwe, sasa na yeye ashughulike kama alivyowashughulikia hao waliokuwa wakihatarisha amani na utulivu wa nchi na hawa wizi awashughulikie. Kinyume na hivyo Mhe. Spika, ni tatizo.

Hawa watumishi wa haya mashirika ni watu waliofaidi, haki na mapendeleo ya nchi hii lakini hawana shukurani Mhe. Spika. Ni watu walio chini ya bendera ya nchi hii lakini inaonekana kuwa hawana utii. Ni watu ambao hawa wanafaidi mapendeleo ya nchi hii lakini kwa kweli shukurani imekuwa ndogo.

Sasa Mhe. Spika, naiomba serikali ili itende haki basi hawa wezi wote na haya mapungufu yote, kwanza pesa zirudi serikalini halafu sheria ichukue mkondo wake. Hapa katika kufichufua niwapongeze wamefichua siri lakini na hawa watendaji nao ni balaa, kwenye mitandao wanapofichuliwa siri hawa watendaji mara utasikia mheshimiwa fulani amechukua rushwa, mheshimiwa amefanya hivi, kumbe ni kwa sababu ya kufichuliwa hizi siri. Sasa naomba serikali isikae kimya iishughulikie hii ripoti na iwachukulie hatua wote waliohuka.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa sababu sikio halipiti kichwa tunasema, kichwa kinakuwa ni kirefu zaidi kulikio sikio na kwa sababu mimi kabla ya kuchangia alisimama kichwa wa Chama cha Mapinduzi, kwa hivyo mimi ninadhani kwake yeye ni sikio, nisije nikazidi sana. Niunge mkono hoja na kwa vyovyote vile hii ripoti ifanyiwe kazi na serikali na ninaiunga mkono.

Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Mansour Yussuf Himid: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa mchango wangu mdogo sana kwenye hoja hii ya Kamati ya Baraza letu tukufu inayohusiana na Shirika letu la Umeme la Zanzibar.

Mhe. Spika, demokrasi ina gharama na demokrasi ina machungu yake na nchi yetu inabadilika na imebadilika. Mimi nimeingia Barazani mwaka 2000, huu ni mwaka 2013 lakini mtiririko wa uwazi kuwa na Kamati Teule umekuwa mkubwa kati ya kipindi hiki cha Baraza hili la Nane.

Hii ni ishara au ni dalili ua kupanuka kwa demokrasi katika nchi yetu. Ni jambo la faraja na ni jambo la furaha na hasa faraja kwa wananchi kwa sababu muhimili huu unafanya wajibu wake ipasavyo ya kusimamia na kulinda maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Ni jambo ambalo tunapaswa kulikuza, kuliunga mkono na kuhakikisha kwamba Baraza hili linaendelea kufanya wajibu wake kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi yetu.

Mhe. Spika, nilikuwa ni Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kuanzia mwaka 2005 hadi 2010. Sijasimama hapa kutetea jambo hata moja. Nimesimama hapa kukumbusha Wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu yale tuliyokuwa tunayazungumza, tuliyoazimia, tuliyoyapanga na kuyatekeleza tangu Baraza lako la Saba.

Nina maneno matatu ambayo nataka niyazungumzie na yamo kwenye ukurasa wa 145 ya ripoti hii ya PAC. Nikianzia na kipengele cha mwanzo ambacho kimemshutumu Ndugu Mohamed Hashim Ismail ambaye ameshutumiwa kwa kusababisha hasara, sio kwa wizi ni kwa sababisha hasara ya shilingi thalathini na moja milioni.

Na pili ni kifungu cha 6 ambacho *conclusion* yake Mhe. Spika, na kwa heshima kabisa kwa kamati yetu hii sikubaliani nayo nikiwa ni mjumbe mwenzio wa Baraza hili. Kipengele cha 6 kinasema “kwa kuwa uendeshaji wa majenereta 32 umekuwa ni mzigo mkubwa kwa shirika ama ichangie ruzuku katika uendeshaji wake au kutafutwa utaalamu utakaowezesha majenereta hayo kutumia diesel ya kawaida yenye gharama nafuu au yauzwe”, hapo ndio kidogo nimeshtuka na kutishika na badala yake yatafutwe mengine kwa mujibu wa sheria yatakayoweza kutumika kama inavyokusudiwa.

Kipengee cha 7, “kwa kuwa kamati imepata wasi wasi kwamba kuna hujuma imefanyika iliyopelekea kukosekana kwa umeme Unguja ndani ya miezi mitatu; 2009/2010 serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kuwasilisha ripoti hii iunde tume iliyokuwa huru ya kuchunguza chanzo cha sababu iliyopelekea kukosekana kwa umeme huo na ripoti yake iwasilishwe na kujadiliwa katika Baraza hili.

Mhe. Spika, jengine ni zaidi kwa watu mbali mbali walioshutumiwa na wengine kutajwa kwsa majina. Sina tatizo na hilo isipokuwa nitakuwa na indhari tu kwa sababu pamoja na kupanuka kwa demokrasi na umuhimu wa chombo hiki kuweza kufanya shughuli zake kwa mujibu wa Katiba na Sheria na kufanya wajibu wake ina faida kubwa.

Kwa maana panapokuwa na ubadhirifu au utendaji mbovu kwenye shirika lolote la umma sote tunaathirika. Kwa sababu ya gharama kubwa za uendeshaji wake hatimaye tunaathirika moja kwa moja sisi wananchi wa nchi hii, lakini Baraza hili pia linapasa kuzingatia utu wa watu, heshima ya watu na umakini katika mijadala yetu na hatimaye kuwasilisha yale ambayo tunataka kuwasilisha.

Mhe. Spika, nianze na yale niliyosema ya kuwakumbusha wajumbe wenzangu. Mhe. Spika, mripuko wa mwanzo wa umeme ulitokea tarehe 25 mwezi wa tano 2008, ukafuatiwa na wa pili tarehe 10 mwezi wa kumi na mbili 2009. Nini walibainika kipndi kile.

Nawakumbusha mimi ndiye niliyekuwa dhamana ya wizara yake kwa wakati huu. Waya wa umeme tuliokuwa na hivi sasa unaotika Ras Kilomoni kuja Unguja ni waya ambao unaotumia teknolojia ya miaka arobaini au nineteen fifteen, ijapokuwa hapo umeekwa miaka ya thamanini au sabini mwishoni.

Waya ambao unatumia mafuta kujipoza, una shaba ndani na unahitaji uwe na *pressure* na *vacuum* kwa masaa 24. Kama tunavyoelewa waya ni mkongwe umefikia mwisho wa maisha yake na bahati mbaya sana, hata vipuri havipatikani tena, kwa maana hata kipuri ukikihitaji inabidi kichongwe na hao wachongaji ni wachache mno ndani ya dunia hii.

Kwani waya wa aina hii kwa teknolojia ile zinatumika kwa nchi chache mno. Moja ikiwa ni Norway, South Africa katika mji wa Cape Town, Amerika nafikiri ya Kusini baadhi ya mji mmoja au miwili, Kaskazini ya Amerika si sana na Uingereza bado baadhi ya maeneo bado wanatumia waya wa aina hii.

Baada ya mripuko wa mwanzo na kuweza kutengeneza, ilipotokea mripuko mkubwa wa pili, serikali ilifanya maamuzi makhususi. Jambo la kwanza tulilolifanya ni kushauriana na Serikali ya Norway kwa sababu kampuni iliyoweka waya ule ni ya Norway, wakaleta mshauri wao, tukashirikiana naye mshauri huyo na Kampuni ya Noriplan kwa gharama za ubalozi wa Norway pamoja na mshauri tuliyekuwa sisi Shirika la Umeme Bwana Martin Bolls kutoka South Afrika ambaye tulimuajiri baada ya ule mripuko wa mwanzo kuanza utaratibu wa kuvihaulisha vituo hivi, kwa maana Ras Kilomoni na Fumba, tukielewa kwamba huu waya wa pili ndio kwanza tulikuwa katika hatua za mazungumzo na utachukua muda kuwepo.

Tulishauriwa kwamba ni lazima vile vituo viwili vifanywe vihaulishwe ili kuwa na salama na usalam wa hali ya juu. Washauri wakatueleza na serikali ikakubali kwamba lazima tutulizane na tufanye maamuzi ijapokuwa yatakuwa na machungu, lakini tufanye maamuzi sahihi ya kufanya ukarabati ambao utatupa uhakika wa kuwepo huo umeme kwa muda mrefu ili tusipate taathira nyengine kama hiyo, angalau basi mpaka huu waya wa pili ukishakuwekwa. Bahati mbaya sana katika mwezi ule kati ya hiyo miezi mitatu tulipoteza zaidi ya siku 20, kwa maana kulikuwa na mapumziko yale Christmas na New Year kwa kipindi kile. Tulihangaika dunia nzima tukishirikiana na mshauri wetu na *Norplan* iliyoletwa na Serikali ya Norway, kutafuta kampuni ambayo itaweza kufanya matengenezo yale.

Mhe. Spika, kwa kiasi kikubwa wengi walikataa kwa sababu taaluma hawana. Tuliuliza Europe, India, South Africa, America kote huko walikataa. Tulipata kampuni mbili, moja kutoka Norway lakini tukaambiwa hata hao mafundi ambao wangeweza kufanya hiyo kazi, kwanza wako kwenye mapumziko ya *Christmas* na pia wameshakuwa watu wazima mno hawaiwezi ile kazi, hatimaye tukabahatika tukapata Kampuni ya *Emirates Cables* kutoka Uingereza. Nini kilifanyika Mhe. Spika, walikuja wakafanya ukaguzi kwa kushirikiana na wataalamu, kwa taaluma tuliyokuwanayo pamoja na mshauri wetu na Norplan na tukakubaliana njia na utaratibu wa matengenezo ya pahali pale. Kila kifaa kilichohitajika ilibidi kichungwe kwa sababu hakuna vifaa hivyo.

Kwa mfano, *connector* zile mbili ambayo kila moja ikiwa na uzito wa tani moja za *Stanley steal* zenye upana wa *inch* moja, zinazofanyiwa *welding* mahususi na binadamu lakini na mashine, zilipatikana Sweden na hao peke yao ndio waliokubali kuzitengeneza *connector* zile. Kutokana na kipindi kile kigumu cha *Christmas* na mwaka mpya, tulikubaliana ndani ya serikali kwamba usafiri wa vifaa hivi vikipatikana ili tusichelewe na huku machungu ya wananchi yakiongezeka na uchumi wetu kuathirika kwamba usafiri wake ufanywe kupitia DHL, zile *connector* mbili peke yake ilichukua zaidi ya wiki tatu kutoka huko zinakotoka kupitia Uingereza, Nairobi na kufika hapa. Nairobi ilibidi tutafute ndege mahususi, kwa maana ndege zilizokuwepo ndogo ndogo zinazotoka kule kuja hapa, milango yake ni midogo. *Connector* zile mbili zenye urefu wa karibu futi 12 na mapana ya karibu futi 4 hadi 5 na uzito wa tani moja kila moja zisingeweza kuingia.

Halikadhalika na vipuri vyote vile tumefanya kazi kwa kuhakikisha kwamba tunapata vitu ambavyo vinastahiki kwa kushirikiana na Ubalozi wa Norway, Mshauri wetu pamoja na serikali yenyewe kutambua. Kila kipuri kilichokuja kilihakikishwa kwamba tunaweka *electronic record,* kwamba kila kipuri kinapigwa picha kinakotoka, kinapokuja, kinathibitishwa na kinatumika. Yalisemwa mengi, lakini *Alhamdullilah* tumeweza kufanikisha ile kazi na umeme tunao hadi hii leo, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo.

Hujuma, hilo nalo tulilitafakari kwa sana kipindi kile ndani ya serikali. Kwa sababu miripuko miwili ilitokea karibu mno. Lakini baada ya wataalamu wale tuliosaidiwa na Serikali ya Norway, *conclusion* ikawa ni kwamba kuna mitiririko ya matokeo yaliyosababisha yale, hakuna hujuma wala mkono wa mtu kusababisha mripuko ule. Kwa sababu nayo hayo watu walitafakari, tukajiuliza na yakafuatiliwa.

Mhe. Spika, nirejee tena kukumbusha kwamba hata zile mashine za kusukumia mafuta kwenye mkonge ule na ya kuhakikisha kwamba hakuna upepo mule, ni mashine ambazo lazima ziundwe kwenye kampuni mahususi ziletwe kwa ajili ya matumizi yetu. Hata hayo mafuta ambayo yanatumika kwenye waya ule, yana *viscosity* maalum na yanahitaji kuagiziwa na kwa vile palipokuwa na mripuko pale, tulihitaji mafuta ya ziada yakaletwa mengi sana, sikumbuki tani ngapi, lakini nayo yaliagiziwa mahususi kufika hapa na hayo pia yalitafutwa kwa tabu kubwa mno.

Pili, washauri walitushauri pale katika vituo vyetu vya Rasikiromoni na Fumba kuwe na *system* mbili, kwamba ndani ya *connector* ile mafuta yapokelewe mpaka nchani na kuanzia pale tuwe na *system* wanayoiita *dry system*, kwa maana huku ambapo umeme unapokelewa kuja juu Unguja, pasiwe na maingiliano baina ya mafuta na hewa na yote tumeweza kuyakamilisha yale.

Mhe. Spika, nije kwenye majenereta. Nataka niwakumbushe Wajumbe wa Baraza hili, kwamba hata kabla ya mripuko ule gumzo kubwa kwenye Baraza la Saba, ilikuwa kuiagiza serikali kuchukua juhudi mahususi za kuhakikisha nchi yetu ina uwezo wake wa kuzalisha umeme, ikiwa kwa jua, upepo, *diesel* au gesi. Naamini hatua hizo bado zinaendelea kutafakariwa na kuchukuliwa hatua na serikali.
Ni nini madhumuni ya serikali kwa kipindi kile. Majenereta haya ni *emergence standby generators.* Wala haikuwa dhamira ya serikali kuleta vinu vya kuzalishia umeme ni vitu viwili tofauti hivyo. Makubaliano ndani ya serikali kipindi kile ilikuwa kwamba haya majenereta yatumike kwa namna mbili. Moja ni mfumo wa upambanishaji *pick serving mode*

Mfumo wa pili ni mfumo wa dharura, kwa maana *total black out*. Ikitokezea nchi yetu imekosa umeme kabisa basi hapo ndio yatumike. Tangu huko serikali ilikuwa inajua kwamba uwezo wa kuendesha vinu vile ulikuwa mdogo, kutokana na mazingira ya shirika na serikali yenyewe. Lakini maamuzi yakawa kwa vile tumepata wahisani ambao wako tayari kwa mazingira tuliyokuwa nayo, kutusaidia vinu Mhe. Spika, ambavyo vinabeba nusu ya mahitaji yetu ya kisiwa cha Unguja. Kwa nini tukatae wakati vinu hivyo hatutumii pesa zetu, pesa ni za washiriki wa maendeleo, wameona hali yetu, serikali imejenga hoja na hoja zote hizo pamoja na hoja za uwezo wetu wa kuendesha vinu hivyo, kwa sababu yote hayo yalihojiwa na washiriki wa maendeleo na wakaambiwa kwamba uwezo wetu ni mdogo, lakini umuhimu wa kuwepo *emergence standby generators* likitokezea la kutokezea basi tusiwe giza moja kwa moja, ndio dhamira ya kuwepo vinu vile. Havina dhamira ya kuendesha au kukidhi pengo linapotokezea mgao, sio dhamira yake. Baraza hili linaelewa, yamezungumzwa humu na waziri kivuli alikuwa ndugu yangu Mhe. Hamad Masoud kwa kipindi kile, sote tunayakumbuka na *hansard* zipo.

Kwa hivyo, hili lililoelezwa humu na kamati kwamba serikali imekosea kwa kuweka majenereta yale. Mimi naamini sio sahihi na wananchi wa nchi hii hawatotufahamu tukisema leo tuyauze yale na kwamba kuna watu wametia pesa mifukoni mwao, sio kweli. Kwa sababu tangu tunaanza kuzungumza na washiriki wa maendeleo, jambo ambalo tulisisitiza Mhe. Spika, ni kwamba wao ndio wasimamie kila hatua ya manunuzi, uchaguzi na uwekaji wa majenereta yale. Kwa hivyo, hakuna mtu ndani ya serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuanzia Serikali Kuu, wizara na hata shirika walioshiriki kufanya maamuzi yepi yanafaa, yepi hayafai na ulipaji wa jenereta zile ulifanywa na Norplan na walilipwa na Serikali ya Norway na wakisimamiwa na Serikali ya Norway, Sweden na Uingereza na mimi nikiwa Waziri nilisisitiza hayo, kwa kuhofia kwamba

kipindi kile ni kigumu cha dharura ni lazima tuwe na usimamizi mzuri. Kwa hivyo, hii dhana ya kwamba watu wametia pesa mifukoni mwao kwa zoezi lile sio sahihi na mimi Mhe. Spika, sikubaliani nalo.

Mhe. Spika, ndio maana hata tukawa na uwezo wa kupeleka umeme katika kisiwa cha Tumbatu. Kama wale wanaokumbuka mradi wa usambazaji wa umeme wa awamu ya nne, kisiwa cha Tumbatu kilikuwa hakimo. Lakini kutokana na usimamizi mzuri wa fedha, tukabakiwa na karibu dola milioni 3 tukafanya nyongeza ya vijiji 21 na ndugu zetu wa Tumbatu tukaweza kuwapelekea *submarine cable*, ambayo imegharimu zaidi ya dola milioni moja.

Kwa hivyo, ninawasihi sana Wajumbe wa Baraza hili, sidhani ni sahihi kwa sasa sisi kuchukua hatua ya kuuza jenereta zile, mimi sioni mantiki yake. Vyuma vile viko pale haviozi, haviliwi, wala huwezi kuvipaka siagi ukatia kwenye mkate ukala. Tunayo rasilimali ambayo sisi hatujatoa hata shilingi yetu, tuna *asset* tayari pale, inaongeza *asset base* ya shirika lenyewe kuongeza thamani ya shirika letu wenyewe. Kama kuna haja kwa vile sasa tuna kituo, hatuna dharura tuna kituo basi ninaweza kukubaliana na ushauri wa Wajumbe wa Baraza hili, kwamba pengine sasa tufikirie namna ya kuwa na majenereta, kwa sababu pia maamuzi tuliyofanya, sisi uzoefu wetu ndani ya nchi hii ni *slow engines* Mhe. Spika, zinazozunguka mara 800 kwa dakika moja kama zile zilizokuwa za Pemba, ndio uzoefu wa wataalamu wetu.

Lakini kama mtakumbuka kipindi kile mafuta yalipanda bei mno, majenereta kupatikana ndani ya dunia hii ilikuwa ngumu, hata Bara walikuwa na matatizo makubwa sana. Majenereta ambayo yalikuwa ndani ya soko yalikuwa *fast on use*, kama hizi zinazozunguka kwa zaidi ya mzunguko 1200 kwa dakika moja. Kwa hivyo, nawasihi sana Wajumbe wa Baraza hili, serikali ilizingatia kila jambo, tulifanya maamuzi ya kina, tulifanya maamuzi kwa kufikiri na kujadiliana sisi na washirika wetu wa maendeleo na maamuzi yale mimi mpaka hii leo naamini ni sahihi.

Mhe. Spika, nikimalizia, ile indhari niliyotaka kuitoa. Mhe. Spika, Baraza hili ni Baraza la wananchi na ni Baraza la watu, Baraza lina kazi ngumu sana. Mimi nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati ya PAC, kwamba kazi waliyoifanya ni ngumu na kwa mazingira ya nchi yetu unapofika sasa kuwataja watu sio kazi nyepesi kwa mazingira ya nchi yetu, inataka ujasiri mkubwa sana na inataka moyo na inataka imani na uzalendo mkubwa sana. Nikiwa sehemu ya Baraza hili hilo nalifahamu na ninalipongeza sana.

Mhe. Spika, lakini wakati tunakuza demokrasia ndani ya nchi yetu, *cheque and balance*, lazima tuwe makini na kuelewa kwamba hata yule ambaye unamshutumu na wewe kuamini kwamba kafanya kosa fulani, ana haki ya utetezi. Baraza hili haliwezi kushtumu na kuhukumu, utaratibu huo ndani ya katiba haumo. Baraza hili linaweza likashutumu, likabainisha, likaelekeza na kuwaacha watu wakapata fursa. Serikali ikafanya wajibu wake na mimi naamini serikali hii inayoongozwa na Dk. Shein na shughuli za serikali zikisimamiwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Mimi naamini ni watu makini na watafanya wajibu wao, kwa sababu wameshadhihirisha wazi kwamba hawataki uzembe wala lolote lile ambalo litakwenda kinyume na maadili yetu. Lakini niwaombe sana Wajumbe wa Baraza hili, tusiwe wepesi wa kuanza kuwahukumu watu hapa, tutoe nafasi na fursa ili na watu nao wapate kujitetea kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi hii.

Lakini pamoja na yote hayo Mhe. Spika, mimi nikimalizia nasema, nikiwa Mzanzibari na nikiwa Mjumbe wa Baraza hili ninafarijika sana na mabadiliko haya na namna demokrasi inavyokua ndani ya nchi yetu, namna Baraza lako hili linavyofanya na kuelekea kufanya wajibu wake ipasavyo ya kuisimamia serikali na haki za wananchi wa nchi hii. Lakini ninawaomba sana kwa mara nyengine, tuwe makini sana wakati tunawataja watu, pia tukumbuke na tupime yale ambayo watu hao hao kazi za kizalendo na wao wanazifanya katika taasisi zao ili kusogeza mbele maendeleo ya nchi yetu. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu Mwenyezi Mungu Azza Wajalla, kwa Rehma zake na kwa kuendelea kutupa neema zake za uhai na uzima, tukiamka wazima na tukiendelea na shughuli za kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, pili nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu katika ripoti hii na nitaomba univumilie kidogo, ingawa nitajitahidi sana kufupisha yale ambayo nayazungumza ili na wenzangu wapate muda.

Tatu Mhe. Spika, naomba nishukuru na kuipongeza Kamati ya *PAC* ikiwa imefanya kazi maalum katika suala zima hili la uchunguzi wa utendaji wa Shirika la Umeme Zanzibar, yaani *ZECO*. Ukiisoma ripoti yao Mhe. Spika, wamefanya kazi ngumu na nzito na ni kazi ya kina kabisa.

Mhe. Spika, kwa maoni yangu na nitayasema yapo mapungufu machache, lakini upungufu ndio maumbile ya binadamu, aliyekuwa mkamilifu ni Mwenyezi Mungu tu Subhanahu Wataallah. Hayo nitayasema Mhe. Spika, kwa sababu najulikana katika Baraza hili, hata ilipokuja ripoti ya mwanzo kabisa ya uchunguzi katika Baraza hili yako mambo niliyaunga mkono na yako mambo nilitahadharisha. Kwa sababu kama nilivyosema sio mmoja katika wanaoamini kwamba ili ulikubali jambo ni lazima ulikubali lote, au ukilipinga ulipinge lote. Sote ni binadamu kila mmoja na uwezo wake.

Mhe. Spika, na mimi naomba niungane na Mhe. Mansoor Yussuf Himid kusema kwamba ninafarijika sana na jinsi chombo hiki ambacho alikianzisha Rais wa Pili wa Zanzibar, Mzee wetu Mhe. Aboud Jumbe, alikiita ngome ya wananchi kwamba sasa katika Baraza hili hasa ndio kinafanya kazi ya kuwa ngome sahihi.

Mhe. Spika, jambo la kutia moyo wala wala sio jambo la kusikitika kwamba kwa nini hatukuwa hivyo miaka 10 au 20 iliyopita, mabadiliko ni hatua na ni utaratibu. Tulipo leo sio tulipokuwa miaka 5 iliyopita, na tulipokuwa miaka 5 iliyopita sio kama tulivyokuwa miaka 10 iliyopita na hivyo hivyo Mhe. Spika.

Kwa hivyo, na mimi nafarijika. Juzi nilipokuwa nimetoa hoja hapa kuhusu mtiririko wa shughuli za Baraza, nilikuwa nina ombi kwako Mhe. Spika, kwamba tufanye kazi ya kurejesha imani ya wananchi katika chombo hiki, kwa sababu hapa katikati kidogo ilitetereka.

Niwaambie Wawakilishi wenzangu Mhe. Spika, katika hili kwamba tutahadhari sana na hili. Mtu asije akadhani ni Baraza la Wawakilishi hili kwamba utatumikia maslahi fulani, yawe ya chama chako, yawe ya mtu fulani pengine unayemtumikia huko nje, ukaja kujaribu kuzorotesha chombo

hiki ukategemea utakuwa salama kwa wananchi ukifika wakati wa uchaguzi. Wananchi wa leo wa Zanzibar, sio wananchi hata wa mwaka 2010 walipotuchagua Mhe. Spika. Miaka miwili hii imebadilisha sana mtazamo wa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kama ingekuwa ni suala la kudhamini ningesema tusubiri mwaka 2015 tutakuja kuona wananchi wetu wanaerevuka Mhe. Spika, na dunia nzima inabadilika. Leo ikiwa nchi za Arabuni kuna kitu kinaitwa *Arab Springs*. Waarabu wote walikuwa wanaonekana kazi yao ni kukaa Jangwani na kula tende. Leo watu wameamka na kuzitaka mamlaka zao ziwajibike ni kwa sababu dunia nzima imebadilika.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, na mimi naunga mkono kabisa yale maneno aliyozungumza Mhe. Mansoor Yussuf Himid kwamba hili ni jambo la kutiwa faraja. Katika hili Mhe. Spika, wewe hatuwezi tukakutoa kwamba ni kielelezo na mfumo wa mabadiliko haya yanayotokea katika Baraza hili, kwa sababu kama sio uhuru ambao unautoa kwa Wajumbe wako Mhe. Spika, tusingefikia hapa.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea na mchango wangu, nataka nimpongeze sana kaka yangu Mhe. Mansoor Yussuf Himid kwa mchango wake aliokuwa kautoa punde. Kwa kawaida ya nchi hii, tunavyopenda kuchukua mambo binafsi, sio rahisi kwa mtu ambaye alikuwa na dhamana ya wizara ambayo mambo mengi yaliyokuwa yanazungumzwa alikuwa nayo, akachangia kwa namna alivyochangia hapa. Ama angekuja na kutaka kukataa yote, lakini kuna sehemu kubwa kapongeza kazi ya kamati na kuonesha mafanikio yake na pale ambapo alikuwa anahisi ana taarifa ambazo zinaweza kusaidia kukamilisha taarifa ambazo kamati haikuzifanya, amelisaidia Baraza hili. Hilo ni jambo la kutiliwa mkazo sana, kwa sababu ili ukweli ukamilike ni lazima kila mwenye taarifa aweze kuzitoa hizo taarifa ili tuweze kusaidia. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Mansoor kwa sababu ameonesha hasa ukomavu wa uongozi ambao wengi katika Baraza hili tunapaswa tuige kutoka kwa mtu kama Mhe. Mansoor.

Mhe. Spika, sasa nije katika ripoti yenyewe. Mhe. Spika, sikusudii kwenda kifungu kwa kifungu katika yale ambayo yamegusiwa, kwa sababu tumeshasomewa ripoti hapa na wananchi wameisikia. Lakini nataka kusema kwamba kuna mambo ya msingi ambayo yameibuka katika ripoti hii ambayo serikali ni lazima iyatazame. Haya Mhe. Spika, yameonekana katika *ZECO* kwa sababu imekwenda kuchunguzwa. Naamini mimi haya kila shirika, idara au wizara za serikali yatabainika haya. Mhe. Spika, tukitaka tusitake utendaji katika serikali yetu umevurugika sana, ile dhana ya kuona kwamba nafasi ya utumishi wa umma ni dhamana ambayo itapasa kuwatumikia wenzako imeondoka sana katika nchi yetu Mhe. Spika.

Kwa hivyo, mambo kama yameonekana humu upendeleo katika utoaji wa huduma, upotevu wa mapato, kwamba mtu analipwa lakini hapewi risiti, kuhujumiana katika idara, yameelezwa Mhe. Spika, huku kwamba, kwa sababu amefanya jambo ambalo mimi silipendi basi nitahujumu idara yako, na ni shirika moja. Haya Mhe. Spika, sio katika idara moja ndani ya shirika tu, hata ndani ya idara kwa idara na wizara kwa wizara wanahujumiana, yako mambo haya, kwa sababu tu mtu hakupata chake cha kutia mfukoni, yapo hayo Mhe. Spika.

Mhe. Spika, yamebainika na tulikuwa tukiyapigia kelele kila kikao cha bajeti hapa, tunapopiga kelele kwamba bajeti za safari za viongozi hizi zinawaumiza wananchi, imeonekana tunaunda

safari hazina mwanzo wala mwisho kumbe watu wanatafuta posho za safari basi Mhe. Spika, yameonekana humu.

Lakini kuna masuala ya ubadhirifu vile vile Mhe. Spika, yameonekana humu, kwamba watu wakitaka kufanya jambo wanakwenda kukodi gari ili kwenda kutoa huduma fulani, ambayo pengine serikali ingeweza ikanunua lake kwa gharama ile na ikawa ile ni mali yake, badala ya kutumia pesa chungu nzima kwenda kukodi gari wakati pesa ile ingeweza shirika kulipatia gari lake, ni aina ya ubadhirifu ambao unaendelea katika serikali yetu.

Pia Mhe. Spika, imeelezwa humu bado tuna tatizo sugu sana kwenye upendeleo katika kutoa ajira. Katika hali kama hii Mhe. Spika, tusitegemee hata siku moja kuwa tutafikia kiwango cha ufanisi katika utendaji wa serikali yetu. Ukishakuwa unaajiri mtu sio kwa sababu ya sifa na uwezo wake, lakini kwa sababu anamjua fulani tutapata matatizo. Hii tujifunze Mhe. Spika, humu humu Barazani iliwahi kutokezea miongoni mwetu, katika Baraza hili hili Mhe. Spika, tukakauka vifua kwa kuwatetea baadhi ya watu, serikali ikajakujibu hapa ikaonesha kwamba yule mtu alikuwa ana sifa. Kwa hivyo, hili sio kwa serikali tu hata sisi wenyewe tukiwatetea watu hapa, tusibebe hoja tu kwa sababu unataka kumpendelea mtu fulani, hii itatuletea matatizo makubwa sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, wanasema ukianza kubadilisha utaratibu wa uajiri, badala ya kuwa unamwajiri mtu kwa sababu ya *know how* yake, ikawa ni *know who* basi una matatizo. Yaani badala ya kwamba unajua nini, ikawa unamjua nani basi ni matatizo katika nchi. Hayo Mhe. Spika, yamebainika.

Pia Mhe. Spika, yamebainishwa humu na Kamati masuala ya upendeleo katika hata utoaji wa nafasi za masomo na haya yamo ndani ya serikali Mhe. Spika. Mhe. Spika, mara nyingi tulikuwa tunazungumza tulipokuwa tukijadili rushwa hapa, kuna baadhi ya Wajumbe walizungumzia habari ya kuwepo rushwa, iliitwa rushwa ya ngono, haya yapo Mhe. Spika. Kuna watu wanapewa nafasi za masomo kwa sababu tu wakubwa wana maslahi fulani na mfanyakazi yule, yapo Mhe. Spika. Kwa hivyo, nafurahi kwamba kwa muhtasari nimeyazungumza yamejitokeza katika ripoti hii, sikutaka kwenda ukurasa kwa ukurasa kwa sababu tutakuwa tunayarejea yale kwa yale ambayo tayari Kamati imeyasoma.

Lakini yale mazito Mhe. Spika, ambayo naomba niyaseme. Kwanza la jumla la Shirika la *ZECO*. Mhe. Spika, ziko taarifa kwamba hii *ZECO* imegeuka ni mradi kwa wakubwa na wakubwa haina maana serikalini tu Mhe. Spika. Ziko taarifa na hili sio kwa *ZECO* tu, hata kwa mashirika mengine, lakini tunaizungumza *ZECO* hapa kwamba hata baadhi ya Wawakilishi, kuna mafungu pale ya kutusaidia sisi miradi, inatumika hii ama kunyamazisha au kumtuma Mwakilishi aseme, yapo hayo.

Kwa hivyo, nasema hili tusije tukawa ngariba wa Kilwa, kwamba hodari wa kuwakata wenzetu, lakini sisi wenyewe hatutaki kujikata. Mhe. Spika, kuna maneno haya yanazungumzwa na kuna watu wengi wanatumwa. Lakini inasemekana hata vyombo vya ulinzi Mhe. Spika, ambavyo ndio tungevitegemea ndio vingekuwa vinafanya kazi ya kusimamia hizo sheria za nchi hii, kwamba mara nyengine vinarudi nyuma kwa sababu na wao pia wana maslahi yao vile vile pale.

Sasa tukifika pahala Mhe. Spika, ikawa tunatumia mashirika ya umma kwa maslahi kama haya, basi tusitegemee kupata maendeleo katika hii nchi Mhe. Spika. Kwa hivyo, nasema hili tunapaswa tuliangalie.

Jengine Mhe. Spika, ninalotaka kulizungumza ni la wafanyakazi na sio wa *ZECO* tu, lakini tunaizungumzia *ZECO* kwa sababu ripoti ndio iko juu ya meza Mhe. Spika, watu kutumia nafasi zao hizi kwa ajili ya kujinufaisha wao. Tumeona Mhe. Spika, humu. Mfanyakazi Zakia Juma Azzan anaagiza aingiziwe katika *account* yake binafsi, shilingi 37,720,000, kwa mradi ambao gharama yake hasa alizoandikiwa mteja, nadhani ni ndugu Aman Ibrahim Makungu, ni shilingi 2,052,696 pana ziada ya 35 milioni, hizi zimekwenda mfukoni kwa huyu mama ndio maana yake. Ni kwa nini utoe *account* yako na haya Mhe. Spika, yameoza. Tunaambiwa sio hili tu, kuna miradi mingine mpaka ya nje huko inayofadhiliwa na inafika pahala watu wanaingiziwa fedha katika *account* zao binafsi.

Mhe. Spika, tujifunze kwa sababu rushwa ina sehemu mbili, ina mtoaji na mpokeaji. Kwa sababu na wewe vile vile unapofika pahala ukaambiwa uingize pesa katika *account* binafsi ya mtu katoa, maana yake na wewe vile vile una walakin. Najua ulikuwa unataka huduma, kama ilivyosema ripoti kwamba unaweza ukafanya lolote, lakini kuna vyombo na suala kama hili kwa sababu sio pesa kidogo, ungeweza hata kufanya mkutano na waandishi wa habari kwa sababu ni mwekezaji mkubwa ukasema, kwa nini ulipe pesa hizi katika *account* ya mtu binafsi. Lakini nasema hiyo haiondoshi kwamba aliyefanya mambo hayo amefanya kosa kubwa sana katika nchi. Mhe. Spika, nasema hili sio kwa huyu tu, haya yapo kila pahala Mhe. Spika.

Mhe. Spika, jengine katika hili limezungumzwa hapa na hili linasikitisha sana, kwamba na wananchi walikuwa wakipiga kelele siku nyingi, tulikuwa tukiwakatalia, lakini Kamati imekwenda kuthibitisha, kwamba wakubwa wa shirika hili, lakini pengine kuna wakubwa wengine serikalini, kumekuwa na tabia kwamba wao wako *above the law*, hawa wanatumia huduma ya umeme bure wanalipiwa na shirika hawalipi.

Hivi Mhe. Spika, tukienda namna hii si hatari, maana yake kesho itakuja kuwa kwa sababu wewe ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali basi kama kuna ada ya Chuo Kikuu, basi wewe usilipe kwa sababu Chuo Kikuu kiko chini ya wizara yako, itafika pahala kama wewe ni Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, basi usilipe maji kwa sababu wewe uko katika wizara ile.Vile vile tutafika pahala kama wewe ni Waziri wa Afya unatakiwa utoe mchango wa kwenda kufanyiwa matibabu wananchi walipe na wewe usilipe kwa sababu ni wizara yako na tukifika hapo ni hatari kubwa, kwa kweli tumefika hapo Mhe. Spika tumethibitishiwa na Kamati hii.
Kwa hivyo, hii ni hatari, kwa sababu hawa wakitumia umeme Mhe. Spika wanaongeza gharama za uendeshaji kama yeye halipi basi nitalipa mimi na wewe Mhe. Spika ndio tutakaolipa gharama za umeme. Kwa maana hiyo, huku ni kuwakamua wananchi wetu wanyonge na wala sijambo sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Jambo jengine ambalo limejitokeza humu ni suala zima la namna ya kupeana kazi na limezungumzwa hapa, kwamba Sheria ya *ZECO* imeipa *monopoly*, kwamba *ZECO* ndio msambazaji na mtoaji huduma pekee katika suala hili na huduma zinazofuatana na huduma hizi.

Lakini tumeona humu kuna Kampuni ya *GECCO*, ambayo nasikitika mimi kwamba kwenye wakurugenzi wake kuna wafanyakazi wawili ambao ni watumishi wa shirika na kuna mwengine alikuwa mtumishi wa zamani ambaye ana nafasi kubwa ya kisiasa katika nchi hii wanatumika Mhe. Spika.

Sasa badala yake wao wanapewa kazi, kwa hiyo mimi nitaamini vipi Mhe. Spika, kwamba katika kutoa kazi hizi kwa makusudi na kufelisha *ZECO* isipewe kazi ile kwa sababu mimi ninayo maslahi yangu mule ndani, kwa sababu hawa wawili ni watumishi wa *ZECO*.

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika kwamba katika hili asitafute maneno na hata akiwa huyu mwanasiasa anatoka Chama cha *CUF* kinachoeleza kwenye ilani yake kwamba mtu akatumie nafasi yake katika dirisha. Kwa hivyo, yeyote ambaye amehusika katika suala hili nasema kama sheria zilikuwa zinavunjwa, basi hatua zichukuliwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaambiwa hapa kwamba serikali imekosesha shilingi 185 milioni mapato kwa hujuma ambayo imefanywa na *GECCO*, ambapo kama ingefanywa na shirika basi fedha hizi zingeingia katika mapato ya shirika na zingekuja kuwahudumia wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Vile vile kwenye ukurasa wa 53 zimetajwa tena shilingi 116 milioni na hizi ni huduma katika minara ambazo zingekwenda kwenye shirika, lakini zimekwenda kwenye kampuni ya mtu binafsi kwa sababu watu kuna maslahi yao. Kwa kweli masuala haya hayafurahishi hata kidogo.

Mhe. Spika, hii ni hatari na mara nyingi hapa tunatumia kauli za siasa sana kutukana na kusema wakoloni ni wabaya na wala hakuna aliyesena kwamba wakoloni ni wazuri.

Lakini Mhe. Spika, nataka kuonesha mfano mmoja wa tofauti ya uadilifu ulivyokuwa zamani na ulivyo hivi sasa. Mhe. Spika, haya tunayoyaeleza haya ni wizi wa mamilioni, maana kuna milioni 35 na wala hakuna laki hapa isipokuwa ni mamilioni tu hapa.

Mhe. Spika, nimepata habari kwa sababu mimi ni mtu mwenye kupenda sana kusoma mambo ya historia. Katika kumbukumbu za kihistoria wakati nilipokuwa Uingereza nilikuwa nikisoma katika *Public Record Office*, yaani lile Nyumba wanayoweka Nyaraka za Kumbukumbu za Zamani na bila ya shaka nilikuwa napenda kwenda kusoma zinazohusu Zanzibar.

Kwa kweli kuna kitu kimoja ambacho nataka nikipigie mfano sana, nadhani kama sikosei ilikuwa mwaka 1959 au 1960 aliyekuwa Mfalme wa Unguja wakati ule Said Khalifa Bin Harith aliwaomba Waingereza ambao waliokuwa wakiilinda, yaani *Protecting Power* kumpeleka mjukuu wake kumpatia mafunzo fulani, kwa sababu katika elimu ya kawaida haoneshi *interest* akapelekwa Said Jemshid kwenda kujifunza mambo ya Serikali za Mitaa kama Said Soud, basi aliekewa posho yake kama mtu mwengine yeyote anayepelekwa kusoma kule.

Lakini kwa sababu ya maumbile yake ukisoma hizi *records* yeye na mkewe walikuwa ni watu wa kupendana sana na ikawa kile kiwango kilichowekwa hakimtoshelezi kwa matumizi yake, kwa sababu ni kiwango cha kawaida kama anacholipwa mtu mwengine yeyote. Sasa wakaomba familia ya Kifalme wakaomba aongezewe *pound* 5 kwa wiki, kwa sababu wenzetu wanalipa kwa wiki.

Mhe. Spika, ukisoma ripoti hizo nilizozisoma Mhe. Spika maana wakati huo aliyekuwa Mfalme ni Said Khalifa aliyekuwa mrithi wake ambaye ndiye baba wa Said Jemshid, yaani Said Abdalla, imeandikwa mule alivyokuwa akipanda ngazi na kushuka Idara ya Elimu kwenda kulilia hali mwanawe aongezwe *pound* 5, sasa hawa wakoloni Mhe. Spika wabaya.

Kwa hivyo, sisi leo tumefanya mapinduzi kwa ajili ya kuwakomboa wananchi na hali ya mambo ni hii, kwamba watu wanatafuna tu fedha za walipa kodi. Mhe. Spika, nasema haya ni mambo ya msingi sana ya kujifunza, kwamba unapopewa dhamana ya uongozi fedha ziliopo pale si zako ni fedha za nchi tujifunze katika hapa Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, amezungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin na mimi nakubaliana naye, kwamba Pemba ndio imegeuzwa ndio kichaka cha wakubwa kula na hili si la mwanzo Mhe. Spika, wakati alipokuwa akisema Mhe. Mjumbe mimi nilikuwa nikiwaambia wenzangu hapa kama ameyachukua maneno yangu, kwamba kuna *account* inaingizwa shilingi milioni 2 kwa siku ya *other charges* matumizi ya kawaida na watu wanatumika.
Nina hakika Mhe. Spika wala haziliwi Pemba hizi kama Pemba zinaliwa basi ni chache sana. Lakini watu kudhani kwamba kule jicho halifiki, kwa hivyo ziondoe hapa na kuzihamisha kuzipeleka Pemba halafu mimi nitapata *change* kule, ndivyo ilivyozoeleka Mhe. Spika. Kwa hiyo, nasema haya Mhe. Spika tuyatizame sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika mambo ambayo yamenipa huzuni sana yanayohusu ukaguzi, kwa sababu kwenye fedha siku zote kuna matatizo yake na ndio maana tumeweka utaratibu wa ukaguzi, ili kujua matumizi yanavyofanyika na tunao ukaguzi wa ndani na nje.

Kwa kweli humu Mhe. Spika yameoneshwa katika ukurasa wa 55 aliyekuwa Mkaguzi wa Ndani ndugu Moh'd Khamis Juma ameadhibiwa kwa sababu ameonesha wakubwa wanavyozitafuna fedha za shirika. Mhe. Spika, hili limetopea ndani ya serikali humu, wakaguzi wa ndani kuadhibiwa baada ya kudhihirisha au kubainisha uchafu wa wakubwa, basi hupewa adabu kwa kuhamishwa sehemu za kazi na haya yameoza au yametopea ndani ya serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niliwahi kumwambia Mhe. Waziri wa Fedha hapa na bado sijaona hatua mpaka leo, kwamba nilimwambia wakati umefika na sisi tuanzishe *Chief Internal Auditor or Internal Auditor General* kama zilivyo nchi nyingi za Jumuia ya Madola, Mhe. Waziri wa Fedha akasema serikali inachukua hatua na wala sijaiona.

Kwa hivyo, ukimalizika mwaka huu wa fedha kwa sababu aliniahidi wakati wa bajeti mwaka jana, basi kama sijaiona Mhe. Spika hivi sasa ninavyozungumza tayari ninajiandaa kuandaa mswada binafsi wa *Internal Auditor General* nitauleta katika Baraza hili la Wawakilishi kama serikali haijachukua hatua, kwa sababu hapa yapo matatizo makubwa. *(Makofi)*

Lakini hilo dogo Mhe. Spika, kubwa itakapofika kwamba Mkaguzi wa Ndani anatakiwa akosee na Mkaguzi wa Nje aoneshe mapungufu yake. Lakini leo Mkaguzi wa Ndani ameonesha mapungufu basi Mkaguzi wa Nje akenda kuzidisha kuficha uchafu uliopo pale na hii ni hatari sana.

Mhe. Spika, imetwambia Kamati kwenye ukurasa wa 58 kwamba wamefika pahala wamekuta wino wa kijani, kwamba Mkaguzi wa Nje *CAG* ameshapita. Mhe. Spika, kamati zako za Baraza ni sehemu ya Baraza hili kwa hivyo si aibu wala sioni haya kusema mambo ya kamati hapa.

Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako Mhe. Spika, nilizungumza kipindi si kirefu nakumbuka tulipoanza kuja Baraza hili nilikuwa miongoni mwa Wajumbe wa kwanza kuipongeza Ofisi ya *CAG* kwa kazi ilizokuwa ikifanya, lakini baada ya kubaini kwamba kuna *loop holes* zimetumika mule nilisema ndani ya kamati na Mkaguzi alikasirika sana wa *CAG*, akasema pale kwamba kazi ilikuwa ngumu na mambo mengine, lakini kumbe leo imethibitishwa hoja yangu na Kamati ya *PAC* na imeonesha mfano hai. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maneno ya jamaa zangu wa Kipemba wanasema "*ikiwa kilemba kimeroa mkuti uhali gani*" na mkuti wanasema kile kikoi. Sasa ikiwa Ofisi ya *CAG* ndio inayotegemewa ilinde fedha zetu na badala yake ndio inayotumika kuficha wizi wa fedha zetu, tumtegemee nani Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu posho za safari tayari nimeshalizungumza na hili limenishtua na hili ndio kosa na mara nyingi nimesema humu ndani. Kwa kweli tumefika pahala Mhe. Spika, lazima tuwe na sera zinazoongoza utendaji na uongozi wa mashirika na wala hatuwezi kuliacha shirika likafanya linavyotaka tu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ilizungumzwa hapa wakati wa Ripoti ya Kamati Teule yako ya mwanzo uliyoiunda Mhe. Spika, kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege watu wanafanya wanavyotaka kule.

Vile vile hapa nimeona nadhani kwenye ukurasa wa 60 mtu amelipwa posho safari ya siku mbili shilingi 260,000/= mbali ya nauli, sasa hii maana yake kwa siku moja ni shilingi 130,000/= najiuliza hichi ndicho kiwango cha posho hata kwa watendaji wakubwa wa serikali na huyu ni mtumishi tu wa shirika na hawa wakubwa wa shirika wanapata kiasi gani. Mhe. Spika, haya ndio matatizo ya kutokuwa na sera inayoongoza mambo haya.

Kutokana na hili nadhani serikali ijifunze lazima kuwe na sera inayoongoza, yaani kuwe na *uniformity* na tujue kwamba posho za safari ndani ya shirika la serikali ni kiasi gani, basi iwe hivyo kwa wote kama usafiri kwa daraja gani kama ilivyo viongozi, ikiwa Wawakilishi wa wananchi ipo sera ya muongozo unaowaongoza, kwa nini isiwe hivyo kwenye mashirika na ikawa kila mmoja tumuachie afanye anavyotaka na fedha za wananchi zinatafunwa.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ripoti hii pia imeguswa kampuni na Mhe. Spika nakuona unaangalia saa nitamaliza Inshaallah muda si mrefu. Katika ripoti hii kuna Kampuni imeguswa *Chinese Railways Jianching Engineering (CRJE)*. Mhe. Spika, mimi naomba hasa serikali ije itueleze kwamba ina *interest* gani kwenye kampuni hii, kwa sababu gani nauliza hivi.

Kwa kweli mwaka jana niliwahi kumuuliza mwenzangu mmoja kwamba mbona kila mradi wa serikali ni *CRJE* tu na kwa sababu sijapata ushahidi wa kumtia mtu hatiani na leo silisemi na wala simtaji jina.

Lakini niliwahi kutajiwa jina la kiongozi mmoja mkubwa katika serikali hii kwamba huyu pia anacho chake humu kwenye hii miradi inayoidhinishwa, na ndio maana kuna shindikizo fulani kwamba miradi yote wanapewa hawa tu *CRJE* tu. Mhe. Spika, naomba hii tuiangalie kwa makini kabisa. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Spika, naomba nilizungumze kwa uchache suala la majenereta 32 na nimeyasikiliza kwa makini maelezo ya Mhe. Mansoor Yussuf Himidi. Katika yale maeneo ambayo nina *reservations* zangu na niliwaambia Wajumbe wa kamati na kila siku tukizungumza hapa na mradi huu ulifadhiliwa na washirika wa maendeleo na washirika ni Uingereza, Sweden na Norway.

Kwa hivyo, niliwaambia kwamba mumefanya kazi nzuri, lakini Ubalozi wa Norway na nyengine ziko Dar-es-Salaam tu hapo kwa nini musiende kuwahoji kwa ajili ya kukamilisha ripoti yetu na tukajua ukweli uko wapi na tulikuwa tukizungumza kirafiki tu, wakasema kwamba hilo hawakulifikiria.

Mhe. Spika, nasema kwamba hili linafanya ripoti hii kidogo katika kipengele hichi cha majenereta 32 kidogo iwe haikukamilika. Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu gani, katika nchi ambazo huwezi kuchezea fedha zake ni Norway tunakumbuka mwaka jana tu Bara walizuia fedha kwenye bajeti ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano baada ya kuwa kuna mradi katika masuala ya maliasili ambao walikuwa wakifadhili kusikia kuna harufu ya rushwa.

Sasa katika suala kama hili sidhani kama kungekuwa na kitu kama hichi wangenyamaza na hasa kwa sababu wizara inatuambia kila kitu waliachiwa wao. Lakini nasema ili tupate taarifa kamili basi tuwapate hawa, ili wahojiwe.

Kwa hivyo, hili ni bahati mbaya halikupatikana na nimeliona halikukamilika Mhe. Spika kwa sababu hata hizi fedha zilizotajwa humu na mimi ni mfuatiliaji sana wa mambo. Kwa mfano, wakati ule tunakumbuka fedha ambazo zilitolewa haikuwa dola milioni 1 wala majenereta yale hayakuwa shilingi milioni 1 nakumbuka zilikuwa ni shilingi milioni 11 tena nakumbuka hata kwenye magazeti ilitajwa.

Kwa maana hiyo, hizi milioni 1 inaonekana ni malipo na huduma fulani katika zile ambazo shirika ililipa na Mhe. Mansoor Yussuf Himidi ananisaidia hesabu na anasema Serikali ya Norway ilitoa dola milioni 4, *SIDA* walitoa dola milioni 4.5 na *DFID* ambao ndio Waingereza waliotoa dola milioni 3 na SMZ nayo ikatoa dola milioni 1.5.

Mhe. Spika, inawezekana hata hii iliyolipwa na *ZECO* ni katika hiyo iliyotoka SMZ, kwa sababu si rahisi kama nilivyosema ninavyowatambua washirika wa maendeleo hawa kwa fedha zao zikachezewa. Kwa hivyo, nasema hii ni muhimu tungeikamilisha, ili tukapata ukamilifu wake.

Vile vile katika suala la hatua za kuchukuliwa na mimi kijumla sina matatizo na yale maeneo yote ambayo tu mamlaka nayo kutoa mapendekezo ya kuchukuliwa hatua za kinidhamu pale panapohusika, kwa sababu ndio jukumu letu katika kuisimamia serikali. Lakini pakiingia hatua za kisheria Mhe. Spika, sisi letu lile liliomo kwevye ripoti hii ni kupendekeza kwamba hatua za kisheria zichukuliwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama alivyosema Mhe. Mansoor Yussuf Himidi misingi ya kisheria Mhe. Spika unaifahamu vizuri sana kwamba haituruhusu sisi kutuhumu na kuhukumu, yaani kwenye *Principles of Natural Justice* wanasema "hakuna mtu ambaye atakuhumiwa bila ya kusikilizwa" wa pili unasema "*no one shall be a Judge of his own cause*", yaani huwezi kutuhumu na halafu ukahukumu.

Sasa nasema utaratibu uko wazi na kwenye Katiba yetu Mhe. Spika, ibara ya 56(a) imetaja Mamlaka wa Mkurugenzi wa Mahakama na ndio utaratibu wote Mhe. Spika kama kamati yetu ya Kutunga Sheria inafanya kazi yake, baadaye yale iliyoyagundua na imeshaisaidia Ofisi ya *DPP* na vielelezo vyake vinapelekwa pale, ili Ofisi ya *DPP* aone kwamba kuna hatua za kisheria za kuchukuliwa.

Kwa hivyo, nasema yale ya kinidhamu yako serikalini na tunayo mamlaka ya kuwaambia na tunalo na kisheria, basi tufuate utaratibu, ili tuendeleze utawala wa sheria.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nimenigusa linalohusu katika kuchunguza pia walitakiwa Kamati wachunguze sababu za usumbufu na gharama kubwa ya umeme na walizungumzia suala la *ZECO* na *TANESCO* na wala sitaki kuchukua muda wako Mhe. Spika nimeshauchukua mwingi.

Nataka kusema kwamba najiuliza mimi na kila siku tunasifiwa kwamba hawa ni ndugu zetu wa damu wanatupenda sana wengine mpaka wanalia humu wakiwatetea Mhe. Spika, na sisi wengine tunaotetea mahusiano mapya tukaonekana mahaini katika nchi hii. *(Makofi)*

Lakini uhaini huu hapa Mhe. Spika ule wanaotufanyia wao, kwamba mtumiaji wa kawaida wa umeme kwa Tanganyika analipa *unit* moja shilingi 118, lakini mtumiaji wa umeme Mzanzibari analipa shilingi 210 kwa *unit* moja, sasa huu kama si unyonyaji ni kitu gani Mhe. Spika.

Kutokana na hali hiyo, ndipo pale niliposema kwamba mara nyengine wanatufanyia ni aghasi ya ukoloni halafu tunaonekana ni wabaya ni haya Mhe. Spika. Vile vile nimeona kwenye ripoti hii tena nashukuru kamati kwa kuyabainisha, kwamba kwa Bara wanaotumia huduma wanaambiwa walipe asilimia moja ya gharama ziende kwenye uendeshaji wa gharama za kulipia *EWURA*.

Mhe. Spika, *EWURA* si chombo cha Muungano na kwa kule wametoa asilimia moja ya *TANESCO* mapato yake yaende kule, lakini kwa hapa *ZECO* inatakiwa ilipe asilimia tatu. Huu si kama unyonyaji wa Tanganyika dhidi ya Zanzibar tuite nini! *(Makofi)*

Mhe. Spika, nasema kwamba haya ndiyo yanayowafanya wananchi wa Zanzibar wakafika pahala tulipofika kwamba kila mtu abaki na mamlaka yake kamili na Muungano wa Mkataba kila mmoja aishi kivyake na tukifanya mahusiano, basi tufanye mahusiano ya kibiashara kama zinavyofanya nchi nyengine zozote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nimesema sana pia Mhe. Salmin Awadh Salmin hapa kwamba serikali kwa mujibu wa kifungu cha 43(5) cha Katiba yetu, mawaziri wanawajibika katika chombo hichi kwa pamoja chini ya Makamu wa Pili wa Rais na hili walichukue kwa umakini sana.

Kwa kweli siku ilipoletwa ripoti ya kamati ya mwanzo tulisema hapa kwamba msijemkatufikisha pahala ikiwa tumekata tamaa kwamba serikali hai-*respond* juu ya mambo haya na tukalazimika kuja kupiga kura ya kutokuwa na imani ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu Katiba inaturuhusu, alilisema Mhe. Hamza Hassan Juma wakati ule hapa na watu wengine walikasirika.

Lakini tukifika pahala kwamba tunaona serikali haisimamii kwa nini hatutumii njia nyengine au tufike pahala tuiambie serikali nzima iwajibike iondoke na serikali mbovu, kwa sababu hayatekelezwi haya na Mhe. Spika hilo ni jambo la hatari.

Mhe. Spika, tunapoona leo katika nchi yetu hata Bara hapo na mimi kila ninaposoma magazeti siku hizi wananchi wanachukua sheria mikononi mwao, na hata yaliyotokea Zanzibar mwaka jana. Kwa hivyo, tusidhani kama yote yale wale watu wanaunga mkono yale ambayo waliyokuwa wakihubiriwa na waliokuwa wakihubiri hapana Mhe. Spika.

Kwa maana hiyo, mara nyengine wananchi huwa wanakata tamaa na viongozi wao kwa mambo kama haya, sasa linapokuja lolote la kuonesha hasira zao dhidi ya serikali hawa tunaowatawala wanaingia mkumboni na kuonesha hasira zao na tukifika hapo ni hatari Mhe. Spika.

Mhe. Spika, wananchi wanayaona haya kwamba tunajenga tabaka katika nchi yetu, kwamba kumbe ukitaka uifaidi nchi, maana tumegeuka kunakuwa na wananchi na wala nchi, kwamba kwenye tabaka la wala nchi hawa ni tabaka la wanasiasa akina sisi ndivyo wanavyoamini wananchi, lakini ukipata nafasi kwenye mashirika kama haya unamjua fulani na hapo ndipo.

Sasa ndio maana wanajiuliza kwamba kwa nini mtu akiajiriwa *TRA* au *ZRB*, *ZECO* baada ya muda fulani tayari ana magari, nyumba za kifahari na wala si mambo ya kawaida wananchi wanayaona Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tusije tukatafuta sababu nyingi za kuweza kusababisha mambo kama haya yanayotokezea Bara au sehemu nyengine. Mhe. Spika, vijana hasa wa rika jipya wanaona kwamba hawa wapo kwa ajili ya maslahi yao tu. Sasa Mhe. Spika, hiyo ni *challenge* kwetu na hiyo ndio *point* yangu ya mwisho ambayo nataka kukaa kitako.

Kwa kweli hiyo ni *challenge* kwetu kwa viongozi kurejesha imani ya tunaowaongoza kwa kuonesha kweli tunawatetea watu, kama nilivyosema mzigo huu baadaye unabebwa na mlipa kodi mwananchi masikini ambaye yuko Mkokotoni, Makunduchi, Micheweni ama Mkoani. *(Makofi)*

Naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ripoti hizi zichukuliwe kwa umakini, mapendekezo yake yatekelezwe na kama nilivyosema yale ambayo yalikuwa ni mapungufu basi tutajitahidi kuonesha mapungufu, ili tujirekebishe na pale panapohitaji hatua za kisheria, basi tufuate utaratibu wa kisheria ambao umewekwa ndani ya Katiba zetu pamoja na sheria zetu, ili haki itendeke kwa wote. *(Makofi)*

Lakini nimalizie Mhe. Spika, kwa kusema naipongeza Kamati kwa kazi waliyoifanya na niendelee kulishajihisha Baraza lako na wewe Mhe. Spika, kwamba kazi hii iendelee, ili

wananchi wa Zanzibar waamini kweli kwamba Baraza hili ni ngome yao. Mhe. Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametuwezesha kufika leo kwa salama na kutupa afya njema.

Vile vile nianze kwa *Bismillahi Rahmani Rahiim*, kwa sababu nilipoapishwa hapa Mhe. Spika nilikamatishwa Msahafu kwa mujibu wa dini yangu. Sasa niseme juzuu thalathini kwangu ni kiapo kikubwa sana na kwamba nitatetea, nitalinda kwa uwezo wangu wote kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Pia hivi vitabu vya chama kuna Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuna Katiba ya Chama cha Mapinduzi. Sasa kwa sababu mimi ni mtawala wa Chama cha Mapinduzi na ndio tuliotawala, yaani Chama cha Mapinduzi ndicho kilichotawala Zanzibar pamoja na Tanzania kwa jumla. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kuna mambo yananielekeza kwenye vitabu hivi viwili nivyovitaja mwanzo. Kwa maana hiyo, naomba sana tena naomba kwanza niseme mimi ni muumini wa Chama cha Mapinduzi tena kindakindaki na wala sitokubali kukiona chama changu ndicho kilicholeta serikali kikafanya maovu na akanishtumu yeye mtu wa mwanzo kuliko kukitoa makosa mimi mwenyewe.

Mhe. Spika, kwanza naomba nipongeze Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*), ambayo ilifanya kazi yake ambapo iliombwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, naomba kuipongeza sana Kamati pamoja na Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (*PAC*)), kwa sababu amefanya kazi pamoja na wenzake, kazi ambayo ni ngumu sana, kwa hiyo niseme hongereni. *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii kwa kuipa pole Serikali ya Awamu ya Saba na hasa kupitia kwake mwenyewe Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya mambo ambayo yanayojitokeza kipindi kwa kipindi katika Baraza hili. Kwa kweli niiombe sana serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba haya tunayoyazungumza humu si kwa utashi tu, isipokuwa ni kwa kusaidia na kutaka kuona kwamba tunabadilika hii Serikali ya Awamu ya Saba. Kwa maana hiyo, yale mambo ambayo yamekorogwa huko yasijitokeze tena. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwanza naomba niseme kwamba nampongeza sana mwanangu Mhe. Mansoor Yussuf Himid, kwa sababu ni wachache mno wanaoweza kusimama wakaweza kuipongeza ikiwa ni Kamati Teule au ni Kamati ambayo inafanya wajibu wake kwa mujibu wa taratibu na sheria tulizozitunga humu. Kwa kweli ameeleza aliyokuwa nayo, pia amepongeza na kusema yale ambayo yanapaswa kuchukuliwa hatua hana wasi wasi nayo, huu ni moyo wa kijasiri na mtu akifanya lake mpe lile ambalo anawajibika kupewa. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Spika, mimi nimesikitishwa sana kuona kwamba Waziri muhusika hayupo hata huyo ambaye anakaimu sijui yuko wapi na wala sijui nani anakaimu. Lakini naomba niseme tu Mhe. Spika, kwamba hili si suala la mchezo na wala si la kutumwa mtoto.

Vile vile jambo jengine kubwa hata hao watendaji wale wakuu wa shirika na wizara hawapo na kama wapo basi wengine wamejificha huko nyuma. Kwa hivyo, hii yote ni kuonesha kwamba ah! Si Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tu hao watapiga kelele na wakishapiga kelele mambo yamekwisha na wala hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. Hili kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana.

Na si suala hili tu Mhe. Spika, lolote tunaloona kwamba kwa kweli kuna mambo ambayo yanahusu serikali na yanawahusu wenyewe Mawaziri na watendaji wao wakuu basi huwa watu hawafiki kule juu. Kwa sababu wao ndio watendaji wakuu, waziri ni mwana siasa, wasikilize matatizo ili wakitoka hapa wakawajibike. Lakini tunashangaa sana.

Mhe. Spika, sasa niende moja kwa moja na mimi nitachangia kwa jumla kwa sababu wajumbe walioanza kuchangia kwa kweli wamenifilisi kidogo. Sasa nimezungumzia vitabu hivi ni kuona kwamba dola inakuwa muhimili wa uchumi, lakini uchumi wenyewe ndio huu. Huo uchumi wa kuutafuta ndio huu, unakwenda songombingo.

Mhe. Spika, na mimi nitilie mkazo suala la CAG kwa kweli nimeingiwa na fadhaa. Kwanza nikitizama na hili bora nilizungumze kabisa. Wale wafanyakazi wanaoajiriwa kwa CAG, utamuajiri mtu kwa nia safi lakini matokeo yake ikifika katika miezi sita mpaka imekuja mingi basi mwaka mmoja. Ana magari huyo, ana majumba huyo, ana mambo wewe mwenyewe utashangaa wakati hajatimiza miaka kumi wala ishirini na mshahara wake tunajua sisi tunaompa na si shirika hili tu ni mashirika mengi.

Mimi naiomba serikali tuwe makini na tukiwabaini watu na namna hiyo, tuwaite na tuwahoji, watwambie wamezipataje maana mshahara wako tunaokulipa ni huu haya mengine umepata pataje mpaka ukawa na magari sita, majumba kumi, maviwanja ishirini, naomba Mhe. Spika, tubadilike.

Lakini nitoe mfano wangu mimi mwenyewe, maana mimi siku zote hupenda nijitolee mfano mimi mwenyewe. Mimi nimeingia kwenye Baraza lako tukufu tokea mwaka 1985, nimebakia kipindi kimoja tu nje. Nina nyumba nimeijenga kipindi kile nilichokuwepo nje, nilifikiri itageuka gofu mpaka leo hii miaka 23, nyumba moja sijaimaliza. Kutokanja na matumizi yangu na familia na nini, leo mtu unampa wadhifa tena afisa mdogo tu huyo, ana majumba ana magari, ana maduka, ana mifugo, huwezi kuamini Mhe. Spika, fedha hizi anazipata wapi?

Lakini jengine niwape pole wananchi ule uzigo mkubwa wa shirika la umeme tumewabebesha wananchi. Kwanza huko kulipa umeme kila kituo kinakata pesa zinavyoona yeye. Ukenda kituo hichi unapewa units 13, ukenda kituo kile unapewa units 18, ukenda kituo chengine unapewa units 25, ukenda kwengine wale angalau wanafanya kazi zao kwa uaminifu na uadilifu unapewa units 35 au 38, maana mimi nimeshazunguka vituo kwa kutaka kujua. Huu ni mzigo ambao tumewabebesha wananchi kwa uharibifu wa watu wachache wa Shirika Umeme. Sasa yale mambo ambayo yamejitokeza tunafidia kwa wananchi. Mhe. Spika, mimi Bajeti inayokuja nitakuwa mgumu kweli kwa shirika hili na nitakuwa mgumu kwa wizara hii, mpaka tuhakikishe watu wanajirekebisha ipasavyo.

Mhe. Spika, Mhasibu wa Shirika aliyekuwepo hapa Unguja basi na mama watoto ni Mhasibu wa Shirika lililokuwepo Pemba. Hee, jamani tutakwenda namna hii, maana huyu ananyofoa upande wake na yule anakula upande wake. Si semi kwamba ni makosa lakini asingetafutiwa wizara nyengine. Maana huku kuna madhambi, kule kuna moto, zote ni dhambi Mhe. Spika, hili nalo liangaliwe tena kwa jicho la huruma liangaliwe haraka iwezekanavyo. Si kweli, siamini kama hakutonyofolewa, siamini.

Mhe. Spika, huruma siku zote hailei mwana, kama unampenda mtoto wako mpe kula ashibe vizuri, umfundishe mema yale anayopaswa afundishwe umfundishe, umkataze mabaya, utajiri wake umsomeshe mtoto wako ili ajue kwamba na wewe baadae utamuhitaji. Haya kwa nini nikasema hivi Mhe. Spika. Si kwamba sisi tunaihujumu tu serikali, si kwamba serikali hatuipendi hasa mimi niliyetawala kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, lakini kuipenda serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi sio nikumbatie maovu, sio nibakishe maovu, kwa sababu 2015 nataka nirudi madarakani na kurudi kwangu 2015 Mhe. Spika, yale mabaya ya mtoto niyakataze.

Mhe. Spika, mimi niseme la mwisho kwa sababu wamechangia wenzangu wengi zile dondoo muhimu wameshazizungumzia. Niombe sana serikali na mimi mwisho wangu huwa natoa nasaha za utuuzima. Niiombe Serikali ya Chama cha Mapinduzi hili suala la Kamati liangaliwe kwa uadilifu mkubwa sana, pale panapohitaji kuchukuliwa hatua basi zichukuliwe hatua. Pale panapohitaji uchunguzi mwengine zaidi, tuwaache watu wafanye uchunguzi zaidi. Sisi ni wawakilishi wa wananchi, hata hao wanaofanya madhambi sisi ndio wawakilishi wao. Tusije tukaangalia upande mmoja tukafumbia macho upande mwengine. Tutende haki wanaohusika kutiwa adhabu watiwe, waliokuwa hawawajibiki kutiwa adhabu tusiwatie adhabu ambayo haiwawajibikii.

Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Spika? Hili shirika ni kubwa, kuna wengine masikini za Mungu wanafanyiwa mambo wenyewe hawajui. Lakini wakaja wakajikuta wameingia katika mtego huu. Naomba tutahadhari tutakuja kufanya madhambi makubwa sana. Sisi tunaaminika na wananchi wa nchi hii. Naiomba sana serikali tena naiomba tena serikali nasema mara ya tatu tusiache mambo ambayo hayatotuletea mnasaba mzuri katika serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono japo sipo kwenye mambo ya hoja lakini naliunga mkono hili kabrasha lote hili, lifanyiwe kazi kwa uaminifu na uadilifu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia machache katika ripoti hii ya Kamati Teule ya PAC ambayo imefanya kazi nzuri ya kuchunguza kadhia hii ya Shirika la Umeme, niwapongeze sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wake kwa taarifa hii ambayo ni kubwa na yenye mambo mengi.

Mhe. Spika, ripoti hii ni kubwa hatuwezi tukaichambua yote, lakini yale ambayo yatapewa kipaumbele katika kamati hii na sisi tuweze kuyachangia na kuweza kufanyiwa kazi ili wale ambao wamehusika kwa njia moja au nyengine katika ubadhirifu kwa pesa za walipa kodi wa nchi hii ambazo pesa nyingi zimepotea katika mikono ya wachache.

Mhe. Spika, nianze kwa kusema kwamba mimi mwenyewe nikiwa na imani kubwa kwa Rais wetu kipenzi Dokta Ali Mohammed Sheni nikiwa na imani kubwa na yeye halikadhalika nikiwa na imani kubwa na Waziri husika wa Shirika hili au wa Wizara hii pamoja na Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu ambao hawa wote ni wapya na kadhia hii wameikuta. Imani yangu kubwa kwamba watafanya kazi ya kuhakikisha kwamba wale ambao wamehusika na kadhia hii basi wanachukuliwa hatua ambazo zinaweza kusaidia kwa kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, ripoti hii imezungumza zaidi katika masuala ya umeme katika kisiwa cha Pemba ambayo matatizo mengi yamejitokeza katika kisiwa cha Pemba. Kuna wale ambao wametajwa moja kwa moja, wengi hapa wameyazungumza akiwemo Mhe. Salmin Awadh, Mhe. Ismail Jussa na wengine. Kuna hii kadhia ambayo imetokezea katika muwekezaji huyu wa Wesha. Hapa kumefanyika ubadhirifu mkubwa wa fedha, wizi mkubwa na ushahidi upo wa kutosha na *documents* tunazo hizi za kuhakikisha kwamba fedha ambazo ametumia mfanyakazi huyu kwa jina la Bi Zakia Juma ambazo ni milioni thalathini na saba, laki tisa na elfu ishirini (Sh 37,920,000) alitumiwa katika *account* yake kwa siku mbali mbali.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kuna pesa za kwanza ambazo zilitumwa katika *account* ya bi Zakia Juma ni milioni thalathini (sh. 30,000,000) ambazo zilitumwa tarehe 17/05/2010 katika *account* yake ambayo imetajwa katika kitabu hichi. Halikadhalika kupa pesa ambazo zimetumwa nyengine ya tarehe 28/7/2010 ni milioni mbili laki mbili na ishirini, (sh. 2,200,20) kuna pesa nyengine ni milioni moja na laki sita (sh. 1,600,00) ambayo imetumwa tarehe 23/8/2010 na kuna pesa nyengine ambazo zimetumwa tarehe 30/8/2010 ikiwa ni milioni moja laki sita na sitini (sh. 1, 600,60) Huu ni ushahidi tosha kwamba mfanyakazi huyu alikwenda kinyume na maadili ya kazi ambayo amepewa na Shirika la Umeme.

Mhe. Spika, ushahidi huu ni wa uhakika kwa hivyo ubadhirifu wa fedha hizi ambazo zimetumika ambazo katika malipo ambayo yameingia katika Shirika ni milioni mbili na elfu hamsini na mbili mia sita na tisini na sita. Ukiangalia tu kwamba katika milioni thalathini na saba, takriban milioni thathini na tano zimeingia katika mifuko wa wajanja.

Katika kuthibitisha hilo Mhe. Spika, huu ni mtandao mkubwa kwa sababu huyo hayupo peke yake, wapo na wenzake. Taarifa tulizonazo za uhakika mpaka muhasibu wa Shirika Unguja na Pemba wamehusika katika kadhia hii. Muhasibu wa Unguja na Pemba ni bibi na bwana ni mtu na mkewe na halikadhalika huyu bi Zakia hata mumewe anafanya kazi katika Shirika hili. Ndio maana nikasema kama ni mtandao mkubwa ambao umehusika na kadhia hii.

Mhe. Spika, tumethibitika kusema haya kwa sababu ripoti ndivyo inavyosema imewataja hawa na sisi ndio tukawataja, ingelikuwa haikuwataja humu katika ripoti na sisi tusingewataja, lakini katika ripoti hiyo wametajwa na ushahidi umeonyeshwa katika kadhia hii. Lakini tukitoka hapo kwa kuthibitisha kwamba kuna majungu, kuna fitina, kuna ubadhilifu, kuna wizi.

Mhe. Spika, mbali na wizi huu ambao umefanyika kuna bwana Muhammed yumo katika kitabu hichi ambaye na yeye pia kalipa pesa katika Shirika za kununua nguzo tatu lakini pesa zile ambazo zimelipwa na bwana Muhammed Habib wa Kigongo huyu. Wakati Kamati ripoti hii ilivyokuwa inaonesha kwamba fedha zile zimelipwa wakati wa kuangalia hakuna risiti za malipo

ambazo zimelipwa shirika, watu wametia pesa mfukoni, kazi imefanywa, pesa za umma zinapotea, shirika halipati kitu, serikali haipati kitu, wananchi wanaumia.

Mhe. Spika, hapa nakuna kutafuta mchawi, wachawi wameshapatikana kwa hivyo lililobakia serikali kuichukua ripoti hii na kuifanyia kazi, yasije yakatokea yale ya katika ripoti iliyopita kama wenzangu walivyosema, itakuwa tunakuja hapa tunapiga kelele, tunatia posho mfukoni, tukifika mitaani tunaulizwa maswali hatuna la kujibu. Kwa sababu yale yanayozungumzwa hapa yafanyiwe kazi.

Kama alivyosema Mhe. Salmin Awadh kwamba Chama cha Mapinduzi kinakemea haya na inalani haya kwa nguvu zote. Kwa hivyo mtu asije akasema kwamba haya yanafanywa na wale ambao wanatoka katika Chama cha Mapinduzi. Sio kweli, hawa wote waliofanya tuna hakika kwamba sio wanachama wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, kuna wengine ambao wamehusika na kadhia hii hata kama hawapo tena katika madaraka lakini wale waliohusika wachukuliwe hatua. Ametajwa hapa Mwenyekiti wa Bodi, kahusika kwa asilimia mia Mhe. Mohammed Hashim, katajwa, sikumtaja mimi, hakumtaja mwengine katajwa na Kamati ambayo imekwenda kuchunguza na kwa ushahidi ambao wameuona, isije ikasemwa kwamba Jazira kamtaja Mohammed Hashim, Mhe. Salmin Awadhi kamtaja Mohammed Shamte, wametajwa na Kamati ambayo umeiteuwa wewe Mhe. Spika, kwenda kuchunguza na wamethibitisha haya.

Mhe. Spika, naiomba sana Serikali yetu ya Mapinduzi Matukufu ni serikali ambayo ina mfumo umoja wa kitaifa, iwachukulie hatua hawa ambao wamehusika. Nimezungumza mwanzo hapa kwamba nina imani kubwa na Rais wetu wa Zanzibar Dokta Ali Mohammed Sheni. Bahati mbaya kiongozi wetu wa Baraza letu sasa hivi hayupo lakini Waziri muhusika ambaye ana kaimu Wizara hii anasikia. Tutakapokuja katika kuletewa majibu ya ripoti hii yaje majibu ambayo ya kuchukuliwa hatua hao ambao wamehusika na kadhia hii.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja ripoti hii na nawaomba kwa heshima na taadhima ripoti hii wale ambao wamehusika wachukuliwe hatua. Wasipewe lawama wale ambao wapya, nimezungumza hapa mawaziri, makatibu wakuu, ambao ni wapya. Lakini wale ambao wamehusika katika kadhia hii wachukuliwe hatua. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo hapa asubuhi hii katika kuendeleza majukumu yetu ya kitaifa ambayo tumetumwa na wananchi.

Pia nachukua nafasi ya kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi ijapo kwa muhtasari nitoe mchango wangu kwa mujibu wa ripoti ya kazi maalum ya Kamati ya PAC ya kuchunguza Shirika la Umeme na mimi nikiwa ni mmoja katika wajumbe wa Kamati hiyo.

Mhe. Spika, nitakuwa mchache sana wa fadhila kama sikumpongeza Mwenyekiti wangu Mhe. Omari Ali Shehe jinsi ya umakini wake alipoiwasilisha ripoti hii kwa muda mrefu na kwa *speed* ile ile ya ukakamavu wake ambao ulionesha umakini na wajumbe wameifahamu vya kutosha.

Lakini pia nachukua nafasi ya kuwapongeza pia Makatibu wetu kutokana na kazi ngumu ambayo walikuwa wakipambana nayo katika kuendeleza kazi yetu hii pia naipongeza kamati kwa jumla.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi wangu huo mimi mchango wangu utakuwa katika ukurasa wa 15 tukirejea nyuma kidogo unaozungumzia hadidu rejea nam. 1 ya upotevu wa fedha unaotokana na uungwaji wa umeme ambao waungaji hawa hawakuwa na uaminifu.

Mhe. Spika, kwa kweli tatizo hili la uungwaji wa umeme kwa watu wetu au wafanyakazi ambao hawakuwa waaminifu. Suala hili linaonesha dhahiri kwamba hapa panakuwa na upotevu mkubwa wa fedha na zinapotea fedha hizi kiholela, lakini zinapotea kuingia katika shirika yaani kuingia katika mapato ya serikali, lakini fedha hizi zinaingia katika mifuko ya watendaji wasiokuwa waaminifu.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie kuhusu wateja ambao wachache tu walioidhinishwa hapa katika hii ripoti, halafu tuangalie hii tofauti iliyopo kati ya mteja mmoja na mwengine. Tunasema kwamba kuna bwana Juma Dadi wa Chokocho ameunganishiwa umeme kwa masafa ya nguzo moja na *roof poll* moja ambapo vifaa vyote ni ya shirika, ameunganishiwa tarehe 22/02/2012 akiwa amelipia huduma hiyo kwa shilingi laki nne na arubaini na mbili elfu, mia tano tisini na tatu (Sh. 442,593). Wakati bibi Zuhura Nasir Nassor huyu yupo katika jimbo langu la Chambani, bibi huyu ameunganishiwa kwa masafa hayo hayo ya nguzo moja na *roof poll* moja kwa jumla ya shilingi milioni moja laki mbili thalathini na sita elfu mia saba arubaini na saba (Sh. 1,236,747). Hapa kuna tofauti ya karibu shilingi laki saba kati ya mteja wa kati na mteja wa pili. Hebu tuangalie shilingi laki saba hizi zimekwenda wapi, zimekwenda mikononi mwa mfanyakazi ambaye alikwenda kuwaunganisha au zilikwenda kwa Shirika.

Mhe. Spika, nikienda katika ukurasa wa 16 kuna malipo wanayolipa wateja yanayotofautiana na risiti wanazopewa wateja. Mhe. Spika, hili ni tatizo na ni tatizo ambalo linawanyanyasa wananchi wetu na linawanufaisha baadhi ya watendaji wasiokuwa waaminifu. Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa heshima kubwa tunawaomba watendaji waliopewa majukumu ya kusimamia Idara, Mashirika au Taasisi zozote, wajitahidi kuwa wakweli, kuwa waaminifu, kuwa waangalifu katika kazi ile waliyopangiwa. Tunapotunga sheria tunaangalia vipengele mbali mbali ikiwemo siku nyengine Mwenyekiti wa Taasisi fulani au Mkurugenzi au Meneja wa Taasisi fulani tunamuangalia yule je, mtu huyu anatakiwa awe na kiwango gani cha elimu, hatutaji kuwa na kiwango cha elimu cha juu kwa sababu apate sifa kwa elimu yake. Tunamtaja angalau mtu huyu ana digrii moja au mbili au vyenginevyo. Madhumuni makubwa ni kutaka kuwa awe muadilifu, awe msimamizi mzuri katika taasisi yake anayoisimamia. Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha sana kwa shirika hili la umeme kuona kwamba usimamizi wa baadhi ya watendaji ni mbovu, usimamizi ambao unahimiza mno kuingiza fedha katika mifuko yao bila kuziingiza katika shirika.

Mhe. Spika, kwa sababu tumeleta ripoti hii nikiwa mmoja katika Wajumbe tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi waichangie kwa mapana sana ili serikali iwawajibishe kila ambaye anahusika na kadhia, ubadhirifu, au ukosefu wa kusimamia kazi yake vizuri.

Kwa haya machache kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani ninaiunga mkono ripoti hii kwa asilimia 100 na wanaohusika wachukuliwe hatua ya kinidhamu. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kupata nafasi hii fupi ya kuweza kutoa mawazo yangu machache juu ya ripoti hii ya Kamati Maalum iliyochunguza Shirika la Umeme.

Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kufika hapa nikiwa mzima kwa uzima wangu na kutuwezesha sote kufika katika Baraza hili kuja kutekeleza majukumu yetu ya kawaida ya kazi zetu. Pia nikupongeze wewe Mhe. Spika, katika kutuongoza katika shughuli zetu za Baraza.

Mhe. Spika, serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inafuata utawala bora na inasimamia haki, haki upande mmoja inasema inasimamia haki, humu mna watu wa aina mbili, upande mmoja unasimamia haki wanamaliza hapo haki. Upande mmoja unasimamia haki wanasema haki sawa kwa wote. Sasa katika mambo kama haya ningeomba hawa wa pili hawa hii *slogan* yao ichukuliwe kuwa haki yenye sawa kwa wote.
Mhe. Spika, nilipoangalia mimi ripoti hii kwa kweli kidogo imenisikitisha kuona shirika letu ambalo linahitaji kutoa huduma kwa wazanzibari kupata nishati hii muhimu ya umeme linavyotoa huduma zake hizo.

Kabla sijachangia chochote ningetazama lile deni ambalo kamati hii imeona kwa shirika inadaiwa na shirika kwa upande wa pili. Karibu bilioni ishirini na mbili na milioni kadhaa, tulichukulie Mhe. Spika, Shirika hili ni mtoto kwa wazanzibari. Na wazanzibari wote milioni moja na laki tatu iwe ndio wazee tukae kitako kujadili kwamba mtoto wetu anadaiwa, kwa hivyo tumlipie deni lake. Sisi wazee sote tukikaa pamoja tukigawana deni kila mzee mmoja atachukua deni la karibu shilingi milioni 15. Kama ingekuwa mtoto huyu deni hili anayemdai kamshtaki na atalichukulia hatua kali za kisheria. Sisi tukaamua mtoto wetu asichukuliwe hatua hizo tukae kitako tugawane deni kila mmoja angelichukua zaidi ya shilingi milioni 15. Hapa naonesha kuwa jinsi hili shirika linavyoongoza shughuli zake sijui linafanyaje hata likawa na deni la kiasi hicho, kulingana na ripoti hii mpaka likambebesha kila Mzanzibar kiasi hicho cha deni. Nadhani kutokana na madeni hayo ndio maana ikawa huduma zao na malipo tulilolipa ikawa si *stable* yanaongezeka mara kwa mara, pengine sina hakika wanataka kufidia hii hasara au hili deni ambalo wanadaiwa.

Mhe. Spika, kutokana na kitabu hiki Shirika hili, linatoa huduma kwa watu aina tofauti wenye huduma ya aina moja kwa malipo tofauti hii ina maana kuwa watu wanahurumiwa na kuna watu wanakomolewa. Hapa kuna mtu katajwa katumia nguzo mbili katika kuunga umeme kalipa laki moja na kidogo. Kuna mtu katumia nguzo moja kalipa laki tano, na sijui haya mahesabu yamekwendajekwendaje mpaka mwenye kutumia nguzo nyingi alipe kidogo, aliyetumia nguzo kidogo alipe nyingi. Hapa inaonesha hii huduma inakwenda kiujamaa jamaa, kiupendeleo pendeleo, kiudugudugu, kiami, kiujomba. Kwa sababu mimi si mtaalamu wa mahesabu lakini mmoja kalipa nyingi wa pili kalipa kidogo. Ndio nasema mimi kama nguzo moja kalipa tano na kwa hivyo nguzo mbili alipe tano na mara mbili kwa hesabu za wakati wangu mimi. Kumbe hesabu za leo ni *vice versa* kila ukitumia zaidi unalipa kidogo na ukitumia kidogo unalipa kingi. Kwa nini kwa kweli sijui tofauti hii kujitokeza.

Kwa hivyo Mhe. Spika, jambo hili linahitaji lichunguzwe kwa makini na mimi sitaki jambo hili liwe mtego wa panya, watu wanapompata panya kwa kuweka kitoweo kama samaki hata paka akipita atanasa haidhuru siye aliyekusudiwa. Kama utatumia ndizi hata komba kwa sababu anakula ndizi atanasa kumbe hajakusudiwa komba kakusudiwa panya. Hivyo basi yoyote atakayebainika kahusika kwa njia moja au nyengine, awe yeye ndie yeye ili ile dhana ya haki kwa wote iende pale. Kwa sababu mtu asiadhibiwe mwengine, Mhe. Spika, hapa ilioneshwa hii hoteli ya Misali Pemba ambayo kwa ripoti hii risiti ya malipo ni milioni mbili na kidogo, lakini Kamati ilipokwenda iligundua kuwa huyu mlipaji kalipa karibu milioni 37 na kati ya hizi kwa kuwa risiti milioni mbili na kidogo hizi ni za Shirika, hizi nyengine labda zitakuwa za washirika. Hapa patakuwa pana Shirika na washirika. Shirika itakuwa ni ile taasisi na washirika watakuwa ni wale walioshirikiana kufanya risiti iwe milioni mbili na kidogo lakini wamedai milioni 37 na kidogo sasa zilizobakia labda zimekwenda katika mikono ya washirika.

Mhe. Spika, utumishi wa aina hii tuufanye upitwe na wakati. Sisi katika nchi hii tunakwenda kwa ombaomba. Leo kama yule tunayemuomba na akatusaidia hatimae akasikia namna hawa wanavyosaidiwa wanavyojiendesha wanatumia pesa, kwa kweli itafika pahala tuwavunje moyo hata kama zile tulizoziharibu hawajatusaidia wao. Lakini kwa kuwa ubadhirifu umetokea na chombo hiki kinausema bayana tunawambia sisi tunaosaidiwa tuko hivi, mnachotupa mnachotusaidia kinakwenda kwenye mifuko yetu kuliko kule kulikokusudiwa. Sasa tukiwajenga dhana hii washirika wa maendeleo, *donors* wetu tutafika pahala watuache mkono kati kati ya bahari na pengine kuogelea hatujajua, matokeo yake tutazama na tufe.

Mhe. Spika, jambo hili lazima serikali ilichukulie hatua wanaohusika kuchukuliwa hatua. Mhe. Spika, wananchi wanaotusikiliza, wananchi tunaotuwakilisha na wananchi ambao serikali inawaongoza wanasikiliza zile *concerns* ambazo wajumbe wa Baraza wanazipeleka serikalini, je serikali inachukua hatua gani? Lakini serikali haichukui hatua yoyote sisi watatuona kama ni watu tunampigia mbuzi gitaa tu. Kwa kuwa tunafanya jambo na hatimae serikali haichukui hatua. Na wale ambao wanaoshtumiwa kwa kufanya moja au jengine pia hizi kamati itafika siku Mhe. Spika, iwe hazina thamani kwenda katika Taasisi za serikali, wataona vinyago tu vinakuja, tujitahidi wasijekufika wakatuweka hapo wakati huo tutakuwa hatuna maana yoyote si wanapiga kelele tu na sisi tunafanya yetu. Hii lazima serikali ijitahidi isimuonee mtu lakini pia isimpendelee mtu. Isimchukie mtu lakini pia isimpende mtu, isimdharau mtu ambaye hadharauliki, wala isimtukuze aliyekuwa hatukuziki.

Mhe. Spika, suala hili ni muhimu sana kwa sababu shirika hili ndilo shirika pekee ambalo linatoa huduma hii ya nishati ya umeme. Kama ingelikuwa nchi hii ina shirika jengine imani yangu shirika hili lingepoteza zaidi ya asilimia 60 ya wateja wake. Lakini kwa bahati niseme mbaya hakuna shirika jengine ambalo linatoa huduma hii ya nishati na katika mtaa Mhe. Spika, kukawa na duka moja tu muuzaji atafungua wakati anaotaka kwa sababu wateja hawana pa kwenda lazima watakuja kwangu mimi. Nadhani huduma hizi ambazo hazina mpangilio maalum kwa sababu shirika linaona mteja akitaka atatumia umeme wa ZECO hataki atatumia wa ZECO kwa sababu mwengine wowote wa kutumia jua bado haujakuwa na nguvu yoyote wala hauwezi ukakidhi mahitaji ya wazanzibari.

Kwa sasa hili shirika lijione kwamba linategemewa na wazanzibari kwa hivyo liwahudumie wazanzibari kadri ya uwezo wao kwa haki na upendo, hili ni shirika la biashara. Mara nyengine

mteja anaomba huduma ya umeme akazungushwa wee wao wanafanya biashara, lakini mteja wanamuhangaisha, kwa hivyo ile lugha ya kitanzania kuwa *mteja ni mfalme* hapa haipo katika shirika hili mteja ni mtwana. Na nchi hii haina watwana, kuna watumishi na wanaotumikiwa. Kuna viongozi na wanaoongozwa, kwa hivyo basi Mhe. Spika, mimi nimalizie kwa kuiomba serikali waiangalie kwa makini ripoti hii na katika kipindi ambacho kamati imependekeza, tuiombe serikali ije na majibu sahihi yasiyo na upendeleo wa aina yoyote ili kila ambaye kahusika kwa namna moja au nyengine, hatua za kisheria zichukue mkondo wake.

Mhe. Spika, ninaiunga mkono ripoti hii mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia ripoti ya Kamati ya Fedha, lakini vile vile nawapongeza wajumbe wa kamati teule ambao wamefanya kazi hii nzuri kiasi. Vile vile niwapongeze wachangiaji wenzangu ambao wametangulia.

Mhe. Spika, moja kwa moja na mimi niende hasa katika hadidu rejea nambari moja kuanzia na kipengele cha mwanzo upotevu wa fedha unaotokana na uungwaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasiokuwa waaminifu. Katika hili kuna kifungu cha (a) kinazungumzia tofauti ya malipo kwa kazi wanazofanyiwa watu, kazi ambayo inafanana au ile kazi moja inakuwa kubwa lakini malipo yake yanakuwa madogo na ile kazi ndogo inakuwa na malipo makubwa. Mhe. Spika, hiki ni kitendo kibaya sana kwa sababu mimi nilipoangalia majina ya watu hawa niliamini moja kwa moja hawa ni raia wa Tanzania na ni wakaazi wa Zanzibar kwa mujibu wa sheria. Lakini kuna tofauti kubwa ya upendeleo unaooneshwa na watendaji wetu wa Shirika la Umeme. Kwa hivyo Mhe. Spika, kitendo hiki ni kitendo kibaya na hakistahili kabisa kufumbiwa macho. Kwa hivyo kila aliyehusika na kadhia hii achukuliwe hatua za kinidhamu hasa zile za kisheria ili kuonesha kwamba Zanzibar inaongozwa kwa mujibu wa Katiba na sheria za nchi zilizopo.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kifungu cha (b) kinazungumzia malipo wanayolipa wateja kwa kazi ambapo hutofautiana na thamani na malipo yaliyomo kwenye risiti. Mhe. Spika, hivi sasa tumeona moja kwa moja kwamba watu wanalipa pesa nyingi lakini badala yake zinazoingizwa katika risiti za serikali ni pesa kidogo sana. Hii ikithibitika kwamba kitendo kinafanyika basi huu ni wizi, na kama pana wizi si kitendo cha kufumbiwa macho nacho kichukuliwe hatua za kisheria kuliko zile za kinidhamu.

Mhe. Spika, tukiangalia mfano mzuri wa malipo haya tunakuta katika hii hoteli ya Pemba Misali ambayo imezungumzwa sana hapa tumeona tofauti kubwa ya zile fedha ambazo muwekezaji huyu alizilipa, mbali ya hayo pia kwamba sasa hivi watu wamekuwa wakitumia *account* zao binafsi kwa kuhifadhi pesa za serikali, jambo hili ni baya sana. Hatujawahi kusikia duniani kwamba watu sasa wanaweka *account* zao kwa kuweka pesa za serikali. Kwa hivyo hawa waliohusika na jambo hili wachukuliwe hatua za haraka ili wananchi wetu wawe na imani na serikali yetu hii. Kwa sababu Mhe. Spika, hapa inaonekana dhahiri kwamba kuna watu hawana nia njema na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wanachotaka wao kila siku serikali yetu ilaumiwe. Sasa sisi hatuko tayari kwa kitendo hichi, hapa serikali ichukue hatua za haraka ili kudhibiti hali hii na kuonesha wananchi hatua zipi zilizochukuliwa kwa ajili ya kuwaadhibu watu hawa ili kitendo hiki kisiendelee kwa watu wengine.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele katika hadidu rejea hii namba moja kuna kifungu cha ‘c’ kuwepo kwa upendeleo kwa sababu husababisha usumbufu kwa wananchi jambo ambalo hupelekea kuzaliwa kwa rushwa. Upendeleo Mhe. Spika, ni kitu kibaya sana, hatutaki tuongozane watu kwa ubinafsi, upendeleo kuonekana wengine wana haki na wengine hawana haki. Watu wote ndani ya nchi hii wanazo haki sawa kwa mujibu wa sheria. Mhe. Spika, nalo hili lichukuliwe hatua za kinidhamu, lakini vile vile hatua za kisheria.

Mhe. Spika, katika hadidu rejea hii namba moja vile vile kuna kifungu cha (d) hapa kinazungumzia malipo yanayolipwa bila ya risiti. Sasa hivi watu katika Shirika la Umeme wamekuwa kama wanakwenda kununua mchele wa kilo dukani kwamba unakwenda unanunua mchele unaondoka. Kitendo hiki ni kitendo kibaya nacho kinapaswa kuangaliwa kwa umakini mkubwa zaidi kwamba risiti hazitolewi, hili hasara yake Mhe. Spika, linaweza likapelekea mtu aliyepata zile huduma akalipa zile fedha, lakini ataonekana kwamba yeye hajalipa zile fedha, jambo ambalo ni baya nalo linatakiwa lichukuliwe hatua.

Mhe. Spika, tukiacha hayo kuna kifungu kinachozungumzia wateja waliotembelewa Unguja. Hapa tumeona kuna mtu yeye amewekewa nguzo 31 na transfoma lakini kile alichokilipa ni shilingi milioni nne laki mbili na elfu hamsini na tisa mia saba na thamanini na saba, ukiangalia hii utaikuta katika ukurasa kuanzia 40 na kuendelea mbele. Kwa hivyo Mhe. Spika, nchi hii inaongozwa kwa sheria na taratibu za nchi walipa kodi wetu kwa kweli ni wanyonge jambo ambalo linapelekea hadi hivi sasa Shirika la Umeme limeshindwa kabisa na ningethubutu kusema Shirika hili lilikuwa livunjwe kabisa lakini umeme kutokana na umuhimu wake mkubwa hatuwezi tukasema hivyo. Hadi hii leo miaka 49 ya Mapinduzi kuna vijiji hasa umeme wanausikia ama wanauona wanapokuja mjini tu basi, lakini kama hakuna huu wizi unaofanyika na ubadhirifu wa fedha, upendeleo uliopo basi mimi naamini kwamba wananchi wetu wangepata umeme. Leo Wizara inayohusika na masuala ya umeme tunapowauliza kuhusu utekelezaji wao katika ahadi walizoziweka vijijini kila siku tukisimama hapa unaambiwa bajeti ijayo, bajeti ijayo, bajeti hiyo sijui itafika lini, sijui kama si siku ya kiama umeme utakuwa haujapatikana.

Kwa hivyo Mhe. Spika, pamoja na kwamba watendaji wetu wanaonekana kwamba si waaminifu au si wa kweli, lakini ipo haja wizara yenyewe sasa kujisahihisha, kujirekebisha lakini nao pia kufanya uchunguzi juu ya watendaji wa namna hii. Kwa sababu siku zote tutakapowaachia Kamati Teule kuna mambo si kwamba Kamati Teule ziundwe Barazani zikafanye kazi lakini kama Wizara imepewa jukumu la kusimamia hii taasisi nayo ina wajibu wa kufuatilia na kuangalia upotevu wa fedha pamoja na mambo mengine yoyote ya ubadhirifu ambayo yanafanywa katika maeneo yao.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kwa kumalizia tunaangalia katika hadidu rejea, taratibu za ajira kwa upendeleo pamoja na nyongeza za mishahara kwa wafanyakazi wa Shirika. Mhe. Spika, taratibu za ajira zinajulikana zipo tumepitisha sheria sio zamani mwaka 2011 tumepitisha sheria hapa ambayo inaongoza taratibu za ajira. Na ninavyoamini watendaji wakuu wote wa serikali sheria hii wanaijua inataka nini na inasema nini katika haya. Lakini bado kwamba taasisi hii tunaiona imegubikwa na masuala ya upendeleo, upendeleo uliopo hawa wa kuajiri watu, Zanzibar hatuna makabila lakini sijui kwa mujibu wa kitu gani ambacho wao wanaona ni kigezo. Mara nyengine watu kwa taratibu za kawaida mtu anayeomba ajira atimize hayo ndipo aajiriwe, lakini wao bado tatizo hili lipo la kupendelea watu kuona kwamba hawa wanafaa na hawa hawafai. Mhe. Spika,

huku tunakokwenda ni kubaya zaidi, kufika pahala leo kwamba watu wanabaguana kwa sababu pengine huyu katoka wapi huyu anaamini nini katika siasa, jambo hili litatupeleka pabaya kule tunakotoka nyuma na tutakaokwenda mbele kwa hivi sasa.

Mhe. Spika, pamoja na upendeleo katika ajira hata katika mishahara nyongeza kuna wafanyakazi tumeona katika ripoti hii kwamba wamesoma, wameongeza ujuzi lakini mishahara hawataki kuwaongezea. Na wao wana haki ya kuongezewa mishahara, kwa sababu kwa mujibu wa katiba mtu anapofanya kazi basi alipwe kiwango kinacholingana na kazi ambayo anayoifanya lakini hadi hivi sasa Mhe. Spika, kunaonekana kuna watu wao ndio mabwana na wengine watwana. Mhe. Spika, Mapinduzi ya Zanzibar hasa lengo lake kubwa kuondosha hizi tofauti baina ya watu, inataka watu wote wapate huduma sawa wawe sawa mbele ya sheria, jambo hili ni baya nalo si jambo la kufumbiwa macho.

Mhe. Spika, tunaitaka serikali kwa hili ituletee maelezo ya kutosha juu ya hatua ambazo itazichukua tulizozipendekeza sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hapa isije ikatufanyia kama ripoti iliyopita hatutokuja kukubaliana nayo hiyo, tunachotaka kwamba maamuzi yatakayotolewa na serikali sisi tuamini kwamba yemefanywa kwa haki lakini pia wanachi wetu wanaotusikiliza na kutuangalia waone kwamba sisi Wawakilishi wao tunafanya kazi ambayo wametutuma kuja kufanya hapa, chengine chochote hatutokuja kukikubali. Au bora kwamba sisi acheni tuseme tu hapa tupige makelele lakini tusiletewe maamuzi ambayo hayatoturidhisha kabisa.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chaani naunga mkono hoja hii.

Mhe. Spika: Mhe. Abdalla kuna dakika kama kumi sijui kama zinakutosheleza nikiona unasimama kuchangia basi nitasema zinatosheleza.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Spika, japo dakika chache kwa vile nimepitia ualimu nitafanya *summary* ya kile nilichokikusudia. Na mimi ninashukuru adhuhuri hii kunipatia fursa kusema machache ambayo wengi naona wameshayasema lakini kwa ujumla Mhe. Spika, mimi ni imani yangu kwamba ripoti hii imeleta mengi sana. Labda wale waliokuwa vipofu basi wameshaona na wale waliokuwa viziwi basi wameshasikia na wale ambao hawafahamu nina imani wameshafahamu. Wameshafahamu, wameshaona, na wameshasikia nini kinatokea katika shirika la umeme, sisi tulitumwa kazi Mhe. Spika, ulitutuma wewe na kazi hii tumeshaifikisha kwako.

Lakini katika nchi hii Mhe. Spika, kunakuwa na mihimili 3. Mhimili mmoja ni wetu sisi ambao wewe ndio kiongozi wetu, kazi yetu tumeshaikamilisha, lakini kuna mihimili mengine miwili hii inayoitwa ya *executive* na *judiciary* na wao wana kazi wasikae bure, sasa sisi tunasubiria kuona nini *executive* watafanya na nini *judiciary* watafanya. Ninafikiri ripoti hii imetuonesha mengi kuna wale wanaohusika moja kwa moja *executive* wafanye wajibu wao basi tunawaomba *executive* wafanye wajibu. Na kuna wale ambao tunawahisi kwamba wao watahusika kwenda katika *judiciary* basi na wao wafike katika *judiciary* ili vyombo hivi navyo vifanye wajibu wake. Tusije tukafika wakati tukaonana wabaya kwamba mhimili mmoja umekuwa mkorofi, na mihimili mengine sote mihimili hii mitatu tunafanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba

nchi hii inakwenda katika hali inayotarajiwa kama wenzetu wanavyokwenda huko nchi nyengine.

Mhe. Spika, ripoti hii imetuonesha mengi mimi sitaki nirejee kwa sababu kila mtu anayejua kusoma akisoma ripoti hii atafahamu. Kama nilivyosema mwanzo isipokuwa kuna mambo machache sana nataka niya-*emphasize*. Mhe. Spika, kuna mwandishi mmoja wa vitabu kule nchini Uingereza anaitwa William Shakespear yeye alitunga tamthilia yake moja inaitwa *hamlet* na katika tamthilia hii lengo lake kumtafuta nani anahusika na mauaji katika kundi la watu. Yeye mwisho katika mchezo ule alijiuliza yeye mwenyewe mwandishi katika kufanya *conclusion* kwa sababu hakujua nini la kufanya akasema yeye katika *conclusion* yake kwa maneno machache sana alisema *to be or not to be that is a question.* Kwa hivyo kuwa au kutokuwa kwa jambo hili hilo ndio suala, *that is a question,* sasa na sisi tunajiuliza tena jambo hili litakuwa huyu mchawi keshajulikana, ndio sasa Mheshimiwa kwa vile mchawi keshajulikana ninafikiri adhabu ya mchawi inajulikana ni nini.

Mhe. Spika, ripoti hii pia imetuonesha mengi yaliyojitokeza, kuna watu ambao ninahisi ni wao ni *tax payers* wakubwa katika nchi hii, lakini nashangaa kwamba watu hawa sijui kwamba ripoti imewataja na wao watakaokwenda katika vyombo vya sheria au la. Kuna watu ambao wamejionesha dhahiri kwamba walikuwa wanajua nini wanachokifanya. Haiwezekani watu katika nchi hii anajua kwamba malipo ya serikali yanaingizwa katika akaunti za serikali na sio akaunti za watu binafsi. Lakini akaingia moja kwa moja na akakubali ushauri wa mfanyakazi akakubali kuziingiza fedha zile katika akaunti ya mtu binafsi, hili alikuwa analijua ni kosa kwa sababu watu hawa ni *tax payers* wanalipa *tax* kwa kipindi kirefu sana. Sasa inakuwaje aje mtu binafsi akwambie ingiza pesa hizi katika akaunti yangu na wewe ukubali kuziingiza. Nahisi ripoti haya imeyasahau, kwa hivyo naomba na wao katika kuchukua hizo hatua aidha za *executive* au za *judiciary* basi na wao wakaangaliwe kuwa walifanya kosa. Kwa hivyo adhabu ichukuliwe kutokana na makosa yao.

Jengine Mhe. Spika, ni kwamba tumejifunza tena tuna chombo chetu kinachoitwa CAG ambacho ninahisi ndicho kinacho-*control* mambo ya udhibiti wa matumizi, Mhe. Spika, ninahisi chombo hichi nacho kina kasoro. Kwa hivyo hivi sasa tunatakiwa kiangaliwe kwa makini sana, kwa sababu kila mwaka kinatuletea ripoti Barazani. Lakini sasa kwa mwendo huu nahisi nacho tukitilie wasiwasi, kwa sababu ripoti zake nyingi zinazokuja hazioneshi mapungufu kama haya. Na labda nijiulize wao wanakuwepo wapi.

Sasa labda Mhe. Mwenyekiti ile kasma yao tunayowapelekea tukaigawa ikaletwa hapa katika Baraza ili tukawezeshwa sisi Kamati hasa ile ya PAC au hizo kamati za kuteuliwa basi zikaweza kufanya kazi. Si hivyo itakuwa tuna-*march time*, kwa sababu mimi siamini kuanzia leo hii kwamba hizi kamati kweli inakuwa inatenda yale ambayo imekusudia iyafanye. Lakini Mhe. Spika, liloniumiza sana ni kwamba haya Mashirika yetu yanakuwa chini ya Wizara, sasa je hii Wizara ambayo inayohusika na Shirika hili, muda wote huo ilikuwapo wapi, hivyo mimi sitokuwa na haki hapa Mhe. Spika, kusema kwamba na Waziri aliyehusika na Wizara hii ambalo Shirika liko chini ya Wizara yake na yeye alikuwa na wajibu au sisi tuna haki ya kumwambia na yeye aondoke. Mimi ninafikiri umeshafika wakati na sisi tusimfumbie macho, huyu ameshindwa kuliendeleza hili Shirika. Ulipotokea uzamaji wa meli Mhe. Spika, Waziri hakuwa yeye hakuwa abiria, hakuwa na mzigo, hawakuwa *engineer* wala hakuwa nahodha lakini chombo hiki kilisema

huyu anahusika. Ninashukuru kwamba aliona na akawa muungwana, yeye akaondoka mara moja katika nafasi ile. Sasa na huyu tuliyempa kulishughulikia shirika hili na yeye ana wajibu wa kuona sasa imefika wakati mimi wajibu wangu sikuutekeleza kwa hivyo natakiwa niondoke.

Mhe. Spika, kwa hayo machache, naona muda umefika ninakushukuru.

Mhe. Spika: Ninakushukuruni Waheshimiwa Wajumbe kwa michango ambayo tumeshaitoa hadi kufikia wakati huu. Ipo orodha ndefu kidogo lakini tutaishughulikia jioni. Isipokuwa tunasisitiza kwamba tunategemea michango yote tumalize jioni ili kesho kipindi cha asubuhi baada ya maswali, tumuombe Mhe. Mwenyekiti afanye majumuisho na hatimae kumalizia hoja hii kipindi cha asubuhi.

Waheshimiwa Wajumbe kuna taarifa moja ndogo, Waheshimiwa Wawakilishi wa upande wa Chama Cha Mapinduzi wanategemewa wawe na kikao mara baada ya kuondoka humu ndani pale ukumbi wa juu. Kwa hivyo mnaombwa kuhudhuria kwenye kikao hicho.

Baada ya hayo naomba basi Waheshimiwa Wajumbe sasa niakhirishe kikao hiki hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 07.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia Ripoti Maalum iliyotolewa na Kamati ya PAC kuchunguza utendaji wa Shirika la Umeme.

Awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kuwepo hapa leo jioni hii tukiwa wazima wa afya na aliyetupa uwezo wa kuja kuendelea kufanya shughuli yetu iliyotuleta hapa.

Mhe. Spika, mimi nachukua fursa hii vile vile kuipongeza Kamati ya PAC kwa kazi yao nzuri ambayo wameifanya, naamini kwamba kazi hii ilichukuwa muda wao mkubwa, lakini vile vile kazi hii wameifanya kwa bidii kubwa sana. Mhe. Spika, hii inaonesha wazi namna ya Baraza letu lilivyokua. Mimi naamini kuwa huu sio mwanzo wa hili huu utakuwa ni mwanzo lakini ni muendelezo vile vile wa mambo kama haya ambayo yatakuwa yanatolewa na kamati mbali mbali zilizopo katika Baraza hili.

Mhe. Spika, mimi vile vile napenda sana kumpongeza ndugu yangu Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Omar Ali Shehe, kwa kweli ameonesha uwezo wake mkubwa wa kuiongoza hii kamati na kuweza kutoa ubadhirifu, udangajifu ambao unafanywa na watendaji wa shirika hili.

Mhe. Spika, mimi sina haja ya kurudia yale ambayo yameshasemwa na wengi, mengi yamesemwa lakini Mhe. Spika, nikwambie kuwa, kwa kweli imeumiza sana kwa sababu ripoti

hii imefichua udhaifu sio wa shirika hili, lakini udhaifu wa utendaji katika mashirika pamoja na maidara yetu ya serikali mengi sana.

Mhe. Spika, hapa hakuna kubwa la kujadili ripoti imeshatoka, yaliyokuwemo ndani yanaeleweka yameelezwa wazi na kwa bayana kabisa hata mtu wa kawaida tu anaweza kuyafahamu kwamba hapa wizi mkubwa unafanyika hayataki tochi, sio mambo ambayo unasema kwamba uingie kwenye *dictionary* la *oxford* ukayatizame haya hayataki tochi yamejieleza na vielelezo vyake tumepewa. Sasa mimi naiomba sana serikali tena naiomba kwamba hii ripoti isimalizikie hapa ripoti hii ishughulikiwe.

Kwa bahati nzuri vielelezo vyote vipo, vithibitisho vyote vipo, sasa wanaohusika kwenda mbele Mhe. Spika, lazima wachukuliwe hatua. Taratibu zifuatwe lakini hatua zichukuliwe. Kila mmoja hapa kasema lake kuna wengine wamesema walipe haya madeni na kuna wengine wamesema wafikishwe katika vyombo vya sheria, lakini mimi nasema hivi kwa sababu tunataka tuwape haki hawa waliotajwa na wengine uchunguzi lazima ufanywe. Ufanyike uchunguzi wa kina na wale wote ambao wanahusika wachukuliwe hatua tena hatua kali, kama ikiwa haikuchukuliwa hatua ripoti hii Mhe. Spika, itakuwa kila siku tunalea, Wazanzibari wamechoka kulea wahalifu, hawa ni wahalifu Mhe. Spika, tena wahalifu wanatuzidishia umasikini, nchi yetu ni masikini.

Mhe. Spika, mtu mmoja anachukua mamilioni ya pesa anatia kwenye mfuko wake wakati skuli hatuna madawati watoto wetu wanakaa chini, mtu mmoja akichukua shilingi milioni kumi tu dawati moja linauzwa shilingi laki sita ambalo linakaa watoto watatu. Je, tayari tumeshawapa vikalio watoto wangapi, mtu mmoja huyo huyo anachukua shilingi 20 milioni anazitia kwenye mfuko. Mhe. Spika, tatizo hili liko muda mrefu, watu wanatizama maslahi yao wachache wameaminiwa, wamepewa majukumu wafanye lakini wanaona serikali ni wajinga kiasi kwamba wao wanajali maslahi yao kwa nini na kwa nini tuwanyamazie Mhe. Spika, haiwezekani wachukuliwe hatua.

Mimi nasema kwa moyo wangu wote kama walivyotangulia wenzangu kusema tusikubali jamani. Dada yangu Mhe. Asha Bakari amesema hapa kwamba, kuna watu wanakwenda pahala wanafanya kazi kipindi kidogo wanamiliki mali unashangaa na unajiuliza kazipata wapi huyu, lakini tunajua anafanya kazi wapi, ukiuliza yule anafanya kazi sehemu fulani ndio maana ana pesa vile, tunaoneshwa hii nyumba ya fulani jamani tutaendelea na mambo hayo mpaka lini.

Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha, jamii yetu inakuwa masikini watu wanakwenda skuli sasa hivi wanachukua mafunzo makubwa makubwa kwa ajili ya kwenda kuwaibia wananchi ndivyo hivyo? Sasa hivi ndio maana tunakosa wataalamu katika maeneo fulani. Kwa sababu kuna maeneo maalum ambayo watu wanataka kwenda kwa sababu wanapata urahisi wa kuiba.

Mhe. Spika, hapa tumepitisha sheria ya Rushwa tumezungumza suala la kutoa vielelezo kwa viongozi wa juu kuhusiana na mali zao walizonazo. Mhe. Spika isiishie hapo, kuna watendaji wa chini ambao nao pia kwa mara moja wakifika katika nafasi fulani wanatajirika kwa haraka. Sheria ile isifike kwa viongozi wa juu tu, sheria ile ifanye kazi kwa wafanyakazi wote ambao watapewa majukumu ambayo yatawawezesha kupata pato la haraka.

Mhe. Spika, mimi naungana na wenzangu waliotangulia wengi ambao wamelikemea suala hili na vile vile nakubaliana kabisa na mapendekezo ambayo yametolea na kamati hii. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Rais wetu hili suala aliangalie sana kwa makini waliohusika wachukuliwe hatua. Humu aliyekuwemo hatoki na aliyekuwa hayumo haingii, kama mtu hana kosa mimi naamini haki yake atapewa na yule ambaye ana makosa Mhe. Spika, hatua kali ichukuliwe.

Baada ya kusema hayo machache nakushukuru tena Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia naunga mkono mapendekezo ambayo yametolewa na kamati. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia jioni hii pamoja na wenzangu tuliomo ndani ya Baraza lako tukufu kuwa katika hali ya uzima na afya.

Pili, niipongeze Kamati Teule iliyoteuliwa na kuidhinishwa na Baraza lako tukufu hili kwenda kufanya uchunguzi katika Shirika la Umeme (ZECO*)*. Nataka kwa makusudi nichukue fursa hii kuwapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya bila ya kujali itikadi ya aina yoyote, wana Kamati ya PAC nawapongezeni sana, hongereni sana kwa kazi nzuri.

Mhe. Spika, chombo hiki tunachozungumza ni chombo cha wananchi na wananchi wanatuangalia tunafanya kitu gani, wananchi ndio waliotuleta hapa na kazi yetu kubwa ni kuwatetea wananchi hao pamoja na nchi yetu kwa ujumla. Lakini ukiangalia katika Shirika hili la Umeme basi ubinafsi umejaa na hawafanyi kazi kwa pamoja, hata ukizingatia juzi tumeadhimisha miaka 48 ya Mapinduzi Matukufu ya Mwaka 1964 kufuatia hotuba za viongozi wetu Mheshimiwa aliyekuwa Rais wa Kwanza Mhe. Abeid Amani Karume anasema, “kama una ubinafsi sehemu hiyo haiwezi kufikiwa na maendeleo hata siku moja”. Kwa hivyo, tuzingatie sana kauli za viongozi wetu hizo ni za hekma na tuzifuate kuondoa matatizo.

Mhe. Spika, kuna ubaguzi wa kutosha katika Shirika la Umeme na ubaguzi huu si ubaguzi wa Upemba na Uunguja, ubaguzi huu si wa vyama vya kisiasa CUF na CCM bali ubaguzi huo ni wa wafanyakazi na kama hamfanyi kazi kwa pamoja hamuwezi kufikia hatua hata kidogo. Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano katika hotuba yake moja anasema, “huwezi kufanya kazi waziri ikawa naibu waziri hajui”, hapo patakuwa pana matatizo makubwa. Sasa huwezi kufanya kazi kama Meneja wa Shirika ikawa wa chini yako hawajui ni matatizo itakuwa sehemu hii haina ushirikiano wa kutosha.

Sasa Mhe. Spika, imeelezwa hapa tumesema kuna ubaguzi, hata ukiangalia katika utaratibu wa kazi imeainishwa ndani ya kamati teule hii katika ukurasa wa sita nambari moja pale inasema, kuna nafasi za masomo Pemba zinatolewa kwa upendeleo. Sasa jiulize, kama nafasi hizo ukizitoa kwa upendeleo unachokifanya ni kitu gani, ni kuwa unampendelea akuunge mkono hawezi hata kukukemea unapoharibu. Kwa hivyo, Mheshimiwa hili liangaliwe sana.

Shirika hili imani yangu inanipa linajiendesha kwa hasara halijiendeshi kwa kupata faida na ukitaka kujua hilo kitabu hiki kimeainisha kabisa kwamba kuna ukiukaji wa makusanyo, watu wanakwenda wanatoa pesa hawapewi risiti inavyostahili zinatolewa risiti kwa maslahi ya mtu. Kwa hivyo, shirika hili haliwezi kufikia maendeleo hata siku moja na kuweza kufanya kazi kwa ufanisi kabisa.

Mhe. Spika, kwa sababu Baraza lako limeridhia na kuunda kamati na imefanya kazi kubwa ndani ya Wajumbe tisa na Makatibu wawili na kwa muda mrefu basi mimi naunga mkono moja kwa moja yaliyogunduliwa na aliyestahiki kuwa ameingia katika matatizo hayo basi achukuliwe hatua za kisheria na wale wanaochukuliwa hatua za kinidhamu wachukuliwe, lakini tufikie mahali tujue tunafanya nini kwa wananchi wetu. Wananchi wana shida ya umeme, kila mtu anataka apate huduma hiyo muhimu, lakini kwa umasikini uliokithiri hawezi kufikia malengo. Kuna watu wachache wanajaza mifuko yao kwa kujinufaisha wao na watoto wao, hii itakuwa haipendezi hata kidogo, tutakuwa tunazungumza ndani ya Baraza lako halafu ni kutwanga maji katika kinu inakuwa hayakai ni tatizo.

Mhe. Spika, kwa kweli wenzetu wamezungumza mengi ya kutosha, lakini mimi nataka niseme tu kidogo. Iwapo mtu yeyote amegundulikana kafanya ubadhirifu huu basi hatua zichukuliwe kwa mfano kama Hakimu anapomhukumu mtu akamtia hatiani anamwambia nakupa adhabu hii iwe fundisho kwa watu wengine. Kwa hivyo na hapa ieleweke kila aliyefanya ubadhirifu achukuliwe hatua za kisheria na iwe fundisho kwa mashirika mengine na taasisi nyengine. Kama tutakwenda hivyo kwa kila mfanyakazi alipo ataogopa. Nina imani kuwa atafanya kazi kwa uadilifu wa kutosha na kama tutayazembea haya watu wataendelea kujirundikia pesa za wananchi siku hadi siku.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia hayo naomba nisiende mbali na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Wale wote waliogundulikana na ubadhirifu huu wachukuliwe hatua za kisheria. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi leo kuchangia kidogo tu machache kwa vile ripoti hii watu wengi tayari wameshaichangia. Vile vile mhe. Spika, niseme kwamba ripoti hii ukiangalia hasa hamna kilichokuwa hakijachangiwa na Mwenyekiti hamna alichokibakisha.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii ya PAC kwa kazi yake nzuri aliyoifanya na kuja kuiwasilisha katika Baraza hili tukufu. Lakini pia Mhe. Spika, niwapongeze Wajumbe wake ambao walishirikiana naye pamoja kufanya kazi hii na kuileta hapa Barazani ambapo ilikuwa hawalali mchana na usiku, hawachoki ili kufanyia kazi kile walichotumwa.

Mhe. Spika, mimi nije katika mahoteli. Mhe. Spika, inaonesha wazi kuwa shirika lilikuwa halina ushahidi wa mafaili ya ufungaji wa umeme mahotelini, jambo ambalo lilikuwa ni hatari sana na jambo ambalo liliikosesha mapato serikali katika nchi yetu hii.

Vile vile nije katika sehemu ya ajira. Mhe. Spika, katika ajira shirika linaonesha kuajiri watu ambao hawana sifa kama inavyosema hotuba hii Mhe. Spika, wanaajiri watu wao wanaopenda wao wenyewe jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa serikali yetu. Mhe. Spika, naomba watu hawa wachukuliwe hatua kali za kisheria ili kuwa ni fundisho na mashirika mengine.

Mhe. Spika, vile vile niseme kwamba serikali ichukue hatua kali na kila aliyehusika na hujuma kama hii kwa sababu ukiangalia hasa kwenye ajira watoto wetu sasa hivi wako vibarazani ambao wamesoma na ambao wana elimu zaidi na madiploma. Lakini ukiangalia vijana hao jambo

kubwa ni kuvunja majumba ya watu na kuiba kitu ambacho si kizuri na shirika ambapo linachukua watu ambao hawana hata elimu na kuwatia katika shirika lile kufanya kazi.

Mwisho Mhe. Spika, niseme kwamba tunaunda kamati hapa ili kuchunguza mambo yanayofanywa katika mashirika. Lakini ukiangalia sisi Wajumbe tunapiga kelele sana na ukiangalia Mhe. Spika, serikali haina hata moja inalolifanya ikaonesha mfano kwa watu wengine, na watu wetu tukikaa hapa nje wanasikiliza sana Baraza, lakini siku hizi wameingiwa na uchungu wanasema hakuna chochote kinachokuwa. Kwa sababu kama ni kweli serikali inaunda kamati kuchunguza mambo yanayofanyika katika mashirika lakini leo Mhe. Spika, hakuna hata mtu mmoja anayechukuliwa hatua jamani jambo hili linaudhi sana, Mhe. Spika, linatuumiza sana. Leo kamati tunatumwa tukachunguze, tukaangalie hatimaye tukija nayo hapa serikali haina kinachotenda. Naomba jambo hili serikali ilizingatie sana.

La mwisho Mhe. Spika, naiomba serikali uchunguzi huu usifanywe katika Shirika la Umeme tu, bali yapo na mashirika mengine nayo vile vile yafanyiwe uchunguzi kama huu ili kuhakikisha kwamba hamna mabaya katika mashirika yanayofanyika na kukomesha wale manyangumi ambao wanameza fedha za wavuja jasho na kuhujumu uchumi wa nchi yetu hii.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba nikae kitako nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu ili kwa jinsi ambavyo ametujaalia waja wake kuamka salama tukiwa wazima na leo tangu asubuhi tumekuwa tukijadili hoja hii muhimu ya kamati na bila shaka ni kwa manufaa ya Wazanzibari wote sio kwa manufaa ya Wajumbe hawa tu, lakini ni kwa manufaa ya Wazanzibari wote Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, pia nikupongeze wewe na nikushukuru sana kwa busara zako na umakini wako jinsi unavyoendesha Baraza hili na kufanyia haki inayostahiki Wajumbe wako wote. Na mimi nimekuwa nikisema wazi kwamba, sioni tabu kusema kuwa Zanzibar tunajitahidi kutafuta mrithi wako kwa muda mrefu mana simuoni. Nafasi hiyo uliyonayo ni nafasi ambayo inahitaji busara, umakini na akili ya hali ya juu.

Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa watu waliokuwa Wajumbe wa Kamati hii ambapo nilifanya kazi na wenzangu kwa moyo wote na kwa nia ya kuwasaidia Wazanzibari. Sasa kwanza kabisa niunge mkono hoja ya kamati hii na niseme kwamba, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani niunge mkono kwa asilimia mia moja hoja hii na niwaombe wenzangu wote ambao wanawapenda wananchi wao majimboni waunge mkono hoja hii. Kwa sababu ni hoja ambayo itatusaidia na hatimae nchi yetu itakuwa katika manufaa mazuri sana.

Mhe. Spika, kwa hakika tumechunguza na tulikuwa na hali ngumu ya kuchunguza kwa sababu muda hautoshi na tulikuwa na hali ngumu kwa sababu sisi si wataalamu, lakini yale ambayo yasingehitaji utaalamu wa hali ya juu ndio tumeyaona. Kwanza kabisa mimi Mhe. Spika, niungane mkono na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa ule udhaifu ambao wametuonesha kwamba hatukuweza kufika Ubalozi wa Norway. Naunga mkono kwamba ulikuwa ni wajibu wetu kufika lakini kuna sababu ikiwemo sababu ya nyezo ambapo ofisi yako ilishindwa kutuwezesha. Mbali ya hilo, tulikuwa na haki pia ya kwenda Afrika ya Kusini. Kamati hii iliambiwa kwamba nguzo

na mita zinanunuliwa kwa jila la mtu, tulikuwa tuna haki ya kwenda Afrika ya Kusini kuona jinsi gani mtu huyu anavyonunua nguzo na mita za TUKUZA kama ni mfanyakazi binafsi wa shirika. Pia kutokana na nyezo na muda mfupi hatukuweza kwenda huko.

Lakini Mhe. Spika, pia tulikuwa na haki ya kwenda kuikagua *data base* ya shirika ya wateja ambapo kamati hii iliambiwa ilifutwa kwa makusudi na mfanyakazi binafsi ili kukwepa ile aibu ya fedha ambazo zimepotea. Na mimi kama miongoni mwa wanakamati nataka nianzie hapo, kwamba miongoni mwa mapotevu makubwa ya fedha ni kwamba ZECO ilifuta *data base* ya wateja hasa Mji Mkongwe katika utaratibu wa *aquarium* kuingia TUKUZA na wakapoteza zaidi ya milioni mia saba ndani ya shirika. Zipo *data* lakini tulihitaji kupata mtaalamu wa IT kwenda kukagua bahati mbaya Baraza halina.
Kwa mafunzo hayo Mhe. Spika, nadhani tujipange kila idara ijitosheleze tuwe na *engineer* na wataalamu wengine ili kila hoja tuweze kufuatilia wenyewe. Kwa hivyo hoja ya mwanzo Mhe. Spika, ya upotevu wa fedha ni kwamba ZECO kupoitia mfanyakazi mmoja ambaye anaitwa Abdalla Sten kama tulivyoambiwa aliweza kufuta *data base* ya shirika ambayo ina wateja zaidi ya 700 na fedha za shirika zaidi ya shilingi bilioni moja ambazo zilikuwa ni mali ya Shirika la Umeme. Hiyo ni hoja ya kwanza.

Mhe. Spika, hoja ya pili ni kwamba kweli kulikuwa na fedha zinapotea katika uungaji. Kwa mfano, Pemba kule tuliangalia hoteli ya Pemba Mesali, Wesha; tukaangalia Benki ya NMB, Chake Chake, tukaangalia hoteli ya kaka yangu Said Mbuzi kule Wambaa, zote hizo ziliingiziwa mahesabu yake zaidi ya shilingi 20 milioni, lakini ZECO hawakufika shilingi milioni saba. Sasa hivi utachambua, kwenye vitabu hivi tumeweka waziwazi kwamba makisio ya wenyewe ZECO yalisema, Amani Ibrahim Makungu alipeleka 37 na bahati nzuri akatoa ZECO zikaingia shilingi milioni mbili na hamsini na mbili elfu, Benki ya NMB shilingi 19 milioni zimeingia shilingi milioni tatu na Hoteli ya Baobao kule Wambaa shilingi 34 milioni zikaingia shilingi milioni tatu. Ni dhahiri kwamba fedha ile wateja wale walilipa lakini ziliingia kwenye mifuko ya watu wachache kwa maslahi yao na sio kwa maslahi ya Wazanzibari wote.

Mhe. Spika, jengine ambalo naomba nilifafanue tuliomba kupatiwa mafaili ya minara yote ya Unguja na Pemba ya Makampuni ya Simu ya Zantel, Tigo na wengineo. Pemba ripoti imeeleza kwamba, kati ya mafaili 46 kamati yangu nadhani ilipata mafaili 3. Unguja bahati mbaya tuliambiwa mvua ilinyesha na yakaroa hatukuyapata.

Kwa hivyo ofisi iliyo makini yenye wataalamu waliosemea makini wameridhika kwamba jibu la ofisi imeroa ndio ndio jibu toshelezi. Lakini baada ya kufanya utafiti hakuna mnara ambao si chini ya shilingi milioni tatu gharama yake ya kuunga umeme. Sasa ikiwa minara hii ni 200, piga hesabu milioni tatu mara mia mbili kiasi gani ZECO wanapoteza pesa za wananchi kwa uzembe na kwa makusudi.

Mhe. Spika, nataka uamini kwamba si kwamba hakuna faili, lakini kamati ilikuwa inachezewa mchezo. Lakini pamoja na kwamba kamati hii haina wataalamu lakini bahati nzuri hamna kiziwi na wala hamna kipofu, sote tulikuwa makini na kwa njia moja au nyengine ushahidi tuliopata ni kwamba waliyaficha mafaili makusudi ili tusiweze kupata ushahidi.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka niseme ni upendeleo wa ajira. Naomba nisisitize kuwa ZECO na naomba wajumbe wenzangu kuwa wawe makini, kuwa ZECO hakuna upendeleo wa Unguja na Pemba, kwa ZECO hakuna upendeleo wa CCM na CUF, ila kwa ZECO kuna upendeleo wa ndugu na damu na familia yangu. *(Makofi).*

Kwa hivyo wale Wazanzibari ambao wanaofikiria kwamba ZECO ina ubaguzi wa Unguja na Pemba si kweli. Wapemba walipendelewa, Waunguja walipendelewa lakini lazima uwe damu ibinikinana na ibini mwengine. Kwa hivyo kwa ZECO na upendeleo wa chama hakuna wala Upemba na Unguja hakuna.

Kwa mfano, kamati hii ipo pale Meneja wa Fedha wa ZECO kabla ya kwenda sisi kamati alikuwa ni mama, ni shangazi mtu. Mhasibu Mkuu ZECO Unguja ni mtoto mtu. Mhasibu Mkuu Pemba ZECO ni mke mtu. Kwa hivyo ni familia moja ndio iliyokamata Idara ya Fedha. *(Makofi).*

Ni familia moja kuanzia meneja wa fedha, Mhasibu Mkuu Unguja, Mhasibu Pemba, huo ndio utaratibu wa ZECO. Baya zaidi Mhasibu huyu wa Pemba Mhe. Spika, walitangaza nafasi za ajira hawa vijana wetu wakaomba hatimaye akachukuliwa mshindi wa tatu mwenye maksi 48 akaachwa mwenye wa kwanza na wa pili.

Kwa hivyo nilikuwa na hayo ya kusema hayo ni upendeleo. Na bahati mbaya faili moja la mtu huyo kamati ikagundua mpaka matokeo ya mtihani au *interview*, ana maksi 48 mshindi wa tatu, elimu yake ni ndogo kuliko wengine, kwa nini Mzanzibari kama mimi nisiseme ni upendeleo. Aliajiriwa kwa sababu shangazi ni meneja wa fedha, bwana mkubwa ni mhasibu mkuu Unguja na mimi mke niende Pemba nikakamate fedha. Ni tatizo Mhe. Spika.

Kwa hivyo mimi leo nikiwa ni mwakilishi na mke wangu awe mbunge na mwanangu mmoja awe mkuu wa mkoa na mwanangu mwengine awe ni sheha ni tatizo Mhe. Spika. Si malengo ya serikali kufanya hivyo. Hatimaye Mhe. Spika, tumekwenda Pemba ripoti imeeleza, kila siku mhasibu anakusanya milioni mbili kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Kwenye akaunti 173, Pemba wana akaunti tatu. Wana akaunti 162, akaunti 163 na 173, hii ndio bomba 173 inaingiza kila siku ya Mungu milioni mbili kwenye akaunti. Maana yake nini. Maana yake kila mwezi ni milioni 60 na kila mwaka ni milioni 720.

Mhe. Spika, hivi leo ninavyozungumza hapa Ngomeni jimboni kwa Mhe. Abdalla Juma, tangu mwaka 1964 mapinduzi ni kilomita 6 kutoka Kuyuni hawana umeme, hawana barabara, hawana maji, hawana hospitali.

Kiyuni mpaka Ngomeni si zaidi ya nguzo 30 wameshindwa kupeleka nguzo. Kama ni shirika la umma, unakusanya milioni mia saba kwa mwaka matumizi ya kawaida, matumizi madogo madogo, mafuta, vinywaji, simu ni milioni saba na ishirini.

Unashindwa kuwafikia umeme Ngomeni ambayo inaongoza kwa karafuu Unguja na Pemba kwa miaka 49 ya mapinduzi ya Zanzibar. Hoja ilikuwa si kuwa hatuna uwezo, hoja ni kwa sababu watu shirika ni mali yao. (Makofi).

Mhe. Spika, na mimi nataka niseme kwamba serikali imekula hasara sana. Mashirika haya madhumuni yake ni kusaidia umma na kuchangia serikali kuu. Mhe. Spika, mpaka Pemba kamati inamaliza hakuna mkaguzi wa ndani. Taarifa nilizonazo sahihi aliajiriwa tarehe 1/10/2012 baada ya kamati yako kupita.

Naomba Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri kuwa alitwambia kuwa mkaguzi wa ndani yupo, ameajiriwa baada ya kamati kupita tarehe 1 Oktoba, 2012. Tuambieni ni miaka yote mkaguzi wa ndani alikuwa yupo wapi.

Mhasibu mwenyewe wa Pemba anatwambia niombeeni nihamishwe mimi kazi hapa siiwezi pagumu hapa. Na haya yapo Mhe. Spika, lakini *Hansard* ya *record* tunayo, ifunguliwe asikilizwe, anaomba 'pahali pagumu nihamishwe naelekezwa sivyo".

Sasa kama mhasibu mwenyewe anasema nihamisheni nitafungwa. Hapa wanakusanya pesa bila ya utaratibu, taaluma yangu haitaki hivyo nihamisheni. Sasa Mhe. Spika, mimi nasema akiwa mwenyewe aliopewa dhamana ya fedha anaomba ahamishwe kwa udhia kubwa, seuze mimi nnayekaa Muambe sioni faida ya ZECO.

Mhe. Spika, tumegundua safari za ZECO kwa sababu mambo yanafanywa ndivyo sivyo. Aliyepewa safari mtu mwengine, marejesho mtu mwengine. Tumegundua marejesho ya safari moja tukapewa kumbukumbu za daktari Mohamed Ali Jape ni mtu wa Jimbo langu la Kiwani, si mfanyakazi wa ZECO, ndio risiti yake imeekwa kama marejesho ya safari ya Unguja ya ZECO, vyereje daktari na ZECO.

Sisi Mhe. Spika, tuna macho si vipofu. Kwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa nina haki, wawakilishi walikuwa na haki, serikali ilikuwa na haki ya kutetea ZECO ili maslahi ya Zanzibar yapatikane.

Mhe. Spika, hoja ya majenereta. Si tu kwamba serikali haikuzingatia umakini. Serikali walikuwa na hoja ya kununua majenereta kwa sababu kulikuwa na giza. Hoja ya kamati na humu ndivyo ilivyoandikwa, taratibu za manunuzi zilifuatwa. Hivyo hatuwezi kwa uharaka tukaamua tenda bodi asubuhi, jioni tukafanya hili, saa sita ya usiku tukafanya hili, alfajiri tukafanya hili, hatimaye siku moja tukamaliza yote lakini kwa utaratibu.

Mimi leo ukiniambia hapa saa nane kikao, saa kumi kikao mote nitakwenda, si kwa maslahi. Walishindwaje ZECO kufanya utaratibu wa kisheria haraka hata siku, halafu tunaambiwa kuna fundi akafanyakazi hatimaye akaangusha kitu kizito baadae pakapasuka ikaingia hewa ya oxygen na maji ikafanya kutu pakaripuka. Twambie huyo fundi aliyekwenda, hamjui. Lakini kwa utafiti wangu Mhe. Spika, aliyefanya matengenezo hayo ya kibanda anaitwa Khalfan na ndiye aliyefanya matengenezo hayo na kama nia ilikuwa nzuri basi hapa ndio hapa pa kuanzia.

Lakini taarifa ambazo tunazo Mhe.Spika, ZECO walikuwa na bilioni moja na nusu. Sasa ili itumie mwaka wa fedha unaokuja tayari ikatumiwa. Kamati inaomba matumizi ya fedha hizo hakuna. Mhe. Spika, kama taasisi kubwa kama ile haina utaratibu wa kuweka kumbukumbu zake serikali imekula hasara.

Mimi nasema kwa nia safi kabisa hatukuchunguza kwa kumtafuta mtu lakini uchungu wa mali ya serikali inapotea kwa wachache. Mhe. Spika, tuligusa barua moja ya PRISMO. PRISMO anawasifu GECO kwamba GECO ni kampuni madhubuti kuliko ZECO. Tukajiuliza akaa! hapa Zanzibar pana kampuni mbili. Kampuni ni halali hapa Zanzibar ni ZECO lakini PRISMO anasema kazi zenu GECO nzuri, muda mfupi na gharama kubwa lakini ni *fitness*.

Kwa maana makampuni ya nje wanamsifu zaidi GECO kuliko ZECO, kwa nini kwa sababu ni *shareholders* ni wafanyakazi wa ZECO. Na barua ya bodi ilitoka kwamba chagueni moja, chagueni kubakia GECO au mbakie ZECO, hadi hii leo watu wapo GECO, wapo ZECO. Nidhamu hakuna hata kidogo.

Mhe. Spika, *store* ambayo inaingizwa vifaa vya GECO Pemba, ni *store* ya ZECO. Mtu ambaye anayedhibiti vifaa Pemba ni Habibu ambaye ni mtu wa ZECO. GECO wananunua ZECO anapokea wanahifadhi, wapi na wapi utaratibu huo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hili lilikuwa ni shamba la bibi, hivyo tuamue kurithi au tuamue kuliacha life. Mhe. Spika, kwa hakika mimi niseme tu kwamba mwanasiasa yeyote anajua kwamba ukiamua kuingia kwenye siasa ukubali matusi, vitisho, vya kufungwa hata kifo.

Jana Mhe. Spika, usiku kwa masikitiko makubwa mimi mwenyewe na Mhe. Omar Ali Shehe kuna watu walitutumia *message* mbaya sana na mmoja alipiga simu mwenyewe akajitambulisha mimi ni mtu fulani wa ZECO na nilimjua.

Mhe. Spika, kwa hisani yako naomba *message* hii niiosome ili uone picha kwamba mafisadi hawataki wakosolewe na hii ndio sifa ya fisadi. Fisadi siku zote hujifanya yeye bwana.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu niisome *message* jana ambayo nimetumiwa mimi na Omar Ali Shehe na baadae yeye akaongezewa maana yeye ndiye mwenyekiti; mimi nilitumiwa moja, yeye ametumiwa mbili.

Mhe. Spika, *message* inasema naomba kuinukuu, “Tunakuhakikishia wewe Hija na Omar na kundi lenu, maana yake kundi letu sisi ni Kamati ya PAC ndio kundi letu, ujuwaji na jeuri yenu itawatokeeni puani endeleeni”.

Mhe. Spika, naapa kiapo hapa hapa nipo tayari nife lakini ushahidi ni Wazanzibari. Hata sitomridhia siku moja fisadi. Kama ni kufa si tatizo lakini nnavyotaka mimi nife lakini na ZECO idumu, ili mwanangu na mjuu wangu aje afaidike. Mimi sitishwi kwa hivyo kwamba wewe utuibie kwa sababu rangi yako ni nyekundu au nyeupe, halafu ufanye jeuri sivyo.

Lazima tuseme na tumesema na tutasema na mwakilishi aliyekuwa makini anafanya utafanya utafiti kila shirika. Nilisema juzi pale naomba niwahakikishie wenzangu sote tuelekee ZRB, TRA na kwengine.

Ni haki yetu na wajibu wetu kuwatetea Wazanzibari. Mhe. Spika, sasa mimi ukinitisha na Omar Ali Shehe ukimtisha na Waziri wa Fedha, sasa hiyo ni nchi au ni genge. Maana yake mtu aaibe tumuabudie.

Mhe. Spika, baada ya Mungu aliyeniumba Mungu mwengine simuoni. Nitamwita Mungu yule aliyeniumba mwengine simuoni. Kwa hivyo wale mafisadi ambao wanatutisha sisi, sisi tutaendelea kuendelea kuwatetea watu na nina imani Wazanzibari kwa hili watatuunga mkono. (Makofi).

Mhe. Spika, hii sisi hatukumtisha mtu na mimi nimshukuru sana Meneja Mkuu, kila ambapo kamati inakwenda alikuwa yeye yupo mbele, kwa hili nimpongeze sana. Mengine alikuwa mwenyewe anayashuhudia na kwa hakika mengine hakuyafanya yeye. Lakini yeye ndio *accounting officer*. Mengine hakuyafanya yeye wenzake wamemgeuka.

Sasa Mhe. Spika, kwa hakika mimi niseme kwamba kazi iliyofanywa na serikali na kamati yetu ni nzuri na nia yetu ni nzuri sana, lengo ni kuwasaidia Wazanzibari wapate fursa. Na nimalizie kwa kuwakumbusha Wazanzibari siku moja tarehe 5 hadi 9 mwezi wa Julai 2012, hapa Zanzibar huduma ya umeme ilipanda ghafla. Baada ya kupata unit 40 unapata unit 22 hadi 30.

Baada ya utafiti ZECO walipandisha ghafla. Sasa hoja jee, ilikaa uongozi, jee lilikaa Baraza la Mapinduzi watwambie ukweli. Ninavyojua mimi Baraza la Mapinduzi hawajaidhinisha kupandisha umeme lakini ilipanda ghafla na waziri akaahidi hapa kwamba atarekebisha bila ya maelezo.

Mhe. Spika, mimi ninayo barua ambayo meneja mkuu alimuagiza mtendaji wake kwamba apandishe umeme. Sasa hoja kwa wananchi mutwambie jee ilikuwa ni maamuzi ya *management*, ilikuwa ni maamuzi ya bodi, ilikuwa ni maamuzi ya Baraza la Mapinduzi. Hadi leo kimya. Kwa hivyo Mhe. Spika, kamati yangu na wawakilishi wangu wote tumechunguza kwa nia safi kuwasaidia Wazanzibari wenzetu.

Mhe. Spika, mwisho hata mishahara watu wanapendeleana. Nina orodha hapa ya watu 24, ZECO ina wafanyakazi mia saba naa. Lakini mshahara umepandishwa kwa wafanyakazi 24 tu, kwa nini? Hawa ni VIP, hawa ni ma-*engineers*, hawa ni watoto wa nani, ninao kwa majina na *figure* zao.

Ndio maana kumbe kamati iliambiwa na *hansard* ipo kwamba watu wanapigana ofisini kwa meneja, kuna watu walipigana ngumi mtu, tukenda tukawauliza kwa nini munapigana, aah! Hayasemeki bwana. Watu wanapigana ndani ya ofisi na bahati mbaya wote hao ni akinamama, kwa nini ni kwa haya maslahi yanapandishwa kwa mmoja na mwengine hapati.

Mhe. Spika, mimi nasema ikiwa ZECO ina wafanyakazi mia saba na bodi imeamua kupandisha mshahara, wote wapandishiwe wapate haki yao ni wafanyakazi halali. Kitendo cha kuwapandishia wafanyakazi 24 mshahara si sahihi, si haki, si utaratibu.

Mhe. Spika, leo ZECO inakusanya mapato ya bilioni tatu nukta saba kwa mwezi. Deni wanapata ni milioni tatu nukta mbili, wakilipa deni TANESCO, maana yake wanabakia na *zero point five billion*, ukiwalipa wafanyakazi mia saba, maana yake ni zero. Kwa hivyo ni shirika la kuganga njaa tu. Maana yake deni ni *three point two billion*, makusanyo ni *three point seven billion*, haya lipa hizi zote kwa mwezi, inabakia milioni tano, kuwalipa wafanyakazi mia saba na ZECO

mfanyakazi wa chini si chini ya shilingi tano, wamo humu wana wafanyakazi wana mishahara mikubwa. Kuna mtu hapa ana FTC ana milioni moja ni shirika hili kubwa.
Sasa lipa wafanyakazi, lipa nyengine, maana yake shirika hili ni zee Mhe. Spika, lakini nilitegemea mimi asamehe mteja wa kawaida mnyonge, lakini waliosamehewa na ZECO ni wale watu wenye pesa, watu maarufu na watu wenye uwezo. Hadi leo Mhe. Spika, matumizi ya KVA Pemba hayatumiki. Maana yale ni matumizi ya wateja wakubwa. Pemba mteja mkubwa aliyeopo ni ZANTEL na ZANTEL huyo ZECO wamemsamehe wamemwambia bwana madhali wewe upo peke yako bora tukusamehe kidogo. Haya asamehewe kwa nini.

Sasa Mhe. Spika, kama Wazanzibari bado wanahitaji ZECO, mimi naomba tufanye marekebisho ya nguvu kwa nia safi tuwapate watendaji wenye nia na huruna na uchungu ili ZECO iweze kuendelea, laa tumeamua kuyakasimu madaraka kuwapa GECO na tuamue. Ni wajibu wetu na ni jukumu letu.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi).*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: *Bismillah Rahman Rahim*. Mhe. Spika, nimeanza kutaja kwa jina la Mwenyezi Mungu, ina maana kwa sababu sisi wengine kidogo tumepitia vyuoni.

Kwanza nikushukuru wewe kunikubalie jioni ya leo kuweza kunipa kuchangia Kamati hii ya PAC. Kwanza nimshukuru Mhe. Mwenyekiti ni jemadari, *good experience*, mtaalamu mzuri sana. Ametuletea mambo ambayo tunatakiwa wajumbe tuyachangie yale yaliyokuwa ni ya ukweli na ndio maana nikasema tuwe wawazi na ukweli na mimi nitakuwa ni mkweli.

Mhe. Spika, kwanza nirudi nyuma historia kidogo kwenye shirika hili. Shirika kama sijakosea kwa fahamu zangu za juzi juzi tu kuingia katika utawala huu tutakuwa na mameneja watatu. Hilo ndugu wajumbe mulitambue hivyo.

Lakini uwezo wangu mimi Mhe. Spika, kwa sababu binadamu wote kila mtu ana akili yake humu ndani na hata nywele zinatofautiana. Nywele za Mazrui si zangu mimi, ni tofauti inakuwa. Sasa na akili vile vile Mhe. Spika, inakuwa tofauti, uelewa wa mtu na uonaji wa mtu.

Wenzetu wamekwenda *deep*, waliyoona wameyaona kutokana na uwezo wao, *experience* yao na kama nilivyosema ikiongozwa na Mwenyekiti mwenyewe mwenye uwezo wa hali ya juu, kwa sababu saa nyengine namshukuru sana Mhe. Omar Ali Shehe *wallahi* huandika ripoti kwenye kichwa tu tofauti na sisi wengine tunawatuma makatibu wetu, tuseme ukweli ulivyo hata hivyo namshukuru kwa sisi tunawaambia makatibu wetu watuandikie lakini yeye anatoa kwenye kichwa chake na sasa hivi ana mtindo Mhe. Spika, ana *lap-top* yake anakuwa anaweka, hilo ni moja ni uzoefu mkubwa sana, hongera sana.
Lakini Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa msingi hasa wa shirika hili bado tungali tunaficha. Mhe. Spika, tutaondoa mameneja wengi tu, tutaendelea kuwaondoa. Mhe. Spika, mimi mara nyingi sana nikisema huwa natoa ushahidi na ndio maana nikasema leo nipo katika utakatifu wa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, nakubaliana shirika linaibiwa sana, hilo sipingi. Mimi nasema ukweli ulivyo. Mhe. Spika, nina ushahidi tosha ni jambo la aina hii na inasikitisha sana. Na hasa wanaoonewa Mhe. Spika, ni wale watu wa chini kabisa ndio wanaoonewa ambao ni wananchi wetu.

Mhe. Spika, mimi nikisema ni mwakilishi na nikionesha kitambulisho wewe utanikubali. Lakini mheshimiwa nikikutapeli wewe utakubali kama kweli mimi mwakilishi haki yake kuchukua fedha kumbe si haki yake, kumbe nimekuonesha kitambulisho, nimekwambia na idara yangu ninayofanyakazi.

Mhe. Spika, wafanyakazi wa chini mheshimiwa mwenzangu katishwa, mimi siogopi kutishwa sio kwa sababu binadamu madhali pua imeelekea chini hakuna hata mmoja atakayekuwa na ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa sisi hapa. Yeye kama katishwa basi mimi waendelee kunitisha lakini ukweli tutausema.

Mhe. Spika, hivi karibuni ndani ya jimbo langu imeibiwa *transformer*. Leo mimi niambieni *transformer* ile akaitoa nani, mkulima ana uwezowa kwenda kufyatua pale juu. *Transformer* Mhe. Spika, imetolewa Upenja pale sehemu moja ukiteremka kwenye kilima watu wamakwenda kuitoa *transformer* ile na mpaka leo ipo unaoza pale kituoni Polisi Kiwengwe, ni *reference* hiyo na watu wakaangalie. Kama tunavyojua mawaziri saa nyengine wanatujibu njoo nikioneshe basi na mimi twendeni nikakuonesheni imo ndani ya gari.

Si afisa wala si nani, ni fundi tu aliyekwenda kuitoa pale. Tena ame-*timing*, anajua siku hizi tuna umeme wa ku-*beep*, basi kaona sasa hivi umeme umesha-*beep* na yeye kenda kuitoa, ni expert. Maana yake kuitoa *transformer* jamani kwa masaa si kitu cha mchezo Mhe. Spika.

Amekwenda kuitoa kwa dakika tu anavyojua mwenyewe lakini bahati mbaya na ndio maana nikasema Mhe. Spika, mimi napenda kumsifu mtu kutokana na yale mema aliyoyafanya na hata mimi na mtu anisifu kwa meme niliyoyafanya mabaya yangu aniachie mwenyewe nitakwenda nayo huko huko.

Maana yake unaambiwa saa nyengine aah! Anachukua ATM, wao na Mungu wao ndio wanaojua lakini sifanyi hiyo Mhe. Spika, sili haramu hata siku moja. Lakini katika historia yangu tunakoendelea nitakuonesha na watu wengine wanakula hayo hayo. Mimi nimesema leo sitoficha Mhe. Spika, naomba unilinde.

Mhe. Spika, nimshukuru Kamishna wa Polisi kwa kutuwekea Polisi shirikishi au Polisi jamii. Vijana katika doria yao walishtukia *movement* ile na wakenda kuwanyang'anya wale watu wamekimbia wameacha gari na wameacha *transformer*.

Lakini si hayo Mhe. Spika, kuna mama mmoja alikuja akanililia akaniambia mheshimiwa huwa tunakuoneni kule kwenye televisheni unaambiwa wewe ndio mwenyewe na nini, mimi nimeshatoa pesa ya kuunganishiwa umeme lakini mpaka leo sijaunganishiwa umeme. Naingizwa huku nikitolewa huku. Basi nikaji-*act* nikwambia nipe hiyo namba.

Sasa tazama mchezo Mhe. Spika, kumbe kuna udalali. Kuna watu wa nje special wanaofanya udalali ndani ya shirika. Huyo mtu mimi nikachukua nikaji-*act* kama ni *officer* na kwa kuwa lile shirika nalijua, nika-*act* kwenye *position* ya kitengo.

Basi Mhe. Spika, yule jamaa alitetemeka na akaniambia mheshimiwa kama kanuni inaniruhusu niwataje mimi nipo tayari leo. Lakini naona kama umefanya hivi nisiwataje ahsante Mhe. Spika, nitawalinda.

Mhe. Spika, basi jamaa kanitajia mimi kweli fedha nimepewa na nimezikabidhi kwa muhusika, lakini samahani mheshimiwa nambari yake ya simu sina. *Wallahi* Mhe. Spika, jua halikutua mama ananiambia mwanangu nakushukuru sana Mwenyezi Mungu akupe kila la kheri *inshallah* uwe Makamu wa Pili wa Rais sijui na nini, mambo mengi yule kanipa. (Makofi).

Mhe. Balozi sina haja ya kukunyang'anya ile ni dua tu. Mambo mengi sana yule mzee aliniombea dua. Sasa mimi nikajiuliza dakika ile tu. Lakini si hivyo Mhe. Spika, kuna mtu kenda kuungiwa umeme katoa pesa zake si chini ya shilingi laki sita na kuendelea mbele, hatimaye shirika limekwenda kumng'olea na yule mtu akatiwa ndani.

Mhe. Spika, mimi nikenda ambaye huyo ni kazi yangu huwa nakwenda kununua futari. Siku hiyo kama Mungu nilikwenda kununua futari nikaambiwa kama huyu mtu katiwa ndani Kituo cha Polisi Bububu. Mhe. Spika, nikenda pale kwa kweli nililia machozi na akasema kweli mimi kaja mfanyakazi, maana yake wana mchezo pale wewe kila siku utakuwa unakwenda unarudi watu kumbe wanakuona.

Wajanja wamemuona wamekwenda nje wakamwambia aah! Usijali hilo, lete fedha zako tukusaidie, akatoa fedha zake yule, hakutimia siku tatu kenda kaungiwa umeme. Hatimaye kaingia ndani yeye. Nikampigia simu meneja kuna mfanyakazi wako mmoja mbili tatu anaitwa fulani, ameunga pahali kinyume na utaratibu sasa mumekwenda kung'olea huyu maskini ilikuwaje mheshimiwa na kwa nini atiwe ndani huyu. Lakini Kiswahili chengine tunaambiwa mkamatwa na ngozi ndiye mwizi. Kwa kuwa yule maskini ya Mungu ndiye aliyekutwa na yale mambo na zile waya. Kumbe sasa Mhe. Spika, waya zile zimeibiwa sehemu nyengine.

Mhe. Spika, tuangalie mzizi, mzizi mlizamu unavyotoka mheshimiwa, tutawaweka mameneja zaidi ya 50, lakini mlizamu kama hatujaukata *nothing* tu tuseme ukweli. Huku chini ni kubaya sana. Mhe. Spika, ninaye mwengine ameshatoa milioni 1,500,000 keshang'olewa juzi mita anahangaika mpaka leo na Mhe. Waziri ukiwataka hawa kwa maandishi njoo nitakuandikia. Hichi kitu nakuambieni ukweli ulivyo, amekwishaliwa vibaya sana. Ukimuuliza anakuambia ni mfanyakazi fulani bin fulani. Tena mimi nawahusudu wanataja hasa. Mimi bwana kanikatia fulani bin fulani.

Lakini sio hao tu Mhe. Spika, pamoja na Sheha wangu mwenyewe keshaliwa milioni 3 na mpaka leo umeme hajaupata anakwenda akirudi. Sasa Mhe. Spika, ndio maana nikasema kuwa hili suala, hebu nawaombeni sana Wajumbe tuanzie kukata huku chini ndipo tutakapofika pahali pale tulipokusudia. Mimi nakubaliana nao hawa kwamba kila aliyekutwa na akamatwe na ingekuwa sheria inaniruhusu basi na mimi ningechukua zile pingu ningekwenda kuwakamata Mhe. Spika. Huo ndio ukweli na lazima tuuseme.

Mhe. Spika, kutokana na muda wako. Mhe. Spika, mambo mengine sitosema, hata sisi wenyewe Wawakilishi tuna ujanja, tunadaiwa humu ndani waheshimiwa wengine milioni 20 tunashindwa kulipa katika shirika hili hili na wajumbe wako humu humu. Tunadaiwa ukweli tuuseme ulivyo, tuseme ukweli kwani tunaficha nini, si tuko kwenye haki. Maana yake msema kweli mpenzi wa Mungu, nilianza kwa Bismillah hapa, ili inilinde kwa kusema ukweli ulivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi niishukuru sana Kamati hii ya PAC kwa kuyaona haya na hali halisi ilivyo. Lakini kuna jengine kubwa zaidi tutaliondoa utata wake, kama ikiwa serikali watakuwa wako *sharp*, basi hili suala tutaliondoa utata wake.

Mhe. Spika, sasa hivi shirika letu linaendesha biashara kama alivyosema makamu wa kamati yangu pale, linaendesha biashara kwa kusema kweli haina faida kutokana na hali ilivyo, na kwa kuwa tunawapenda wananchi wetu. Lakini Mhe. Spika, tutoe misaada mingine. Siku zote huwa nawaambieni hapa, kuna kampuni ambazo zinataka kuwekeza umeme. Mhe. Spika, mzunguko wote huu kwa sababu hakuna mwengine. Mhe. Spika, na tuweke mwengine kama tutizame kama ubadhirifu utakuweko hapa, itakuwa ni *challenge* nzuri, wataweza na wao ku-*balance* zile bei halisi ambazo tunazikimbia. Mhe. Spika, mpaka leo sijapata jibu, hizo kampuni zipo na wako *free* kabisa na wanaleta vifaa vyao bure, wewe unauziwa umeme tu. Mhe. Spika, tunangoja nini, tutapata faida nyingi hapo. Ikiwepo *challenge* hiyo Mhe. Spika, basi mimi naamini neno ubadhirifu utaondoka kabisa, hakuna dili tuseme ukweli. Sasa mimi hili ndio linalonisikitisha, maana yake utasema jambo zuri kwa serikali yako, basi mtu anakuambia dili, basi itakuwa tusiseme. Kwa sababu tunachosema tunaitaka serikali yetu iweze kukusanya mapato mazuri, ipate kodi, kusomesha watoto wetu, tupate mishahara. Kwa sababu leo mishahara Mhe. Spika, tunaona haya kusema Mhe. Spika, kwa sababu vianzio vyetu bado ni kidogo ndio maana mishahara inakuwa chini, lakini tukivileta viwanda vikubwa hapa basi na mishahara yetu itakuwa mikubwa.

Mhe. Spika, nimeshakuona hapo, kabla hujanipigia *penalty.* Mimi nawashukuru sana kamati ya PAC kwa kazi yao nzuri na mimi nawaunga mkono, kwa kila wabadhirifu wakamatwe na watiwe ndani mara moja. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Allah Subhanahu Wataalah na mimi jioni hii kuweza kunijaalia kupata uwezo wa kuja katika kikao hiki na wewe kuweza kunipatia nafasi adhimu na mimi kutoa mchango wangu katika ripoti ya Kamati hii ya PAC.

Mhe. Spika, kwa kweli sina budi na mimi kuipongeza kamati ya PAC pamoja na makatibu uliowakabidhi, kwa ufanisi walioufanya katika kazi yao hii ambayo imekamilika kwa kweli. Mapambano waliyokwenda kuyafanya yanahitaji pongezi, kwa sababu baadhi ya watu wengi wa shirika hili, wametoa maelezo yao kwa ufasaha kabisa. Mimi nahisi kwamba malengo ya wafanyakazi hawa wa shirika ni kulitaka hili shirika liendelee, lakini kuendelea huko kusiwe kama hivi sasa lilivyo, linahitaji mabadiliko makubwa.

Mhe. Spika, nadhani tokea kuanza Baraza hili, mimi nimeshuhudia kama sikosei hii ni ripoti ya tatu inayofikishwa katika Baraza lako hili na kila ripoti inayokuja kuna kasoro kubwa kwa watendaji wetu, hakuna ripoti inayowapongeza watendaji. Kwa hivyo, sura inavyojionesha ni

kwamba watendaji wetu wa mawizara, maidara, mashirika na taasisi wote wana matatizo, uaminifu wao umekuwa ni mdogo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, hii inapelekea kwamba tukitaka tusitake kuyafikia maendeleo Zanzibar, ama inahitaji muda mrefu na kufanyiwa uhakiki wa mawizara, maidara na mashirika bila ya kuwa na upendeleo wa aina yoyote. Kama serikali itaamua, kwa sababu hii ni kamati ya tatu na kamati zote hizi zinaonesha kwamba ubadhirifu serikalini umeshaota kutu. Kama serikali itaamua kusimamia na kufanya kamati nyengine za serikali ili kuondosha tatizo hili, basi tunaweza tukafikia maendeleo. Lakini kama Baraza linafanya haya na linawaona wabadhirifu wapo, lakini serikali ikaona kwamba wanaonewa, ni watoto wetu, ni sisi kwa sisi na ni shangazi kwa mjomba basi daima milele Zanzibar hatutofikia maendeleo.

Mhe. Spika, tutakuja hapa kila siku mkitusifia watu wa China, India, Japan na Marekani lakini sisi hatutofikiapo tutabakia kuwasifu watu tu Mhe. Spika. Sisi tutakalosifiwa Mhe. Spika, ni moja tu, la wizi kwamba Wazanzibari katika maidara yao, mawizara na mashirika yao kwa wizi ndio nambari moja, lakini kwa suala zima la maendeleo litakuwa abadan hatutolifikia. Waswahili walisema Mhe. Spika, "*ukiacha mwana kulia, basi utalia wewe*". Tutafikia pahali serikali ishindwe kuwalipa wafanyakazi wake, kwa sababu mtoto atalia. Tutafikia pahali serikali ishindwe kuleta maendeleo na tutafika pahali hawa wanaotuchukua kwa huu umeme waseme jamani tumechoka, watakata mawasiliano ya umeme.

Kwa hivyo, hili Mhe. Spika, sio suala la kulifanyia mchezo ni suala la kulipa na kulishika kwa meno ya magego, kinyume na hivyo tukishikia kwa meno ya mbele basi yatang'oka na hatimaye ubadhirifu utazidi kuendelea katika serikali yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika mambo haya nimenukuu kitu, huko nyuma sifahamu mambo ya ASP na TANU siyafahamu. Lakini ilipofika mwaka 1977 vyama hivyo viliungana kikawa chama kimoja ambacho hadi hii leo kipo madarakani ambacho kinaitwa CCM. Chama hiki Mhe. Spika, kilipokuja tafsiri yake inayojulikana kitaifa ni moja tu yaani Chama cha Mapinduzi, lakini wataalamu wengine na watu wengine binafsi kila mmoja alitoa tafsiri yake. Lakini kwenye serikali kulikuwa na tafsiri moja ambayo mpaka kesho na keshokutwa inatumika kwamba 'Chukua Chako Mapema'. Hii ni tafsiri ambayo ipo na ndio hali tunavyoiona kwamba hii ni kamati ya PAC, lakini ni kamati teule ya tatu. Tokea tuanze sisi Baraza hili la mwaka 2010/2015 ni la tatu, hatujakuta kamati kupongeza idara au shirika, kumbe watu wana ile ile tu kwamba Chukua Chako Mapema. Inaelekea Mhe. Spika, kwamba zikija hizi ripoti ni sisi kwa sisi tunaowatoa wale wanaoharibu maendeleo na kuchukua fedha za umma tukawafanya kwamba wao hawana kosa. Sasa mimi hujiuliza aah! Kumbe ni jumla ya moja ya maana ya CCM.

Lakini sasa Mhe. Spika, hivyo wanavyovichukua sio vyao peke yao, hivi ni vya umma. Kwa hivyo, kama ni vya umma basi ni lazima Baraza lisimamie na serikali itekeleze maazimio ya Baraza. Kinyume na hapo Mhe. Spika, *kichukuliwacho humaliza*, mtakuja kutuongoza vipi, kama tukisema mtoto wangu, ni mtoto wa shangazi, ni mjomba kwa sababu sisi Wazanzibari sote tunajuana tutafika wapi. Mhe. Spika, '*huruma hazilei mwana*'. Mimi nakubaliana na maoni yote yaliyotolewa na kamati, kwamba hatua za nidhamu zichukuliwe. Nahisi kama hatua za nidhamu zitachukuliwa basi nina uhakika Zanzibar tutafika katika maendeleo.

Mhe. Spika, nikija katika ukurasa wa 6 hadi wa 8 wa ripoti hii, yamezungumzwa mambo mbali mbali hapa ambayo yamegunduliwa na Kamati. Lakini nataka niseme katika ukurasa wa 8 mwishoni pale pana mistari mitatu na kidogo, naomba niruhusu niisome, inasema kwamba

> "Aidha, kamati ilipata fursa ya kukutana na wakuu wa idara mbali mbali wa shirika kwa nyakati tofauti, katika kikao hicho wakuu hao wa idara walishtumiana ikiwa ni pamoja na idara moja kudhorotesha maendeleo ya idara nyengine"

Mhe. Spika, taasisi yoyote ikifika pahali ikawa sasa watu hawaaminiani tena, wao kwa wao wanashtumiana, wao kwa wao watakuwa wanafanya vibaya basi hapo panahesabika hapana tena kazi, watu hapo wasubiri mwisho wa mwezi wachukue mishahara na maposho mengine. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hili ni tatizo, hapa hapana tena kazi. Ndio utakuta Zanzibar maeneo yetu mengi nguvu hizi za umeme hazifiki, kumbe idara kwa idara hawapendani, idara kwa idara hatushirikiani vipi wananchi watafikia maendeleo na sisi wenzetu tumewaamini wachukue nafasi hizi ili watupeleke katika yale maendeleo tunayoyakusudia. Leo hakuna tena maelewano, kwa hivyo Mhe. Spika hili ni tatizo na linastahiki kufanyiwa kazi na serikali suala hili walichukue haraka kulifanyia kazi, kwa sababu idara kwa idara tena shirika moja maelewano hamna. Mhe. Spika, ni sawa sawa na mtu aliyekuwa na mke wa ndoa, inafika pahali mume haelewani na mke na mke haelewani na mume, lakini magombano yale watoto waliowazaa wanawasikia. Kwa hivyo, na wale watoto wanaompenda mama hawasikilizani na baba na wanaompenda baba hawasikilizani na mama, maendeleo katika nyumba hiyo itakuwa hapana.

Kwa hivyo Mhe. Spika, hapa imejionesha wazi kwamba maendeleo ya shirika hili hayapo kwa sababu maelewano yamekuwa hafifu mno. Naiomba sana serikali ilisimamie hili na wanaohusika basi wachukuliwe hatua.
Mhe. Spika, tunapofikia katika mambo kama haya basi utakaotawala hapo ni ubaguzi, wale watajiona ni Wapemba na wengine watajiona ni Waunguja, wale watajiona ni Waarabu na wale watajifanya ni Waswahili, kila mmoja atakuwa anajiona yeye ni bora kuliko wengine. Kwa hivyo, ufanisi wa shughuli zile utakuwa haupatikani. Nilisema msemo mmoja wa Kiswahili, '*ukichelea mwana kulia utalia wewe'* Mhe. Spika.

Kwa hivyo, ili kulinusuru shirika basi mimi ningeiomba sana serikali, mashirika mengi wameyabinafsisha kuna tatizo gani kuhusu kulibinafsisha shirika hili la umeme kama mashirika mengine. Mimi nahisi kwamba shirika hili likibinafsishwa basi wananchi wengi tutapata nafuu kwa masuala haya ya umeme. Mhe. Spika, mtu kama mimi sasa kuingiza umeme imeshakuwa ni tatizo sugu. Hivi sasa ni Mwakilishi *Alhamdulillah*, lakini kuna watu milioni nzima sio Wawakilishi wala sio Wabunge na ziada, na wengi wao nguvu zao ni dhaifu.

Mhe. Spika, tumeona hapa katika ukurasa wa 15 hadi wa 27 jinsi watu wanavyounganishiwa umeme na pesa zile hazifiki kwenye shirika. Pahala pa nguzo na poli moja ni milioni moja na zaidi. Lakini pahali kama hapo hapo ni shilingi 400,032,000, laki tano na pesa nyengine. Maana ule mpangilio wa mahesabu haupo, hii Mhe. Spika, inauma, kwa hivyo utendaji wa haki katika shirika hapana na haki ikiwa haipatikanwi basi huhesabiwa kwamba haki hiyo haikutolewa kabisa na tumeona hapa Mhe. Spika, kwamba ni mambo yako wazi kabisa, kamati wamefuatilia vya kutosha na hawa watu wametoa ushahidi. Kwa hivyo, tumesababisha kwamba maeneo yetu mengi yakose umeme na tumesababisha kwamba mtu mnyonge asiweze kuingiza umeme, kwa

sababu sio rahisi mwananchi wa kawaida kuitimiza milioni moja na zaidi ili akaweza kupata umeme.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, matatizo kama haya ni lazima yasimamiwe kwa nguvu zote na kama hayakusimamiwa, kama ningekuwa na uwezo Mhe. Spika, basi ningeyataka mataifa yote yanayoisaidia Zanzibar yakatishe misaada yao.

UTARATIBU

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, kutokana na kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu cha 68, Mjumbe anaposema mambo yasiyofaa. Mhe. Spika, wakati mjumbe anachangia. Kwanza naomba nikinukuu hiki kifungu Mhe. Spika, "baada ya kujulisha juu ya tabia ya mjumbe anayeshikilia kusema mambo yasiyofaa kwa mujibu wa kanuni hizi, Spika, anaweza kumuamuru mjumbe huyo kukatisha hotuba yake na kukaa".

Mhe. Spika, wakati mjumbe anachangia alizungumza neno maana ya CCM na kusema kwamba Chukua Chako Mapema. Mhe. Spika, maana ya CCM ni Chama Cha Mapinduzi, sio Chukua Chako Mapema. Mhe. Spika, naomba arekebishe kauli yake, la sivyo naomba ufuate kanuni hii ya Baraza la Wawakilishi, ahsante Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Mhe. Rufai Said Rufai hebu rekebisha hiyo kauli, CCM iwe na maana ile ile ya Chama Cha Mapinduzi kama kusudio ni chama, na hii Chukua Chako Mapema isiwe inahusishwa na CCM hiyo.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nilivyosema nadhani Mhe. Mjumbe hakunisikia. Naomba uniruhusu nirudie kidogo. Nilisema kwamba vyama vya ASP na TANU sivifahamu, lakini chama nilichokuja kukifahamu ni chama cha CCM, na CCM ilivyokuja, baadhi ya watu walileta tafsiri mbali mbali, lakini tafsiri ni Chama cha Mapinduzi, hivyo ndivyo nilivyosema. Sasa ukisema watu wametoa tafsiri mbali mbali ni kweli watu wametoa tafsiri mbali mbali na nikasema hasa kwamba hasa sehemu hiyo ya serikali yaani maidara na mengineyo, kuna tafsiri inayosemwa kwamba CCM maana yake Chukua Chako Mapema. C- Chukua, C- Chako, M- Mapema, hizo ni tafsiri za watu wamezitoa sio kwamba nimesema mimi.

Mhe. Spika: Isitufanye shughuli zetu zikatetereka, hili ni suala la kuacha tu, ni kwamba CCM kwa maana ya Chama cha Mapinduzi, isihusishwe na hii chukua chako mapema kwa wizi huu. Tumalizie hapo tu kwamba hii CCM ifahamike na wananchi huko kwamba maana yake ndio hii hii ya Chama cha Mapinduzi, ni hivyo tu basi. Kwa hivyo, tuendelee, lakini nadhani utafute lugha ambayo itaweza kufahamika vile vile bila ya kuhusisha Chama cha Mapinduzi. Tuendelee Mhe. Rufai Said Rufai.

Mhe. Rufai Said Rufai: Ahsante. Hayo Mhe. Spika, yanaweza kuwa ndio mawazo yangu kwa mwisho kulisema suala hili, nashukuru. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kutokana na mwenendo huu wa kwamba kila taasisi inayofanyiwa uchunguzi, kwa kweli mwenendo wa watendaji wetu umekuwa ni mbadhirifu. Wachangiaji wengi hapa wamewasema sana wahasibu, na wahasibu sasa imeshakuwa kama ni chama cha ukoo, kama mhasibu mkuu sio mke basi chini yake ni mume wake, kama sio mume basi ni mke wake, sasa kimeshakuwa ni chama cha ukoo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama wahasibu wetu hawa na wao hawakuundiwa tume, wakenda kufanyiwa uhakiki basi nchi itakwenda na maji. Mara moja tuliwahi kusema hapa kwenye Baraza kwamba wahasibu wasifanywe wa kudumu katika maidara yao, wabadilishwe mara kwa mara. Lakini mtu tokea kashika nafasi ya uhasibu ndiye huyo huyo, pale kafanya kama yeye ndiye wa kudumu hakuna mwengine. Kwa hivyo, ubadhirifu Mhe. Spika, utakuwa ni mkubwa mno. Kwa hivyo, bado tunaishauri serikali wahasibu wetu wasifanywe ni wahasibu wa kudumu. Kwa sababu kila ukimfanya wa kudumu ndio unampa mbinu za kuweza kufanya uharibifu wa mali ya umma zaidi. Kwa hivyo hili wao ndio wataalamu zaidi. Naiomba serikali kwamba kuwe na mbadala wa wahasibu. Pia hili nashauri sana kuwa na wahasibu wote wakaguliwe.

Mhe. Spika, maneno ni matamu, lakini aibu ya maneno ni kuingiliwa na maneno. Kwa hivyo, vile nilivyokuwa nikiweka *target* zangu kwa kiasi fulani Mhe. Nassor Salim Ali kidogo amenichanganya Mhe. Spika. Mhe. Spika, nadhani *message* imefika. Kwa hivyo, naunga mkono ripoti yote hii ya kamati ya PAC, sishauri kwa serikali kwa sababu sisi sio washauri ni waamuzi, serikali itoe maamuzi ya haki kwa wote wale waliotajwa katika ripoti hii. Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hapana shaka marudio ya maelezo ya michango mbali mbali kwa kiasi fulani inaonesha kwamba hakuna zaidi jipya. Kwa hivyo, tuwamalize hawa wachache waliobaki bila ya kurudia sana na tuokoe muda ili twende sasa kwa upande wa mawaziri. Basi kwa haraka nimkaribishe Mhe. Farida Amour Mohamed na baadae Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Ripoti hii ya Kamati ya *PAC*. Mhe. Spika, kabla sijatoa mchango wangu naomba nitoe masikitiko yangu kidogo kutokana na ripoti yetu hii, juzi iliposomwa ripoti hii Mhe. Spika, hii ni ripoti muhimu inayoangalia uti wa mgongo wa nchi yetu.

Lakini kwa bahati mbaya sana Waziri anayehusika na wizara hii hakuwepo, sasa hili kwa kiasi fulani lilitutia wasi wasi na lilitutia shaka baadhi ya Wajumbe kuona kwamba waziri hakuwepo hapa, ili kuona michango itakayotolewa au akaona ile ripoti inaposomwa.

Kwa kweli, ripoti inaposomwa ni tofauti na anapokuja mtu akakwambia, kwani ripoti ni kubwa na pengine mtu hana uwezo wa kuisoma yote kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Sasa angekuwepo mwenyewe ingekuwa ni vizuri zaidi akasikia jinsi ripoti inavyosoma na yale mambo yaliomo.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa akatupa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Pili napenda nimpongeze sana Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*). Kwa kweli Mwenyekiti huyu amefanya kazi kubwa ya kusimama pale masaa karibu manne kwa ajili ya kutoa taarifa hii kama ni mimi mjumbe wake nafikiri ningeanguka pale na nisingeweza kuisoma yote, nampongeza sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Sasa niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Mhe. Spika, ripoti hii mwanzo ilikuwa ni hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija, lakini baada ya kuileta hapa akaikabidhi Baraza la Wawakilishi kupitia wewe Mhe. Spika wetu mahiri ukaikabidhi Kamati ya *PAC* kwa ajili ya kufanya uchunguzi. Kwa hivyo, naomba kwamba hoja hii si hoja ya Kamati ya *PAC* wala Mhe. Omar Ali Shehe isipokuwa hoja au ripoti hii ni ya Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, upotevu wa fedha katika shirika unatokana na uungaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasiokuwa waaminifu. Mhe. Spika, ni kweli usiofichika kama fedha za shirika zinapotea sana kwa sababu ya hawa watendaji wasiokuwa waaminifu na mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati hii ya *PAC*. Kwa kweli tumefanya kazi kubwa katika mazingira magumu na kuona kwamba ni kweli fedha zinapotea.

Fedha hizi zinapotea katika nyanja tofauti. Kwa mfano, baadhi ya wateja wanapotaka kuungiwa umeme wanatoa malipo yao kwa muda mrefu wanakaa bila ya kufanikiwa. Sasa matokeo yake wengine wanakata tamaa na kuchukua fursa hii ya kuwatafuta watu waliokuwa si wahusika (vishoka) wakenda kuwaungia umeme ule kinyume na utaratibu na matokeo yake pale zinaanza kupotea fedha za shirika.

Vile vile kuna baadhi ya wateja wanaungiwa umeme kwa bei tofauti. Kwa mfano, mteja anaweza kufanyiwa malipo makubwa na mwengine anafanyiwa malipo madogo na hali hii haipendezi kwa sababu wateja wote ni wetu. Kwa hivyo, tunatakiwa tuwaenzi hawa wateja wetu, ili shirika letu lipate kwenda mbele.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye maduka yaliyopewa vibali vya kuuzia vifaa vya umeme, lakini kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya maduka kwenye orodha yamo wameambiwa hawa watauza vifaa vya umeme. Kwa kweli naona hata juzi tu hapa Mhe. Ussi Jecha Simai alisema amenunua nguzo katika duka lakini baadaye akaambiwa nguzo zile hazifai na kupata hasara kubwa.

Kutokana na hali hiyo, Shirika la Umeme liwe na mpango maalum wa kuaminika kwamba duka hili ndilo linalouzwa vifaa na mtu akinunua vifaa na kupeleka pale asijekuambiwa vifaa hivi havifai.
Mhe. Spika, pia mbali ya upotevu wa fedha hizi kugawa makundi katika shirika. Kwa kweli shirika ni moja na wala haipendezi hata kidogo kuambiwa kuna watu au majina kama vile *State fuel* na *ZECO*, tukifanya hivyo maana yake ni kuwa unawagawa wale wafanyakazi na unawakosesha ari ya kufanya kazi na kulipatia shirika letu mapato. Mhe. Spika, hili lipo na tumeliona kwa macho yetu kwamba kuna *state fuel* na *ZECO*. Kwa kweli hili halipendezi na linapotezea mapato yetu ya shirika.

Pia baadhi ya maeneo tumegundua mambo ya malipo madogo na makubwa. Kwa mfano, tumemkuta bwana mmoja katika kijini cha Kigongo Wambaa mbele ya viongozi wa shirika ametoa kauli yake kwamba yeye amelipa shilingi milioni 8, lakini risiti iliyotoka kwenye shirika ni 167,320/-. Sasa je, Mhe. Spika katika hili kweli tunapata mapato au tunapoteza mapato ya shirika.

Kwa kweli suala hili halipendezi na inaonesha wazi kwamba fedha za shirika zinapotea na ile kesi aliyoeleza mwenyewe Mhe. Hija Hassan Hija kuileta kwenye Baraza la Wawakilishi imethibiti na tumeiona wazi wazi.

Mhe. Spika, kuna mteja mwengine ambaye ni mfano wa huyu huyu, mteja huyu ambaye amelipa shilingi milioni 37,720,000/- na kwenye risiti kuna shilingi milioni 2,052,000/-. Sasa Mhe. Spika, katika hali kama hii kweli shirika litajiendesha kwa faida au hasara, kwa hivyo tunaposimama hapa Wajumbe tukitetea tusionekane kama sisi tuna lengo la kumkomoa mtendaji yeyote wa Shirika la Umeme.

Kwa hiyo, sisi tunasema haya kwa sababu ya kuisimamia serikali yetu kwa manufaa ya wananchi wetu, kwa sababu wananchi ndio wanaoumia Mhe. Spika na wala sio mtu mwengine yeyote na hatuna lengo la kumkomoa mtu. Hii ni kazi ambayo tumetumwa na Baraza kwenda kuifanya na matokeo yake tumeyapata ndio maana tumeyaleta hapa, ili yarekebishwe na yachukuliwe na pakionekana pahala kuna kasoro basi zirekebishwe Mhe. Spika. *(Makofi)*

Jambo baya zaidi kwa mteja huyu fedha hizi zimeingizwa kwenye *account* ya mtu binafsi ambaye ni mfanyakazi wa Shirika la Umeme. Je, shirika hili halina *account* mpaka fedha hizi ziingizwe kwenye *account* ya mtu binafsi. Mhe. Spika, inasikitisha jinsi fedha za walipa kodi wa nchi hii zinavyoingia ndani ya mifuko ya wachache.

Mhe. Spika, kuna baadhi ya wafanyakazi wanakaa ndani ya ofisi za kazi mpaka wanastaafu mtu kibanda cha kuishi hana, lakini kuna baadhi ya wenzetu wanafanya kazi muda mfupi mtu anakuwa na magari, nyumba pamoja na mambo mengine na hii ni rushwa kama hawajui.
Mhe. Spika, naomba wenzetu walielewe hili na wala wasifikirie kwamba sisi tunafanya haya kwa sababu ya kuwakomoa.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niendelee kuzungumzia kuhusu suala la uungaji wa umeme kwenye minara ya simu kupewa watu binafsi. Kwa kweli shirika letu lipo Mhe. Spika, tena shirika letu lina wafanyakazi mahodari, mahiri tena waliosoma, kwa nini hizi kazi kubwa za kulipatia shirika letu maslahi zinapelekwa kwa watu binafsi.

Jambo la kusikitisha zaidi kwamba kazi hizi zinapelekwa kwa watu binafsi, lakini watendaji au wafanyakazi waofanya kazi zile ni wafanyakazi wale wale wa Shirika la Umeme na rasilimali zile za shirika ndizo zinazofanyiwa kazi ile. Mhe. Spika, hali hii haipendezi na tunasema na watu watatuona wabaya, lakini sisi tunafanya kazi tuliyotumwa kwa mujibu wa sheria na kuifanya kazi tupate maslahi ya wananchi wetu.

Katika kufanya utafiti wetu tumekuta baadhi ya sehemu watu wenyewe wa Shirika la Umeme wamefanya utafiti wa kugundua baadhi tu ya wateja ambao hawamo ndani ya orodha ya *files* za wateja. Mhe. Spika, watu hao waliofanyiwa utafiti na kugundulikana ni watu au wateja 23 tu, tena hao kwa Kisiwa cha Pemba.

Sasa tufanye tathmini 23 Kisiwa cha Pemba walionekana hawamo ndani ya Daftari la Wateja na wala hatujui wameungiwa vipi na wanalipa vipi, je ikifanywa tathmini kwa Zanzibar nzima

tunapoteza kiasi gani cha fedha zetu za shirika Mhe. Spika na hii ndio hali ya shirika letu ilivyo. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu utaratibu wa maombi ya kuunga umeme kwa wateja wa mahoteli hawafuati utaratibu, labda ni baadhi tu ya mahoteli tuliokwenda tukakuta watu wameomba au wateja wale kwa mujibu wa sheria. Lakini mahoteli mengi hayakufuata utatibu wa sheria.

Mhe. Spika, tofauti kubwa ya malipo ya umeme kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Kwa kweli hili labda tuchukue mfano wa mfanyabiashara wetu maarufu Said Salim Bakhressa anapofanya biashara zake kule Tanzania Bara analipa kwa *unit* moja shilingi 118 na anapokuja kuwekeza hapa Zanzibar analipia shilingi 210 kwa *unit* moja.
Sasa Mhe. Spika kweli hawa wenzetu wa Muungano wanatuonea huruma sisi. Kwa hivyo, suala hili mbali ya kumuumiza yeye linatuumiza wazanzibari kiuchumi Mhe. Spika, kwa sababu watu wote wanaotaka kuwekeza basi wataona ni afadhali wakawekeze Tanzania Bara, kwa sababu ya unafuu kuliko kuja kuwekeza hapa kwetu na hapa wanatukimbia na inakuwa maslahi na maendeleo ndani ya nchi yetu hayapatikani Mhe. Spika.
Mhe. Spika, kwa kumalizia nataka niseme shirika ni letu na Zanzibar ni yetu sote wazanzibari. Sasa kwa nini baadhi ya watu waajiriwe na wengine wasiajiriwe, yaani upendeleo katika ajira upo Mhe. Spika na utaendelea kuwepo. Kwa hivyo, wenzetu wa shirika wajue hili na wala hatulisemi hili kwa kubuni, kwani tumeliona kwa ushahidi kamili.

Lakini kwa kuwa umesema mambo tusirudierudie na hili tayari limeshachangiwa na lipo na litaendelea kuwepo kama wenzetu wa Shirika la Umeme hawajawa tayari, isipokuwa wawe tayari kuwatumikia wazanzibari wote, yaani kila ambaye mwenye haki ya kupewa ajira kwa mujibu wa taratibu na elimu yake basi apewe.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha zaidi baada ya kupita Kamati ya *PAC* katika Shirika la Umeme kuna baadhi ya wafanyakazi wakiwemo wasoma mita waliwafukuza kazi na sijui khofu yao ilikuwa nini. Wakati Mwenyekiti wetu wa Kamati ya *PAC* alishikilia sana kwamba jamani sisi tumekuja hapa na wala hatukuja kumfukuza mtu kazi na sisi hatuna uwezo wa kumuhukumu mtu, lakini kwa bahati mbaya sana hilo limetokezea.

Sasa baadaye wenyewe walivyoona wakawarudisha baadhi yao, lakini mmoja mpaka hivi sasa bado hawajamrudisha kazini. Kwa hivyo, kama walimuajiri hapo mwanzo hana sifa kwa nini hivi sasa wamuachishe kazi na hao wengine waliowaajiri hawana sifa na tumewakuta watu wameishia *Form II* na wengine darasa la saba wameajiriwa.

Mhe. Spika, watu wa Shirika la Umeme wajue kwamba Zanzibar ni yetu sote na shirika pia ni letu sote na kila mmoja anayo haki ya kupata ajira ndani ya nchi hii.

Mhe. Spika, ahsante kwa kumalizia naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*) kwa kusoma hotuba au ripoti hii mbele yetu kwa faida ya Baraza lako tukufu pamoja na wananchi kwa jumla. *(Makofi)*

Kwa kweli kazi ni nzito sana ambayo tunayoifanya hapa na kwa vile sisi ni Wawakilishi wa wananchi ilitubidi tufanye kazi hii, ili tuweze kuileta hapa Barazani na kujadiliwa.

Mhe. Spika, kwanza awali ya yote niseme kwamba wakati wa asubuhi hapa Waheshimiwa Wajumbe walikuwa na wasiwasi wa *CAG*. Kwa kweli kwanza *CAG* nimpe hongera kwa kazi zake nzuri ambazo anazozifanya na kamati hii ni kusema kwamba bila ya kutufundisha au kutupa mafunzo basi isingefikia hapa. Kwa maana hiyo, *CAG* kazi yake ni ngumu ambayo ni nzito tena ni kazi za lawama.

Mhe. Spika, mara nyingi ameshaleta ripoti zake za ukaguzi wa fedha kwenye mashirika yote pamoja na wizara za serikali, yote haya anayasikia na anatizama moja baada ya moja na kwenye mapungufu analeta mbele yetu na sisi kama kamati za Baraza lako tukufu tunazifanyia kazi. Kasoro nyingi ambazo tumeziona ni zile kasoro za kawaida ambazo tunaziona kwenye maeneo mbali mbali.

Kwa mfano, suala la upotevu wa mapato. Mhe. Spika, ni kweli mapato yanapotea kwenye taasisi mbali mbali na kama mapato yanapotea, basi ni sahihi kabisa patakuwa hapana mafanikio. Jambo la msingi ni kufuata zile kanuni na taratibu za manunuzi pamoja na matumizi ya fedha za serikali. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, ni kweli kwamba upo upotevu wa fedha kutokana na kuunga umeme na wale wanaojulikana kwa umaarufu kwamba vishoka, ambapo tunawaona na hata wenyewe *management* ilikuwa inashangazwa na mambo kama yale. Kwa hivyo, ni jambo ambalo tunasema halikufanywa na *management* isipokuwa na wafanyakazi wachache ambao wanapenda kujipatia mambo au utajiri wa haraka na haya mambo yapo kila mahala. *(Makofi)*

Mhe. Spika, niseme kwamba mashirika mengi yanakuwa na bodi na hata wakati nilipochangia kwenye hizi sheria tulizopitisha juzi nilizungumzia kuhusu hili kwamba zile bodi zenyewe ziwe na utaratibu wa kuyafuatilia haya mashirika, kwa sababu unakuta kwamba tokea asubuhi hapa alikuwa anazungumzwa Mwenyekiti wa Bodi.

Kutokana na hali hiyo, hawa wenyeviti wa bodi wawe waadillifu na hii kama walivyokwisha kusema wenzetu kuwa Zanzibar ni yetu sote na wala hakuna kwamba utamuelekeza mtu fulani, kwa sababu kwenye shirika nahisi wako watu tofauti na itikadi tofauti.

Kwa hivyo, hili si kwamba limelengwa mahala fulani, kwamba Pemba ndio kwenye, lakini kule Pemba tumeona kwamba watu wote au wafanyakazi wengi ni kutoka Ole na Meneja mwenyewe ni kutoka Ole na wale wafanyakazi wote ni kutoka Ole.

Nadhani tutafute ule ufanisi wa ile kazi na ufanisi wa kazi ni wetu sote, lazima tushirikiane ili serikali yetu yale malengo ambayo imewayeka basi iyafikie, serikali hii ni yetu sote na sote tunahitaji mafanikio na kama tunahitaji mafanikio basi ni kusimamia zile kazi zetu kwa uzuri zaidi.

Mhe. Spika, naomba niseme kwamba Shirika la Umeme lina kazi nzito tena ni muhimu, kwa hivyo hata hiyo serikali nayo ina wajibu wake, kwa sababu kila inapotaka kuongeza bei ya

umeme mara nyingi inakuwa inarudi nyuma kutokana na labda serikali inakuwa inawaonea huruma wananchi wake.

Kwa hivyo, serikali nayo pia ione hili jambo kwamba shirika nalo linahitaji usaidizi mkubwa sana, kwa sababu serikali ina imani sana na wananchi wake, kwa maana hiyo kila inapotaka kuongeza bei ya umeme, yaani umeme mpaka hivi sasa bado wao wanakula hasara.

Mhe. Spika, niseme kwamba serikali nayo ina jukumu lake kwa wananchi wake, kwa sababu inataka kila inapoongeza bei Shirika la Umeme linarudi nyuma. Kwa hiyo, hapa ni lazima shirika hili litakuwa linakula hasara na bado fedha zinalipwa na deni bado lipo, kwa kweli serikali ilisaidie sana shirika.

Vile vile Mhe. Spika, kama ilivyo kwa mashirika mengine kama ulivyo utaratibu wa kuuza mali za serikali lazima kuna utaratibu huo na hapa zipo na wala sio shirika hili tu, kwa kweli mashirika yote tunakuja kuona kwamba kila tunapopata Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haya mambo tunayakuta.

Kwa mfano, kuna vitu vinauzwa bila ya utaratibu, kwanza hawana *asset register*, kwa sababu lile lina sehemu tofauti ambazo zinaonesha *data* mpaka kile chombo kilivyonunuliwa, yaani siku iliyonunuliwa, thamani yake na kila mwaka kunakuwa na hali ya kushuka thamani kwa mali na hata zile *register* hakuna. Kwa hivyo, inakuwa hakuna yule mdhibiti wa zile mali zenyewe za serikali.

Kutokana na hali hiyo, ni lazima kwa mujibu wa mambo ambayo tumeyaona hapa na mengi ambayo tumeyaona na sisi tunasema kwamba tuilete hapa, lakini bado sisi hatujawa waamuzi wa mwisho.

Kwa maana hiyo, serikali ichukue juhudi kwa vyombo vyake vinavyohusika na ufanywe uchunguzi, kwa sababu tunaona hali ilivyo kwamba pale inakuwa hakuna maelewano ya wafanyakazi wenyewe, yaani kuna matabaka ya wafanyakazi. Mhe. Spika, hapa panaweza kuwa na mtu mwengine anaweza kumfanyia mtu mwenziwe kitu, lakini sisi tumefanya kazi kwa namna tulivyotumwa na Baraza.
Kwa hayo, machache Mhe. Spika naomba kuunga mkono hoja au ripoti hii kwa asilimia mia moja.

Mhes. Spika: Mhe. Hamza Hassan Juma, wakati wa asubuhi hukuwepo sasa ujue kwamba ripoti hii watu wameshainywa sana kwa kuchangia. Kwa hivyo, utumie muda mfupi si kama ile kawaida yako. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma nakukaribisha uchangie na baadaye Mhe. Abdalla Juma Abdalla.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache kabisa. Lakini Mhe. Spika, mjadala huu tangu asubuhi kama ulivyosema nilikuwa sipo nilikuwa na dharura ya kifamilia, lakini nilikuwa na redio yangu mfukoni na nimemsikia kuanzia wa mwanzo mpaka wa mwisho mpaka swahibu wangu Mhe. Mansoor Yussuf Himid nimemsikia.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, nashukuru kwa maana hiyo hutorejea rejea.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi kwanza nataka niipongeze sana Kamati hii ya *PAC*, ambapo ilirekebishwa kidogo ikafanywa kama ni Kamati Teule kwa kushughulikia hoja maalum. Kwa hivyo, tunawapongeza sana kwa kazi ambayo waliifanya na inazidi kulijengea heshima Baraza letu la Wawakilishi. *(Makofi)*

Kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kwa nini nikataka nianze kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na kwamba hajasimama kuchangia, lakini anaridhika sana na Kamati ya *PAC* jinsi inavyofanya kazi zake na inavyoleta ripoti hapa Barazani. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa ushahidi huo hata yeye mwenyewe amekusudia kutafuta namna yoyote kuzidi kuipa mafunzo Kamati ya *PAC*. Kwa hivyo, hili nampongeza sana na ninaamini hii kazi iliyofanywa na *PAC* itamrahisishia sana kuweza kutekeleza au kusimamia majukumu ya serikali. Kwa maana hiyo, Mhe. Spika Viongozi wetu Wakuu wao wanapita juu tu na huku chini hawaingii na wala hawajui kuna nini.

Lakini sisi Mhe. Spika unatutuma na tunakwenda ofisi kwa ofisi ya serikali na kukagua tunaanzia tunapowaidhinishia hapa, wanachokikusanya na namna gani wanavyotumia. Kwa hiyo, lazima tuweze kuisaidia serikali yetu. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba nianze kuchangia hii hoja. Mhe. Spika, nataka niseme kwanza wale wote waliobainika kuiba fedha za shirika wazirudishe, lakini sio kurudisha tu na baadaye sheria ifuate mkondo wake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi karibuni nadhani Baraza lililopita tulipitisha Sheria hapa ya Masuala ya Kupambana na Rushwa na Mkurugenzi ameshatangazwa, sasa tunataka aanzie hapa na tumuone namna gani anavyoanza kufanya kazi yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hapa kuna mambo mawili, yaani kuna mambo ya Baraza kuisimamia serikali, kwa hivyo wale wote ambao wenye nafasi za uteuzi sisi wale tunaowajibu wa kuisimamia serikali na kuwawajibisha na wala hakuna haja ya kuunda tume nyengine, kwa sababu kama hii ripoti ni moja na vielelezo ni *documents* mbili na kazi hii imefanywa kitaalamu sana. Kwa hivyo, kwa wale ambao wateuliwa katika shirika mimi nafikiri Mhe. Spika huu ndio wajibu wetu kuisimamia serikali.

Kutokana na hali hiyo, tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na wala hatumtaki, isipokuwa tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hili aondoke nalo na aende nalo kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa wale walioliibia shirika kama nilivyosema mwanzo kwanza fedha zetu wazirudishe na halafu baadaye TAKUKURU lile jina nimelisahau kidogo na kule Bara kuna TAKUKURU hapa sijui serikali yetu tunaliita vipi, lakini mimi naliita ZAKUKURU waanze kuwaburuza watu hawa mahakamani.

Mhe. Spika, nataka niseme kwa nini nikasema hivyo, wananchi wa Zanzibar ambapo wengi wao wanaishi katika maisha ya hali ya chini kabisa, hivi sasa wanabeba mzigo ambao hawauwezi, yaani mzigo mzito wa bei ya umeme kumbe wanaowabebea watu wenye uwezo wao.

Mhe. Spika, Baraza lililopita wenzetu hawa wa *ZECO* kwanza walituletea mapendekezo tukatangaziwa hapa tukaungiwe mita za TUKUZA na mpaka leo bado sijaiona mita ya TUKUZA wala nini, kwa hiyo tunaomba kwanza ile ahadi yao watutekelezee.

Jengine walitupa semina kidogo ni namna gani gharama za umeme zinavyopanda na wakatu-*alert* kwamba huu umeme hii bei waliopandisha hivi karibuni sio kama ndio mwisho, isipokuwa wataendelea kupandisha kwa *installment* kutokana na yale maelezo yao mengine marefu na mazuri tuliridhika, lakini kumbe mimi nataka kusema kwamba hawakutuambia ukweli na wala sitaki kusema walitudanganya.

Miongoni mwa maelezo yao ni kwamba gharama za umeme Pemba, yaani umeme unaotoka Tanga kwenda Pemba mpaka hivi sasa kwa kule Pemba bado hakujawa na matumizi makubwa, kwa hiyo shirika linabeba mzigo mkubwa sana.

Lakini kama ingelikuwa umeme ule kutoka Tanga unaokwenda Pemba ingelikuwa wanalipa wenyewe wananchi wa Pemba moja kwa moja basi wangelilipa mara mbili ya hii bei wanayolipa hivi sasa. Kwa mfano, hapa tunalipa unit moja kwa shilingi 220 basi kule wangelilipa kwa 240, lakini lile deni lao limejumuishwa pamoja na Unguja, ili kuweza kuwapunguzia mzigo wenzetu.

Mhe. Spika, kumbe si kweli, isipokuwa kuna mapato mengi ambayo yalikuwa yanakusanywa kule ya kuweza kufidia zile gharama za umeme na mapato yale yanaingia mifukoni kwa watu na wala hili hatuwezi kulistahamilia hata siku moja. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Spika, wenzetu lazima wawe wakweli kwa sababu sisi wanapotwambia na sisi tunawaambia wananchi wetu. Lakini unapokwenda *deep* kufuatilia taarifa zao, basi matokeo yake ndio haya.

Mhe. Spika, hapa kuna watu wametajwa kwa majina, yaani wamelipa fedha nyingi, lakini kwenye shirika zikenda kidogo na fedha nyengine zikaingia mifukoni. Mhe. Spika, kwa mujibu wa taratibu hawa wote wanaiibia serikali, kwa hiyo kama kuna mtu gharama alizopelekewa kwa mfano kama ilivyoandikwa humu shilingi milioni 37 Pemba Misali na fedha nyengine akaambiwa aziingize kwenye *account* ya mtu na hizo hakulipia shirika amemlipa mtu au amemgaia.

Sasa yeye na huyo mtu aliyemtilia kwenye *account* yake wakashtakiane, lakini fedha hizi sasa zilizoingia nje ya *account* ya shirika zikalipwe tena, kwa maana hiyo hizi tunaandika deni, kwa sababu wewe kama unahudumiwa na shirika kwa nini ukalipe kwenye *account* ya mtu binafsi, aidha unashirikiana katika wizi au hizi fedha amemgaia na kuambiwa alipe kidogo.

Kwa hiyo, hizi kama ingekuwa ni gharama halisi ya shirika basi fedha hizi tunahesabu ni deni, kwa maana hiyo deni hili walilipe. Mhe. Spika, tunapokuja mwezi wa Aprili katika kuchangia

ripoti za kamati tutauliza kama deni hili limeshalipwa. Hapa kuna nambo mawili, huyu mlipaji wa Pemba Misali amburuze huyo mtu Mahakamani au amrejeshee pesa zake milioni 35.
Lakini vile vile serikali imtake huyu mama kwa nini akatumia *account* yake wakati ni mfanyakazi wa shirika. Kwanza huyu hafai tena kuwa mfanyakazi wa shirika. Kwa sababu kwanza mwizi analiibia shirika anatumia mamlaka yake, ile ya kutumia taasisi hii ndio kutumia malaka vibaya anatumia shirika lakini fedha zinaingia katika mfuko wake.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba ZAKUKURU huyu mama Zakia nafikiri Jumatatu isifike awe keshafika Mahakamani, kwa sababu huyu mpaka ushahidi wa *account*, huyu tena sijui unatafuta nini. Huu ushahidi wa wale shemeji zangu, ushahidi wa kinyamwezi mpaka *account* namba, fedha zilivyoingizwa kwa tarehe. Kwa hivyo huyu ndiye wa mwanzo aburuzwe Mahakamani. Mimi naamini fedha hizi sio zake peke yake. Hapa kuna cheni hizi wanakwenda kugawana. Sasa yeye akenda kuburuzwa Mahakamani na yeye atawataja hao wangine ambao waliogawana pesa hizi halafu baadae sheria nyengine zichukue mkondo wake.

Jengine Mhe. Spika, ukiacha huyu kuna na wengine hapa walilipa nao ni bwana Mohammed Habibu yeye alilipa shilingi milioni nane lakini risiti ikaandikwa laki moja na sitini na saba. Na huyu hizi pesa zilizobakia azilipe, huu ni wizi, haiwezekani unalipa huduma unatoa milioni nane unapewa risiti ya laki moja na nusu, ilikuwaje. Sisi tunaangalia fedha zilizoingia kwenye shirika ndizo ulizopewa risiti. Kwa hiyo na hili deni, hili alilipe sasa yeye huyu, huyo aliyempa hizo pesa atajua namna gani na yeye kurejeshewa pesa zake.

Mhe. Spika, kuna Bwana Hemed Suleiman wa Konde huyu kwa Mheshimiwa Maduhuli. Huyu kalipa milioni tatu risiti imeandikwa laki mbili na kumi na tatu na huyu tuna mdai akalilipe shirika, kwa kuwa kapewa risiti ya laki mbili na kumi na tatu ina maana hizi ndio pesa alizolipa. Kutokujua sheria sio kuvunja sheria na huyu pia akalipe.

Mhe. Spika, nimejaribu tu kutoa mifano ya hawa wachache kwa sababu kama ulivyosema kuna wenzangu wengine waliwataja, lakini kimsingi hawa wote jora yao ni moja waende wakalipe katika shirika, kwa sababu huu ni wizi.

Mhe. Spika, mimi nilidhani labda kuunda shirika labda ndio dawa. Juzi tu hapa tumeunda shirika la ZBC hapa, tukasema shirika linasuwa suwa kwa sababu ilikuwa idara. Sasa hili shirika maana yake limeshaota mwani kwa ukongwe hali ndio kama hii, sasa sijui la ZBC tulililoliunda nalo sijui litakuwa vipi. Mimi nadhani Waswahili wanasema mwenzako akinyolewa wewe tia maji. Shirika la ZBC tumekuundieni juzi sheria Mhe. Rais bado hajaitia saini kwa sababu ndio kwanza imo katika mchakato wa kuandaliwa, someni kutokana na makosa ya wenzenu.
Mhe. Spika, nakuja katika unyanyasaji wa wafanyakazi, sasa hivi katika unyanyasaji wa wafanyakazi Zanzibar aibu, umekuwa mwingi, mameneja wetu na wakurugenzi wetu tukishakuwapa nafasi wakishakuteuliwa wanakuwa kama miungu watu, wanawanyanyasa wafanyakazi. Mheshimiwa hili sio hapa tu katika shirika la umeme na maeneo mengine yapo. Juzi tumewasikia watu wa *Government Press* ambapo pale mimi kamati yangu ndio inayosimamia. Katika ripoti katika safari hii katika kazi za Kamati nimepanga kwenda kuna unyanyasaji mkubwa. Wafanyakazi hawalipwi haki zao, kazi zinakuja za serikali zinakwenda kufanywa nje.

Yaani mimi najiuliza Mhe. Spika, tumuombe sasa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais hebu afanye mabadiliko makubwa sana wa huku apelekwe huku na aliyekuwa kafanya manyago yake mtoe, ndio tutafanya kazi. Tatizo Mhe. Spika, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais umerithi wakati watu wameshaota nabu, hebu tengeneza wako. Tengeneza wako wafanye kazi yako, hao wanafanya kazi ya watu.

Mhe. Spika, tunasema kwa uchungu, haiwezekani leo wafanyakazi wetu wanajituma halafu unawasikia wanalalamika wanadai haki zao. Mfano *Government Press* nimeshamwambia Makamo wa Kwanza wa Rais na Afisi yako taarifa zipo Katibu Mkuu anazijua, bado wafanyakazi wale wananyanyasika. Masikini wanawake wazuri leo nyuso zimeshaanza kukunjana, watoto wadogo kwa adha wanayopewa. Mimi nafikiri wakurugenzi wawatendee haki wafanyakazi wao.

Lakini vile vile Mhe. Spika, mimi naomba sana sasa hivi katika taasisi zetu kuna mambo mengi tunakuwa tunanunua halafu yanakuwa hayafanyi kazi. Shirika la Magazeti siku niliyokwenda na Kamati yangu, samahani hii natoa mfano. Tulikagua mtambo wa rangi, tukategemea magazeti ya Zanzibar Leo yataanza kutengenezwa hapa, mapaka leo hayajaanza kufanya kazi hata siku moja. Huu ni ubadhirifu wa fedha za umma. Mimi nadhani lazima tufike pahala watendaji wetu tunapowapa majukumu sisi tunazungumza hapa kwa niaba ya wananchi waliotuchagua kutuleta hapa. Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais haya mashirika yetu ajaribu kuyaangalia sana.

Mhe. Spika, nakuja makampuni yaliyounga umeme katika minara. Mheshimiwa siku zote sisi tunasema lakini tatizo serikali haitusikii, kwamba kuna wakurugenzi wanakuwa wao wakurugenzi halafu wawekezaji. Ripoti ya Kamati iliyopita tulizungumza hapa kuna Mkurugenzi mmoja yeye hajulikani kama Mkurugenzi au muwekezaji, maana katika orodha ya wawekezaji na yeye yumo. Sasa hatujui wakati gani anafanya kazi ya ukurugenzi haijulikani wakati gani anafanya kazi ya uwekezaji. Ndiyo haya ya Shirika la Umeme leo haiwezekani wafanyakazi wa Shirika la Umeme wawili wanamiliki hisa katika Kampuni ya GECCO. Ndugu Hamidu Saidani Ali ana asilimia 20, ndugu Ali Abeid Haji ana asilimia 15, sasa hizi asilimia 65 Mhe. Mwenyekiti, hebu njoo unambie hizi asilimia 65 anamiliki nani. Kama GECCO ninayoijua miye kuna mkubwa kweli kweli hapa kuna mtu mzito anamiliki kampuni hii. Kwa hiyo kawachukua wafanyakazi wa Shirika kuna Mheshimiwa mmoja nilikuwa nasikia kwamba haya mashirika yetu yamekuwa kama mumiyani, kategа mifyusa, kabandika pale pyaaa, yuko huko Bungeni Dodoma huku anavuta fyuuu fyuuu, ndiyo! Tunajua mwenyewe yuko Dodoma kule anavuta na huku analikamua shirika.

Mhe. Spika, na huyu achukuliwe hatua za kisheria, hatua za uwajibikaji, haiwezekani, wewe Muheshimiwa mzima umechaguliwa na watu Mbunge mzima umeanzisha Kampuni unawatumia wafanyakazi wa serikali, unatumia rasiliamali za serikali, fedha baada ya kuingia kwa wananchi zinaingia mfukoni kwako, halafu unasifiwa kwa barua na prismo, tunakwenda wapi? Mhe. Spika, lazima tuwe wakweli. Mhe. Mansour alizungumza vizuri hapa demokrasia ni gharama, msumeno unakwenda huku halafu unarudi. Na huyu mwenye kampuni hii tena, kwa bahati nzuri bodi sijui wanamuogopa au sijui vipi. Labda miye huyo ninayemfikiria miye labda inawezekana ndiye sijui wa jimbo gani kama Mkanyageni au wapi. Nadhani Mhe. Mwenyekiti, atakuja kusema, maana kama tumekupa kazi ya kwenda kuchunguza uchunguze kila kitu.

Mhe. Spika, na huyu pia nilikuwa naomba kampuni hii ifatiliwe kwa nini mpaka bodi ya wakurugenzi imetoa barua kwamba kampuni hii izuiwe kazi baada yakuonekana kwamba inawatumia wafanyakazi wa shirika halafu wanatumia na rasiliamli za shirika kwa kufanya kazi ambayo Kampuni za ZECO ijiongezee mapato anazifanya yeye. Lakini pia kuna barua nyengine inayoelekeza kwamba tayari kuna kazi nyengine anafanya ndani ya shirika hili hili. Sasa tunakwenda wapi.

Mhe. Spika, najaribu kuchupa chupa ili nisirejee yale waliyoyasema wenzangu. Mheshimiwa utofauti wa bei, hii inaonyesha kutokuwa makini kwa watendaji wa shirika katika kusimamia mapato ya serikali. Hili hata bili za umeme zinazoletwa katika majumba yetu zinakuwa hazina uhakika. Wakati mwengine unamkuta mama pale shirika analia anapelekewa bili ya umeme utafikiri ana kiwanda. Kuna siku moja nimemkuta pale shirika anasema huyo mama yeye baada ya TV na taa zake hana friji, hana kuka, hana kitu chengine chochote, basi kalipa shilingi arubaini elfu (40,000) mwezi uliofuata anaambiwa alipe shilingi laki moja na sitini (160,000) anasema jamani mimi natumia matumizi gani. Kwa hiyo ina maana kumbe huku kuna watu wazito wanatumia umeme bure lakini wanaokamuliwa wengine.

Mhe. Spika, ukitaka nikwambie kuna maeneo wafanyakazi wa shirika mpaka wanataka kupigwa, unampelekea mtu bili hailingani na matumizi yake. Ndio maana tukawa tunasisitiza hebu hizi mita za TUKUZA sasa hivi ziletwe kwa wingi ili huu ubadhirifu uondoke ondoke. Leo unamkuta mtu anadaiwa shilingi laki moja inang'olewa mpaka mita, mnyonge wa Mungu hana pa kwenda anabakia analia lia. Leo hawa wakubwa mtu anaungiwa zaidi ya nguzo ngapi halipi hata shilingi. Mambo kama haya kwa kweli hatuwezi tukayastahamilia.

Mhe. Spika, katika mashirika haya mimi nadhani sasa hivi kamati yako ya PAC ipe kazi ya ziada. Mimi siridhiki na taarifa anazotuletea Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatuletea vijimambo vidogo vidogo ambavyo unaweza ukakusanya ripoti zaidi ya ngapi huwezi hata kukusanya milioni moja pesa zilizopotea. Leo Kamati hii imekwenda kuibua mambo mazito utafikiri Mdhibiti hayupo. Juzi wametupa semina kule, tumewasifu sana kumbe mambo yenyewe ndio haya.

Mhe. Spika, mimi nadhani tufike pahali mimi ninavyojua katika mashirika yote mimi niliwahi kuwa mjumbe wa Bodi wa Shirika la Bandari, kila mwaka kuna mkaguzi wa ndani anafanya ukaguzi wa mahesabu yenu yote halafu anakuleteeni ripoti lakini ile pia ilikuwa haitoshi, halafu kuna *external auditor* anakuja anafanya tena ukaguzi, maana yake inaweza kuwa mkaguzi wenu wa ndani yule inawezekana ikawa kuna mambo pengine anakufumbieni macho, anakuoneeni haya, lakini kuna mwengine kutoka nje kabisa, anakuja tena anatoa *certificate* nimeshaona, najaribu kutoa mifano. Ina maana hili shirika halina *internal auditor* na *external auditor*. Mimi nadhani Kamati ya PAC ifanye kazi ya ziada, ukiacha zile ripoti za Mdhibiti lakini kama wanahisi pahala kuna harufu mbaya basi waweze kufanya kazi na nguvu hizo tuwape kisheria kabisa kabisa.

Mhe. Spika, hapa katika haya mapendekezo imeelezwa hapa hatua gani zichukuliwe. Hii ya mwanzo inasema bodi ya wakurugenzi waliomaliza muda wao mwaka 2012 msisitizo ukiwekwa

kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Ndugu Muhamed Hashim Ismail na hatua za kisheria zichukuliwe.

Mhe. Spika, mwenyekiti wa Bodi siye muamuzi, Bodi ndiyo inayoamua na ndio maana juzi tulivyopitisha sheria hii ya ZBC kuna kifungu kilikuwa kinasema mjumbe mmoja anaweza kuchukua dhima au dhamana ya kufanya mambo chungumzima kwa niaba ya Bodi hii ni hatari. Kifungu kile sijui tulivyokipitisha sijui ilikuwa vipi, kama tulisinzia, hatari yake ndio inakuja kuwa kama hii. Huwezi ukamuadhibu mtu mmoja kwa sababu yeye yule ni Mwenyekiti wa Bodi lakini pale maamuzi yanakwenda kwa *consensus*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwa sababu mimi Muhammed Hashim namjua sana. Mimi niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi na Fedha. Mhe. Spika, ZRB mwaka 2000 alipokabidhiwa huyu bwana kulikuwa mpaka viinua mgongo hakuna, kulikuwa mpaka mishahara hakuna, alianza kuongeza mapato hatua kwa hatua mpaka ikafikia hatua ambayo kwamba serikali sisi mfano uchaguzi uliopita mpaka tunaingia kwenye uchaguzi kuna fedha zimebakia ndani ya mfuko wa serikali.

Mhe. Waziri wa Fedha kaja katueleza, kwamba kuna fedha tulihoji kwamba zilikuwepo wapi. Akasema huwezi ukamaliza utawala wa serikali unaingia utawala mwengine hakuna pesa iliyobakia ya serikali inayokuja kama kulitokea machafuko hakuna mapato alifanya kazi nzuri. Sasa leo ilikuwaje kama huku kumetokezea mambo haya. Mimi nadhani Mhe. Spika, ndugu Muhammed Hashim alifanya kazi nzuri sana ya kuongeza mapato na mpaka sasa hivi. Mimi najaribu sana kufatilia ripoti tokea kuondoka yeye mapato yameanza kushuka sasa hivi, sijui kama hii taarifa tunayo vizuri. Lakini mimi hiyo taarifa ninayo ZRB mapato yameanza kushuka, kuna nini hebu jiulizeni. Tusifanye masihara sana katika kuendesha nchi. Kama hakuna mapato kule ZRB tutakuja kukimbiana sote hapa, tutakuja Mheshimiwa tutapiga vikao wiki hapa, Mhe. Spika, utaingia huku ukitoka huku hakuna kitu kwenye mfuko.

Kwa hiyo ZRB tunawapa angalizo kuna nini mbona mapato yanashuka, mwenzenu alipokuwepo tokea alipokaa mpaka kaondoka mapato yalikuwa yanakuwa na ndio mpaka tukafika pahala Mheshimiwa tukasema TRA ule ukushanyaji wao wapewe ZRB. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana hapa nilipoona hii nilishtuka kidogo nikasema tena huu au ndio anapea tena, maana yake ndio unajua papa akipea anakuwa yale mapembe yake yanazidi. Lakini bado mimi nadhani kama kuwajibika basi ni lazima iwajibike bodi nzima, kwa sababu maamuzi yanayotoka yanakuwa ni maamuzi ya Bodi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nataka niseme mapendekezo yangu ya ziada kwenye Kamati. Kamati imeleta mapendekezo yake na mimi nina mapendekezo kidogo ya ziada. Kwanza shirika la ZECO lote livunjwe liundwe upya. Tunao wataalamu wengi humu wa kukusanya fedha, tuna wataalamu wa *planning* na kila kitu. Shirika hili kama tutaweza kulifumua tukaliunda upya, litakusanya mapato na lile deni ambalo tunadaiwa na TANESCO kule litakuwa linapungua kidogo kidogo mpaka litamalizika. Mhe. Spika, wahasibu hawa waondolewe mara moja wote wa Unguja na Pemba, wahasibu wako wengi wapelekwe wengine pale wakaanze kushika hizi nafasi.

Mhe. Spika, jengine wakubwa waache kwenda kuomba mafuta kule ZECO wakubwa gari zenu haziondoki, huku mnasema huku mnakwenda kuwaomba mafuta, siku zote, tuache Mhe. Spika.

Nadhani hili la wakubwa kwenda kuomba mafuta sitaki liingie katika ripoti lakini haya mambo mawili nasema kwamba nataka shirika livunjwe kabisa liundwe upya, wahasibu wale wahamishwe lakini vile vile wale wote ambao wamehusika na kadhia moja au nyengine ya kuiba pesa za shirika, fedha hizi kwanza wazilipe halafu baadae Mkurugenzi wa ZAKUKURU hapa ndio pahala pa kuanzia kazi.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, pamoja na ufafanuzi utakaotolewa na Mawaziri, hatujaujua utatolewa vipi kwa sababu hii ripoti baadaye tunataka kuipitisha na tutakapopitisha tutapitisha fungu kwa fungu. Jengine Mheshimiwa samahani nilikuwa nataka kusema je, Mawaziri hii ripoti imetolewa tokea siku ya Alkhamis waliwaita watendaji wakakaa nao. Kwa sababu ina maana hapa ilikuwa kila mmoja pale alipoguswa, maana hapa Mawaziri kama hawakukaa na watendaji watajibu nini. Hii ripoti imekuja na *evidence* sasa kama Waziri atataka kupapatua katika hili anapapatua atutolee na *evidence* yake yeye, vyenginevyo kama mtu hana la kusema hapa asisimame kabisa. Watendaji ilikuwa siku nne tumekaa Alkhamis, Ijumaa, Jumamosi, Jumapili, Jumatatu, leo tunajadili ripoti, Mawaziri wamekaa na watendaji kuwahoji wewe umeguswa na hili vipi. Kwa sababu hapa ripoti hii ikishakupita ni *final* hakuna tena serikali wakakae waje watujibu tena. Mtindo ule Mhe. Spika, hatutaki tena, maamuzi ya hapa tunayoyatoa ni maamuzi ya Baraza yakatekelezwe.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunpatia nafasi hii na hasa kwa sababu ni mjumbe wa kamati iliyofanya uchunguzi wa shirika hili.

Mhe. Spika, kwa kuwa wakati mwingi umekwenda na kwa sababu wajumbe wengi wamenitangulia kusema kiasi ambacho yale ambayo nimeyapanga mengi wameshayazungumza na sitaki nirejee rejee sana kwa hivyo pointi yangu ya kwanza mpaka ya nne sitoizungumza. Nitagusia kidogo pointi ya tano mpaka ya saba.

Mimi nataka niseme linaloathiri taasisi zetu za serikali ni ukosefu wa uwadilifu. Ukiwa kiongozi wa taasisi unapaswa kuwa muadilifu katika kiwango kikubwa. Ukiwa muadilifu unaowasimamia kwanza watakuogopa lakini halafu watakuunga mkono.

Lakini pia makundi na majungu ndani ya taasisi yako hayatokuwepo. Moja katika mambo yaliyolisibu shirika la umeme ni ukosefu wa uadilifu wa *management* katika masuala ya ajira, katika masuala ya fursa kwa wafanyakazi wake. Lilipotokezea hili kulizalika makundi na makundi yakishakuwepo, majungu yakaanza. Matokeo yake watu wamefikichua kila kitu ndani ya shirika mle.

Ukweli ni kwamba hakuna taasisi hata moja ya serikali nathubutu kusema hivyo, kila taasisi ya serikali ina matatizo yake. Kuna ukiukwaji wa sheria, kuna rushwa, kuna mambo yasiyoridhisha. Lakini hayatoki mpaka *management* itofautiane na watendaji wake. Kama tutakumbuka huko nyuma kulikotokea ile kashfa ya mishahara hewa sababu ilikuwa ni hii Mhe. Spika.

Kwa hivyo kwa upande mmoja *management* ina matatizo haina uadilifu. Lakini kwa upande wa pili wanaongozwa katika taasisi yoyote ya serikali ni binaadamu na kila binaadamu ana tabia yake. Inapotokea *management* kuona utaratibu anaokwenda nao mfanyakazi huyu hauridhishi akamkosoa kuna mambo mawili yatatokea. Atajirekebisha au kama ni msugu hataki kujirekebisha basi yeye mwenyewe mfanyakazi atazaa makundi na atajaribu kupakaza mambo yaliyopo na yasiyokuwepo. Yote yametokea katika shirika la umeme. Naomba katika kuyaangalia na hili pia tuliangalie.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo nimelihisi limo katika Shirika la Umeme *Management* haiku makini katika kuwasimamia watendaji wake. Lilipotokea hilo ndio sasa tunakutia kuna hii kashfa ya upotevu wa pesa za serikali. Ukishindwa kuwadhibiti watu wako watafanya mambo kinyume cha sheria.

Mhe. Spika, sasa hivi ndani ya Shirika la Umeme kila mtu ni meneja wa biashara yaani yeye ana ruhusa yake ya kuweza kumpokea mteja, kumpatia vifaa, kumuungia umeme, wakati *management* haina habari. Haya tuliyaona *practical* tulivyokwenda Pemba. Katika kukagua miradi ya umeme kule Pemba tulikuta watu tena wengi kweli kweli wameungiwa umeme bila ya lile Shirika lenyewe wale *top leaders* kujua kwamba hapa kuna mradi kumbe umefanywa. Kuna watu wanaitwa vishoka, hawa wengine ni wafanyakazi wa shirika walionekana wabadhilifu wakafukuzwa lakini wanaendelea pembeni pembeni wakifanya kazi za shirika kama madalali hivi. Lakini wengine ni wafanyakazi wa lile shirika lenyewe hasa, wanapita kwa mlango wa nyuma wanakwenda kumuibia meneja muhuri wake na pengine wanabuni mpaka saini, wanajaza mikataba wanatoa huduma za umeme wakitia pesa mifukoni, wapo tele, mpaka miye wameshanipata.

Mhe. Spika, hii ni lazima tuilaumu *management* kwasababu haipo makini katika kusimamia. Mimi nadhani labda pengine ni ukosefu wa wafanyakazi, lakini ukaguzi wa njia zile za umeme ni jambo la lazima. Unaweza kushangaa mapato mengine yanavuja kwa wale wasoma mita tu. Msoma mita uliyemuweka katika eneo fulani mpaka akishazowea ni mla rushwa mkubwa huyo, anakwenda kule anakubaliana na wateja bwana chukua elfu kumi hizi wala hasomi tena kwenye mita anaondoka anakwenda zake. Mtu halipi halipi, hata ukijakumkagua anadeni zaidi ya milioni moja hajalipa. Lakini mtu anakwenda pale anagaiwa shilingi elfu kumi anatia pesa mfukoni huyo anatoka. Yote hapo haya na haya mimi nasema ni kwasababu ya ukosefu wa usimamizi. Haya yote ni mambo ya kuangaliwa.

Jambo la mwisho sitaki nichukue muda wako mwingi. Jambo la mwisho ni hadidu rejea Nam. 5 ambayo inasomeka iwapo upatikanaji wa majenereta 32 yaliyopo mtoni yalifuatwa sheria zinazohusika na kwa nini hayatumiwi kwa manufaa ya wananchi. Mhe. Spika, kazi yetu kubwa kama Kamati katika hili ilikuwa ni kuona tu upatikanaji wa yale majenereta. Je, zilitumika njia za kihalali za kuyapata na la pili je, majenereta yale yana manufaa kwa wananchi.

Mhe. Spika, hili la kwanza mimi nimepata utata mkubwa na nilikujakuchanganywa na Mhe. Mansour kidogo hapa. Alivyoeleza yeye maana yake sisi katika kuchunguza kwetu tuliangalia njia tatu, kwanza tuliangalia na tulipata tetesi ndio tulijaribu kuangalia kwamba pesa alizonunulia majenereta yale ni zile pesa za misamaha ya madeni wanaita MAN TRAC ambazo utumikaji wake pesa zile haziletwi kama keshi serikalini, isipokuwa serikali inapatiwa huduma

moja kwa moja, kwa hivyo hakuna *procurement* ambayo serikali wanaifanya kwa mpango huu. Lakini kama si pesa za madeni tukaangalia kama ni pesa za wafadhili. Mara nyengine wafadhili hata kama ni *procurement* lakini wanatumia sheria za kwao. Watu wetu kwenye taasisi mara nyengine huwa tunadai *documents* za manunuzi na nini na nini wanakwambia bwana hizi walifanya wenyewe wafadhili ndio njia aliyoizungumza Mhe. Mansour Yussuf Himid. Lakini njia nyengine hao wafadhili wanachukua pesa wanaipa serikali, sasa serikali inatumia, sasa ikiwa ni aina hii maana pesa wamepewa serikali na wao wakitumia wanalazimika kutumia kwa mujibu wa sheria nam. 9 ya mwaka 1995 ya *procurement and disposal Act*. Sasa katika kudai *document* ndio nikasema nimechanganyikiwa kidogo na hapa nahitaji ufafanuzi.

Mhe. Spika, tulipokuwa tukiangalia *document* kuna *document* moja tumelifanya kama kiambatanisho Nam. 95 waliyokuwa na hichi kitabu waangalie, ukiangalia hii inasomeka hii *contract* kuna *document* ni *contract between Zanzibar electricity cooperation* ZECO *and* MAN TRAC *Tanzania limited* yaani *catapilar deallers, for procurement of emergence power back up generating set*
Sasa *document* hii Mhe. Spika, inaleta utata kwamba kama ni hii maana yake walionunua ni ZECO wao ndio walionunua kwa MAN TRAC sasa kidogo hii inatofautiana na maelezo ya Mhe. Mansour. Nilikuwa naomba sana serikali itupe ufafanuzi ni pesa za aina gani hizi. Maana ikiwa ni msaada ule ulipewa serikalini basi ni ZECO ndio walionunua na kama ni pesa za misamaha ya madeni hii *document* haina maana na tuliipata naomba ufafanuzi hapo.

Mhe. Spika, ninafikiri baada ya kwisha kusema hayo kama nilivyosema sitaki nipoteze muda wako mwingi mimi hii ripoti ni yangu kwa hivyo lazima niiunge mkono mia juu ya mia. Ahsante.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi jioni hii ya leo niweze kuchangia katika hoja hii inayotoka katika kamati ya PAC juu ya utendaji katika Shirika letu la Umeme la ZECO.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa kutoa shukurani kwa kamati hii kwa kazi nzuri iliyofanya nikiwemo na mimi Mjumbe wa kamati vile vile kwa hivyo ninajipongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa nimekuwa kitinda mimba katika kuchangia, nakuta michango yangu mimi ambayo nilikuwa nimeipanga nichangie imeelezwa. Lakini nitaingia na mimi kidogo kidogo hadidu rejea hizi ili nitie nyama mule ambamo wenzangu kidogo waliacha nafasi ili nijalize vizuri.

Mhe. Spika, tukiangalia hadidu rejea zilizoletwa mbele ya kamati zilikuwa ni sita, tukianza na hii ya mwanzo ya upotevu wa fedha za Shirika unaotokana na uungwaji wa umeme unaofanywa na watendaji wasiokuwa waaminifu.

Mhe. Spika, hili suala kwa kweli lipo na ukiangalia ripoti na vielelezo vile viambatanisho vya ripoti hii basi hata hapataki tochi, viko wazi na vya uhakika kabisa. Kwa sababu kazi hii ilipofanywa haikufanywa na kamati peke yake. Kazi hii imefanywa tukishirikiana na watendaji tena wale wa juu kabisa wa Shirika, kila mahala ambapo tulikwenda au kila mahala ambapo tulikuwa tunafanya mahojiano tulikuwa tukifanya kwa pamoja, na wao walikuwa mashahidi ya wale tuliokuwa tunawahoji juu ya mambo haya.

Mhe. Spika, kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana kabisa kuona kuwa kuna baadhi ya watendaji wetu si waaminifu. Kuna wachangiaji waliochangia hapa wamewazungumza sana lakini wengine wakasema watendaji wote wa serikali si waaminifu, mimi kidogo ninapishana na mawazo hayo si wote. Kuna baadhi ya watendaji wetu wa serikali si waaminifu, wako watendaji wanafanya kazi zao kwa uadilifu na uaminifu kabisa. Kwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa kidogo nilikosoe hilo kwa baadhi ya wachangiaji ambao waliteleza kidogo katika hili. Tunao watendaji wetu wazuri sana na waadilifu na waaminifu katika serikali. Lakini wapo wengine ndio kama hivi wamejitokeza kwenye ripoti. Mhe. Spika, ni aibu kusema.

Mhe. Spika, nikiendelea niende kwenye hadidu rejea ya pili ambayo hii ilikuwa inafanana na ile ya mwanzo; hii ni ya sababu ya usumbufu wanaoupata wananchi wetu wakati wa kuomba na baada ya kulipia. Imechangiwa sana hadidu rejea hii lakini Mhe. Spika, mimi ninachokiona hapa zaidi ni tamaa ya baadhi ya watendaji wetu au tuseme kwa njia ya rahisi sana rushwa, wanatengeneza hii michongo paonekane pana shida sana huwezi kupata umeme, au ushalipia kupata huduma ile ya kuungiwa ni shida, huu ni mchongo unaotengenezwa makusudi ili watu waweze kupata chochote. Kwa hivyo hii Mhe. Spika, ni rushwa inatengenezwa kwa makusudi ili wananchi wetu waweze kupata usumbufu waweze kukamuliwa kitu chochote ili aweze kupata ile huduma. Imetolewa mifano hapa kuna watu wamelipia wanakaa zaidi ya miezi 6 hawajapata ile huduma na kuna watu analipia mwezi huu mwanzoni kabla ya mwisho wa mwezi huduma ile wameshapata. Sasa hiyo haitaki tochi Mhe. Spika, inaonekana dhahiri namna gani baadhi ya watendaji wetu walivyokuwa wakorofi katika suala hili.

Mhe. Spika, nakwenda haraka haraka niende katika taratibu za ajira katika Shirika, hadidu rejea ya tatu. Ni kweli Mhe. Spika, kuna tatizo katika ajira kwenye Shirika la Umeme hilo tumeligundua, tulianza kufanya uchunguzi pale ninafikiria kwenye uajiri wa mwaka 2008 tulianzia pale mpaka 2012. Kila mwaka ambao tuliukagua basi tulikuta maozaoza ya ajira. Ajira zinafanywa kwa upendeleo kweli Mhe. Spika, ni upendeleo wa dhahiri si upendeleo wa Uunguja na Upemba wa U-CCM na U-CUF hapana, ni wa udugu wa damu hilo tumelishuhudia. Kwa kweli Mhe. Spika, ni kitendo cha kusikitisha sana kabisa kinachofanywa. Kuanzia mwaka 2008 mpaka 2012 hakuna mwaka ambao umefanywa ajira kukakosekana kitu hichi. Na kuna watu kabisa tulifichiwa hata mafaili yao kuyaona, maana ile aibu inaonekana imezidi zaidi. Maana waswahili wanasema mambo *mengine ehe mengine kinehe.*

Sasa inabidi watu wafiche hata yale mafaili, unauliza mliajiri wangapi, unaambiwa kumi na mbili tu hao. Lakini ukiangalia kule unakuta kuna 23 hao wengine wako wapo hadithi zinakuwa kama hizo faili limeroa, faili halionekani kaajiriwa juzi huyo faili linaroa, sijui wa mwaka 1990 utalipata wapi wale wanaitwa wa *state fuel*.

Mhe. Spika, niendelee mbele kwenye hadidu rejea ya nne iwapo mali za shirika zinauzwa kwa kufuata taratibu. Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya mali za Shirika ambazo tumezifanyia uchunguzi kule zimeuzwa bila ya kufuata utaratibu, hakika kabisa. Hili halina shaka kwa ushahidi kabisa hata na wao wenyewe hiyo *management* tuliokuwa nao walikiri hilo. Maana yake unapomuuliza mtu anapokosa jawabu anakutizama maana yake kakosa jawabu la kukujibu, hajui hata akudanganye vipi maana hudanganyiki mtu mzima. Sasa lipo na linafanywa kwa njia ya kiujanjaujanja. Mimi ninaweza kusema Mhe. Spika, hili nalo ninalipeleka katika mkondo ule ule kwamba kuna ujanja unafanywa ili watu waweze kupata kipato kwa njia nyengine na ndio maana

yakawa yanafanyika hivyo. Kwa sababu taratibu za serikali zipo, namna ya kuhaulisha mali za serikali, namna ya kuziondosha kuna sheria kabisa ya hili na hili ni Shirika la serikali linatakiwa kufuata sheria zilizowekwa na serikali.

Lakini Shirika hili linafanya linavyotaka, kwa hivyo uhakika Mhe. Spika, kwa hadidu rejea hii mimi ninafikiria ukiangalia viambatanisho vilivyomo ni ushahidi tosha wa kuona kwamba sheria za manunuzi za uhaulishaji wa mali za serikali pale hazifuatwi ni shaghala baghala tu pale. Watu wanaamua Alkhamis, Ijumaa wanaandika barua, Jumamosi unapigwa mnada, mnada wenyewe feki vitu vinauzwa vitu vitatu kwenye mnada, vitu kumi na mbili havionekanwi kwenye mnada anakuja kuletewa kwa nyuma Mhasibu na hivi navyo tumeuza ee andika huko basi ndio mtiririko ulivyokuwa ukienda.

Mhe. Spika, nisogee mbele kwenye hadidu rejea ya tano iwapo upatikanaji wa majenereta 32 yaliopo Mtoni ulifuata sheria zinazohusikana na kwa nini hayatumiwi kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar. Mhe. Spika, mzungumzaji aliyepita Mhe. Abdalla alilizungumzia vizuri hili, kuna mchangiaji mmoja asubuhi alilichangia hili kwa ufahamu ambao kuwa yeye anafahamu. Na kila mmoja anachangia kwa mujibu ambavyo yeye anafahamu. Lakini kwa hili kwa sisi kama kamati ambao tulikwenda pale na tulilifanyia kazi utaratibu Mhe. Spika, haukufuatwa. Maana ununuzi wa mali kama hizi hasa kwa fedha nyingi kuna utaratibu wake haukufuatwa utaratibu. Lakini wakati huo huo wakati tulipokuwa tunafuatilia hoja hii mpaka kufika kwenda Dar es Salaam kwa Mantrac tulikuwa tunajua majenereta yale hayakununuliwa na Shirika la Umeme, maana ndizo taarifa ambazo tumepewa na *management* kwamba majenereta yale hayakununuliwa na Shirika, majenereta yale yametolewa na wafadhili kutolewa maana yake kuletewa. Lakini tulichokikuta Mantrac ni kwamba Shirika la Umeme ndio ambalo limefunga mkataba na Mantrac kwa ajili ya ununuzi wa majenereta yale. Lakini Shirika la Umeme ndio lililolipa. Ukiangalia kwenye kiambatanisho mle kuna *cheque* kule imeoneshwa ya fedha zilizolipwa dola 1,200,800 kama sikosei zilizolipwa kwa ajili ya majenereta yale.

Sasa ukisema majenereta haya yaliletwa tu na wafadhili bila kushirikishwa Shirika la Umeme si kweli. Majenereta haya walikuwa wanakaa vikao, *minutes* za vikao tumeziona namna walivyokuwa wakishauriana mpaka ununuzi wake ulivyofikiwa na Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme ndiye aliyesaini mkataba ule ukiungalia humu umo kwenye kiambatanisho alichokitoa Mhe. Abdalla ninafikiri namba 95 umo mkataba amesaini Meneja wa Shirika la Umeme kwa niaba ya Shirika. Maana sio Serikali ya Mapinduzi iliyonunua iliyonunua ni Shirika. Maana kama serikali ninafikiri angekwenda Katibu Mkuu lakini Shirika lenyewe ndio lililonunua kwa Mantrac. Kwa hivyo kusema kwamba hawakushirikishwa si kweli. Shirika la Umeme ndio lililonunua majenereta haya lakini majenereta haya kwa kweli Mhe. Spika, hayana manufaa kwa wananchi wa Zanzibar. Maana tumeyanunua yapo pale lakini hayatumiki, ndio maana katika mapendekezo ya kamati ukaona kamati imependekeza kama mambo matatu yafanyike, ingawa mchangiaji mwenzetu alichangia moja tu kwamba atashangaa kuona majenereta yale yanauzwa. Lakini la kuuzwa lilikuwa la mwisho. Nikienda kwenye mapendekezo utaona hapa Mhe. Spika.

Mapendekezo ya Kamati kuhusu hadidu rejea imeandikwa namba sita hapa katika mapendekezo. Kwa kuwa majenereta 32 umekuwa mzigo mkubwa kwa shirika, ni mzigo kweli shirika lenyewe limekiri kwamba haliwezi kuyaendesha majenereta yale kwa sababu kuyaendesha majenereta yale ni gharama na gharama zile kama watayaendesha wao Shirika, wanahitaji wapatiwe shilingi

milioni 500 kutoka serikali ili kuweza kufidia ama wapandishe bei na ukweli wenyewe kutokana na mafuta yanayotumia yale, wapandishe umeme bei kutoka hiyo *unit* iliyopo sasa mpaka 560 ili waweze kukidhi haja kwamba sasa wakiyaendesha kwa bei hiyo ndio yataweza kulipa. Ndio hapa tukasema kwa kuwa uendeshaji wa majenereta 32 umekuwa mzigo mkubwa kwa shirika, serikali ama ichangie ruzuku katika uendeshaji wake ndio zile milioni 500 ambazo ichangie serikali imesema haina au kutafutwe utaalamu utakaowezesha majenereta hayo kutumia *diesel* ya kawaida yenye gharama nafuu badala ya ile ambayo inatumia sasa hivi ambayo iko juu kidogo bei yake. Au yauzwe na badala yake yatafutwe mengine kwa mujibu wa sheria yatakayoweza kutumika kama inavyokusudiwa.

Hayo ndio mapendekezo ya kamati yapo matatu hayo serikali itaangalia, ama itachangia katika zile milioni 500 ama italiruhusu Shirika la Umeme lipandishe *unit* za umeme kutoka bei hii iliyokuwepo mpaka 560 au yauzwe fedha zile yakishauzwa yatanunuliwa mengine yatakuwa yanakidhi ile haja ambayo inatakiwa kwa sababu sasa hivi hayakidhi haja, majenereta yale yamenunuliwa kwa sababu ya kutokuwepo umeme. Lakini tunapata matatizo kila siku hapa umeme unazimwa saa moja na nusu kila eneo unazimwa saa moja na nusu kwa sababu ya nini, ile *line* ya kupitisha umeme kule haina nguvu ya kutuletea umeme unaotosha. Sasa majenereta yale sisi wananchi wa kawaida huku tunadhania kwamba yalikuwa yataweza kutusaidia kupunguza lile tatizo, ingawa tumeambiwa yameletwa kumbe mpaka ikiwa umeme haupo kabisa ndio yawashwe. Lakini hata kama utakuwa haupo kabisa yatakapowashwa sijui yatakuwaje. Maana gharama sifikirii kama zitapungua zitabakia pale pale.

Mhe. Spika, mimi kwa kumalizia niunge mkono hoja hii kwanza asilimia mia kwa mia, kwa sababu mimi ni Mjumbe wa kamati hii siwezi kuipinga hata kidogo na nikubaliane na mapendekezo yote yaliyotolewa na kamati hii.

Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mkwajuni, tunaunga mkono asilimia mia kwa mia, mapendekezo haya na tunaiomba sana serikali, iyachukue mapendekezo haya yakishapitishwa hapa na Baraza iyachukue ikakae, itafakari vizuri lakini yafanyiwe kazi na kuyatekeleza. Kwa sababu serikali nayo imekuwa na kigugumizi lazima tuambizane ukweli, serikali imekuwa na kigugumizi. Tumetoa ripoti ya mwanzo hapa ya Kamati Teule mpaka leo tunakwenda tukarudi. Mhe. Mohammed Aboud mara kikao hiki mara leo kimeakhirishwa, mpaka leo hata hilo jawabu hajalileta sijui la kamati ya Manispaa kama itakuja au nayo vile vile haijakaa sawa, lakini wa Kamati Teule mpaka leo hatujamaliza kukaa vikao.

Kwa hivyo serikali isiwe na kigugumizi iende ikayafanyie kazi haya na iondoshe muhali na tatizo linaloonekana ni muhali Mhe. Spika, muhali iondoshe serikali ifanye kazi ya wananchi, hii serikali imewekwa na wananchi, wananchi ndio walioichagua hii serikali na wananchi ndio waliopendekeza haya kwa sababu sisi tupo hapa kwa ajili ya wananchi. Kwa hivyo kama wananchi ndio mapendekezo yao haya tunaomba serikali sasa iyachukue na ikayafanyie kazi, iseme haya ndio mapendekezo ya wananchi. Kwa sababu hiyo serikali iliyokuwepo imechaguliwa na wananchi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuzingatia yale tuliyokubaliana mapema kwamba michango tuimalize leo na kesho mara baada ya maswali tumuite Mwenyekiti, basi inabidi tuombe muda zaidi kidogo kwa kumaliza hawa baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri walioomba.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza hoja iliyo mbele yetu ili kutoa nafasi kwa wachangiaji waliobaki waweze kumaliza kutoa michango yao, na ili kesho asubuhi tuweze kumpa nafasi Mwenyekiti wa Kamati hii aweze kufanya majumuisho ya ripoti hii. Kwa hivyo Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tutengue kanuni ya muda ili tuendelee kumaliza kazi iliyo mbele yetu na baada ya hapo tukutane kesho.

Kwa hivyo Mhe. Spika, naomba Baraza lako Tukufu tukubaliane tuendelee mpaka pale ambapo tutamaliza shughuli iliyo mbele yetu kama tulivyopanga leo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuzungumza machache dhidi ya ripoti hii. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu subhana llahu wataala kwa kutuwezesha kukutana hapa jioni hii tukiwa wazima na salama na amani.

Lakini pili na mimi naomba niipongeze sana sana kamati hii kwa kuwasilisha ripoti yake hii vizuri sana, na vile vile nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii kwa kuja kuiwasilisha vizuri na kuitolea ufafanuzi wa kina, jambo ambalo limetufunua macho na kutufanya sisi viongozi tuweze kujipanga na kusimamia Idara zetu na Mashirika yetu vizuri.

Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tutahakikisha kwamba ripoti hii tunaichukua na tutaifanyia kazi na itajibiwa na serikali majibu yenye manufaa. Na naamini kwamba serikali haitomuonea haya, haitomvumilia yule yoyote ambaye atakayegundulika kama kahusika katika ubatilishaji wa mali za serikali.

Mhe. Spika, wachangiaji wengi waliochangia walikuwa wanalalamika sana kuhusiana na upotevu wa fedha kiasi cha shilingi milioni 37. Lakini na mimi nina masikitiko makubwa sana juu ya upotevu wa fedha hizo, lakini vile vile Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme kila siku huwa inatoa matangazo kwamba mtu yoyote anayetaka kuungiwa umeme basi afike Shirika la Umeme. Na akifika pale ajaze fomu ya mkataba, baadae Shirika la Umeme hupeleka wafanyakazi wetu kwenda kumpimia mteja huyo na kumfanyia hesabu, na hesabu hiyo huingizwa kwenye faili laki. Lakini kinachosikitisha kwamba muwekezaji huyu Amani Ibrahim Makungu ningeomba tufungue ukurasa wa 17 tuangalie ripoti hii. Amani Ibrahim Makungu kapata maelekezo ya kutosha kutoka Shirika la Umeme tena maelekezo hayo kapata kwa

maandishi, kapewa barua ya tarehe 28/4 ambayo ilikuwa na maelekezo ya kutosha, lakini cha kusikitisha hakufuata maelezo hayo na akafuata ushauri wa mtu binafsi na fedha hizi hakuzilipia sehemu husika hatimae akazilipa kwa mtu binafsi. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. Kwa hivyo na mimi ningeomba serikali ianzie kuchukua hatua hapa kwa sababu huyu alikuwa anajua nini anachokifanya. Kama kapata maelekezo kutoka Shirika la Umeme hakuyafuatilia na akapata maelekezo kwa mtu binafsi akafuata muongozo wa mtu binafsi na akaingiza fedha hizi kinyume na utaratibu wa kupitia Shirika la Umeme, basi huyu mimi nasema ni muhusika ambaye kafanya kwa makusudi kuikosesha mapato serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. mimi sitaki nizungumze mengi kwa sababu si mjibuji hoja, lakini vile vile naomba nimshukuru sana Mhe. Mansoor kwa kutoa ufafanuzi wa kina juu ya ununuzi wa majenereta.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, ninakushukuru sana, nasema ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati): Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu inayohusu ripoti ya kazi maalum ya Kamati ya PAC kuchunguza utendaji wa Shirika la Umeme Zanzibar.

Vile vile nimshukuru Mwenyekiti wa Kamati hii na kamati yake kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuibua mambo mbali mbali kwa nia ile ile ya kusawazisha makosa na kuweka taratibu nzuri kwa nia njema ya kuhudumia wananchi wetu vizuri. Nataka nimpongeze Mwenyekiti na kamati yake.

Aidha niwapongeze Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia na wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia nikiamini kwamba nao walikuwa na mawazo kama ya wenzao katika kuhakikisha kwamba tunalinda na kuendeleza raslimali za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti nimshukuru sasa Naibu Waziri kwa ufafanuzi mzuri alioutoa katika kusaidia taarifa ya ripoti hii. Mhe. Spika, kazi hii ni kazi nzito, kubwa lakini imefanywa kama walivyosema Wajumbe waliotangulia kwa umakini mkubwa na umahiri mkubwa sana wa Mwenyekiti na Kamati yake, kwa hivyo hatuna budi kuwapongeza kwa imani hiyo ya kujitolea katika kujenga nchi yetu.

Mhe. Spika, sisi kwenye serikali hatuna hata siku moja nia ya kuficha maovu, ya kuficha ubadhirifu, ya kuripua mambo ama kwa njia yoyote ile ya kufanya udanganyifu wa aina yoyote. Nia ya serikali yetu Mhe. Spika, ni kufanya kazi kwa uadilifu, kwa haki, kwa bidii, ili wananchi wetu waweze kuwa katika hali nzuri zaidi na wapate huduma zilizo bora zaidi. Hayo ndio madhumuni ya serikali wala hakuna dana dana yoyote Mhe. Spika, nia ni kufanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha malengo na madhumuni yaliyokusudiwa na serikali yetu yanatekelezwa kwa nia ya kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kazi ilikuwa nzuri iliyofanywa, lakini kama walivyosema wenzangu waliotangulia hakuna mkamilifu Mhe. Spika, hasa hasa katika kuhakikisha unatenda haki ya wengine. Mhe. Spika, binaadam ni binaadam inaweza kutokea kasoro mbali mbali katika utekelezaji wa mambo, hivyo ni vizuri tukakubaliana kwamba juu ya uzuri wa ripoti, juu ya kazi kubwa iliyofanywa na ripoti lakini na mapungufu ya kibinaadam ni kawaida hujitokeza. Hivyo ni

vizuri sheria zetu, taratibu zetu zikatumika katika kufikia muafaka wa kufanya maamuzi yatakayoleta haki na yasiyo na upendeleo kwa ajili ya kufanya uadilifu kwa watu wote. Nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba inaondoa maovu, inaondoa kero, inaondoa rushwa, inaondoa ubadhirifu hiyo ndio nia yetu ili kujenga serikali yenye heshima kwa jamii yote ya wazanzibari na Tanzania kwa jumla.

Mhe. Spika, serikali yetu inachukua jitihada mbali mbali katika kuondoa matatizo mbali mbali, jitihada hizo zikiwemo za kisera, za kisheria, za kimiundo, zinafanywa hivyo kwa ajili ya kuweka uwazi, uajibikaji na kufanya kazi kwa tija na uadilifu ili mwisho wa siku huduma bora zitoke kwa wananchi wetu. Tusingependa kabisa Mhe. Spika, kuona wananchi wetu wanapata tabu, wanadhulumiwa, wanabaguliwa, wananyanyaswa ama kufanyiwa vyengine vyovyote kinyume na taratibu na sheria ambazo kwa pamoja tumekubaliana ziheshimiwe na zilindwe.

Mhe. Spika, kwa msingi huo serikali haina haja ya kuficha siri yoyote wala haitofanya hivyo na ni madhumuni ya Serikali hii ya Awamu ya Saba kuhakikisha inawatumikia wananchi wake kwa uadilifu na haki ya kila mmoja inapatikana. Na ukweli nia na madhumuni ni kuondosha kila maovu ili mambo yaende vizuri na tufanye kazi kwa pamoja. Tunaamini kabisa Mhe. Spika, kwamba muarubaini wa matatizo yetu ni kufanya kazi pamoja kati ya Serikali na Baraza hili la Wawakilishi, hakuna mapendekezo hata mamoja Mhe. Spika, yanayodharauliwa na serikali, serikali inayafanyia kazi na maamuzi magumu yanafanyika ili kuhakikisha utendaji unakuwa mzuri na shughuli zinakwenda vizuri.

Mhe. Spika, hakuna haja kabisa ya malumbano nia yetu ni kuwa tufanye kazi kwa bidii tuondoshe matatizo yaliyo mbele yetu. Ni uhakika Mhe. Spika, matatizo hayawezi kwisha katika maisha ya binadamu ni jambo la mchakato, likimalizika hili leo litajitokeza lile kesho, lakini cha msingi ni nia njema ya kuyashughulikia matatizo hayo na serikali yetu jambo hilo inayo na itafanya hivyo ili kuhakikisha kwamba kila ovu, kila baya linapata ufumbuzi ili tuishi katika mazingira yaliyo mazuri kabisa.

Lakini Mhe. Spika, sisi kama viongozi lazima tukubali kwamba sisi ni baba wa wenzetu. Kwa hivyo, lazima tuwe waadilifu zaidi na lazima tuwe makini zaidi na lazima tunapofanya mambo tusifanye mambo kabisa kabisa hata kidogo ikatoa sura kwa namna moja au nyengine ya kupendelea, lazima tufanye mambo na maamuzi yetu yatende haki ili maamuzi yetu kila mmoja tunapoyafanya aridhike nayo. Huo ndio wajibu wetu Mhe. Spika. Kwa hivyo, mimi naamini kamati na Baraza lako tukufu litakubaliana na maamuzi ambayo mwisho wa siku serikali itayachukua kwa yale mapendekezo ambayo Baraza lako tukufu hili yameyapendekeza kwa serikali.

Lakini pia tukubali kwamba Mhe. Spika, katika zama zetu hizi kuna baadhi ya wafanyakazi sio waaminifu, sio wakweli, lakini wapo wafanyakazi na watendaji wengi Mhe. Spika, ni waaminifu kwa kweli wanaitumikia nchi hii vizuri sana tena usiku na mchana, wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na wanafanya kazi vizuri lazima hao tufike mahala nao tuwapongeze katika ufanyaji wao kazi. Kwa sababu wanafanya vizuri katika kuitumikia nchi hii. Kwa wale ambao wakorofi basi ni wajibu wetu kwa pamoja kuwashughulikia na kuwapa stahili ya ukorofi wao, hakuna atakayevumilia ukorofi.

Vile vile tuelewe kwamba wengine ni wajanja sana Mhe. Spika, hutoa taarifa kwa viongozi kana kwamba wao ni watu safi, watu wazuri, wana nia njema, kumbe wao ndio chanzo cha matatizo. Kwa hivyo, si kila taarifa tunayopewa tukaiamini kwamba ni sahihi tu Mhe. Spika. Hivyo mimi naomba sana viongozi wenzangu kwamba wako baadhi ambao hutafuta mianya namna hii inapotokea ili ima kuwaumiza viongozi wao au kuharibu jina zuri la shirika wakati mwengine au taasisi wanayoitumikia. Sasa tuwe makini vile vile yanapotokea mambo kama haya.

Mimi ninachoamini waliyoyaibua kamati kwetu sote ni mafunzo ili tujifunze, tuwajibike vizuri zaidi, tufanye wajibu wetu tuondoshe kasoro zilizopo na nia yetu ni kufanya mambo ya kuwatumikia wananchi kwa utaratibu ulio bora zaidi na waridhike ili wasipate bughdha wala tabu ya aina yoyote.

Kwa hivyo Mhe. Spika, tuhuma mbali mbali hapa zimeoneshwa, lakini naomba sana Baraza lako tukufu baada ya kuona tuhuma hizi sisi si vyema tukawa mahakimu wa tuhuma zilizotokea, lazima vyombo husika navyo vifanyie kazi tuhuma hizi ili uadilifu upatikane na taratibu za sheria zichukue mkondo wake ili wale wanaohusika basi ni sheria iwe ndio imechukua mkondo wake kwa nia ya kuhakikisha kwamba haki imetendeka. Tumezungumzia sana hapa suala la upendeleo, suala la ubaguzi, sasa mambo hayo yasigeuke ikawa tumeyafanya sisi ndani ya Baraza hili. Mimi naamini sote nia yetu ni moja nia yetu ni kujenga, nia yetu ni kuondosha matatizo yaliyopo ili watu wetu waishi kwa furaha na haki itendeke na kila mmoja aweze kutimiza wajibu wake.

Lakini vile vile tuelewe kwamba baadhi ya wenzetu ambao tunawazungumza hapa hawana nafasi ya wao kujieleza mbele ya Baraza hili. Baadhi ya Waheshimiwa hapa walisema maneno mazuri sana, kwamba lazima nao utu wao ulindwe, heshima yao ilindwe ili nao wawe na nafasi nzuri katika jamii na tusiwatafsiri kwa tuhuma tuwatafsiri pale ambapo vyombo husika vimefanya kazi yake na vikaona kwamba watu hawa wana makosa stahiki na sheria inapochukua mkondo wake, kufanya vyengine Mhe. Spika, itakuwa hatukufanya uadilifu kwa wengine na itakuwa yale yale ya upendeleo yatajitokeza kwa sura nyengine.

Kwa hivyo, naomba sana chombo chako hiki kikubwa Mhe. Spika, ambacho kina heshima kubwa tuendelee kutunza heshima hiyo kwa kufanya mambo kwa uadilifu mkubwa ili maamuzi yetu yasimamie haki na ili wale ambao wamekwenda kinyume na taratibu wao ndio wahusike na wale waliokuwa hawamo basi wasiwemo. Naamini kwamba serikali yetu itaangalia mambo haya kwa undani sana na serikali yetu Mhe. Spika, imeambiwa tujitizame katika utendaji wetu, huo ndio utamaduni wetu wa sasa wa kila siku. Rais wetu na viongozi wetu kila mara wanatuhimiza kujitazama katika utendaji wetu ili tutoe utendaji uliotukuka kwa tunaowatumikia wananchi wetu.

Mhe. Spika, siwezi kupingana kabisa na Baraza hili kwenye jambo hilo, ni lazima wakati wote tujipime na tujirekebishe. Hata utaratibu ambao Mhe. Rais ameuanzisha ule wa kukutana kwa kila baada ya miezi mitatu ni kipimo cha kutuangalia mafanikio yetu na namna ambavyo tumetekeleza yale ambayo tumeyasema hapa na tumeyasema mbele yake ili utendaji uwe mzuri. Naamini Mhe. Spika, safari yoyote ni hatua, makosa tuliyoyafanya nyuma hatuyafanyi leo tena kila wakati tunapopata mafunzo ya Baraza hili na mafunzo ya viongozi wetu tunachukua kila

hatua ya kuhakikisha kwamba tunajirekebisha ili tuhakikishe tunaongeza kasi ya kujirekebisha na tufanye mazuri kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, limezungumzwa sana suala la upendeleo, nataka nikuhakikishie kabisa kabisa Mhe. Spika, serikali yetu inapiga vita upendeleo wa aina yoyote na isingependa kufanya ubaguzi wa aina yoyote, haingependa kumbagua yoyote, ingependa kabisa kwamba kila mmoja apate haki yake na taratibu zilizopo za kisheria ziheshimiwe. Kwa hivyo, yanapotokea makosa ya namna hiyo isiwe kunaonesha dhamira yoyote kwamba serikali ina nia ya kupendelea, serikali haina nia ya kupendelea na ikiwa ametokea mtu kufanya hivyo ni makosa ya mtu na lazima hatua zichukuliwe dhidi yake.

Nia ya serikali si kuwa na upendeleo wa aina yoyote wala kumbagua yoyote wala hakuna aliye juu ya sheria sote tuko mbele ya sheria na sote tunawajibika kufuata sheria. Hakuna wala nchi na wananchi sote ni wananchi, wala nchi ni wafanya makosa na wanatakiwa wapelekwe katika vyombo vya sheria. Kila kitu chetu ni chetu pamoja, nchi yetu pamoja, kwa hivyo ni kufanya kazi kwa kufuata misingi ya katiba na sheria za nchi yetu ili tutoe huduma zilizo bora.

Mhe. Spika, ni ukweli usio shaka kwamba tunatakiwa tutoe huduma bora na za makini kwa wananchi wetu, hatutakiwi kabisa kuwapa shida wananchi wetu kwa aina yoyote wala hatutakiwi kutoa huduma za kuwapendelea hawa na hawa tukawanyima haki. Wananchi wote ni sawa mbele ya sheria na tunapaswa huduma zetu ziwe za viwango, nzuri, za nafuu, rahisi kupatikana na zisiwe za bughdha yoyote ya rushwa wala kukejeli wengine, kufanya vyengine vyovyote Mhe. Spika, ni kwenda kinyume na dhamira ya serikali yetu.

Mhe. Spika, pia nataka nikubaliane na Baraza lako tukufu kuhusu kuitaka serikali kuhakikisha kwamba CAG anafanya kazi zake vizuri na kwa mujibu wa sheria. Ushauri huo tunaupokea na utafanyiwa kazi ili kuhakikisha kwamba mambo yote yanakwenda kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa ili kuepuka kabisa namna yoyote ile ya kutumika vibaya kwa mali za umma.

Vile vile nakubaliana sana kuhusu suala zima la marekebisho ya ukaguzi wa ndani. Wizara yetu ya Fedha imeanza kuchukua hatua hizo kuhakikisha kwamba wakaguzi wa ndani hawakai mahala pamoja kwa muda mrefu na kufanya marekebisho makubwa ili kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri. Pale inapotokea kwamba mke au mume akiwa ni Mhasibu Mkuu na pengine chini yake ni mkewe au mtu mwenza wake jambo hilo si busara hata kidogo.

Mhe. Spika, hayo kama yametokea katika sehemu mbali mbali waziri muhusika yupo ninae hapa jirani na tumenong’ona akasema bwana hilo si jambo la busara na kila jambo linaloelekea na ishara namna hiyo litachukuliwa hatua ili lirekebishwe mambo yende vizuri. Haiwezekani wapenzi wawili wakawa wapo pamoja wanafanya kazi ambazo zote za kuhudumia umma na matokeo yake ikasababisha hasara kwa nchi, jambo hilo haliwezi kuvumilika. Kwa hivyo, nia ni kuziba mianya yote ile ya rushwa na ubadhirifu.

Mhe. Spika, yamejitokeza mambo hapa kwa baadhi ya wateja wenye kazi kubwa au miradi mikubwa ya Shirika la Umeme na bado ikawa wanalipa fedha kidogo. Kwa mtazamo wa Shirika la Umeme inawezekana kabisa wakati mwengine yakatokea hayo, kwa sababu kuna wateja wanaonunua vifaa vyao vyote ikabaki Shirika la Umeme kutoa *labour charge*, kwa maana hiyo

inaweza kuwa kazi kubwa lakini gharama za malipo zikawa ndogo na vile vile inawezekana kazi ndogo lakini kwa sababu vifaa pia vinamstahikia ilipe Shirika huyu mteja akalipishwa zaidi.

Kwa hivyo, haya mawili yanaweza kujitokeza, inawezekana kabisa ukawa umelipa kidogo na kazi yako ikawa kubwa lakini inategemea na vifaa umevinunua pengine wewe mwenyewe, lakini kama vifaa vimetolewa na shirika na bado ukalipa kidogo hapo lazima utakuwa ubadhirifu upo wazi kabisa. Lakini pale ambapo mteja amenunua vifaa vyake isipokuwa kazi kafanyiwa na shirika basi hiyo itakuwa na gharama zake mbali, *charge* zake zitakuwa mbali. Vile vile pale ambapo vifaa na ufanyaji kazi watu wa shirika basi gharama zitakuwa mbali na kama haikufanyika hivyo maana yake ni kinyume na utaratibu na wanaofanya hivyo lazima wachukuliwe hatua zinazofaa. Nia yetu ni kuhakikisha kwamba jambo hili halitokei.

Lakini wananchi watusaidie sio kubadilika kwenye serikali tu, na wananchi nao wabadilike itakuwaje wewe unataka huduma ya shirika umlipe mtu binafsi, haiwezekani kama unataka huduma ya mtu binafsi ukamlipe mtu binafsi akupe huduma yake yeye, lakini shirika ukalipe shirika upate risiti maalum. Mhe. Spika, ama unatoa shilingi milioni nane unapewa risiti ya shilingi 167,000 hivyo huioni, hivyo hujui, lazima yako mambo na hawa wananchi nao waulizwe. Leo wanasema jana hakusema na hawa ndio watatupa ushahidi mzuri zaide. Kwa hivyo, nataka vyombo vyetu vinavyohusika na mambo ya uchunguzi vianze na kwa wananchi hawa tuujue ukweli, haiwezekani kabisa wewe ulipe shilingi milioni nane upewe risiti ndogo uikubali, ukakaenayo chumbani mwako unaitizama kama mkeo namna gani bwana, haiwezekani lazima anajua kilichopo.

Kwa hivyo, na hapo lazima tupafanyie kazi. Hivyo mabadiliko tuwe sote tuanze kubadilika ndani ya serikali, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wananchi sote *mind set* yetu ibadilike kwa maendeleo ya nchi yetu tusiende shaghala baghala. Mafanikio ni ya pamoja tukifanya pamoja mafanikio yatakuwepo.

Mhe. Spika, ulitolewa ushauri mzuri hapa kuhusu chombo cha kuratibu bei za huduma mbali mbali ikiwemo maji na umeme. Nataka niseme wazi kabisa serikali jambo hili tayari imelifanyia kazi na katika kipindi hiki cha bajeti Mhe. Spika, pengine kesho Mungu akituajaalia uhai rasimu inayohusiana na kuanzishwa kwa chombo hicho mswada wake utasomwa kwa mara ya mwanzo katika Baraza hili tukufu. Nia ni kuwa na chombo kinachoratibu bei za huduma hizi muhimu ili wananchi wetu ziwafikie kwa utaratibu mzuri na naamini tutakuwa nayo. *Zanzibar Utility Regulatory Authority* si muda mrefu baada ya Baraza lako hili tukufu kuipitisha. Kwa hivyo naamini ushauri wenu uko pamoja na serikali tunawashukuru sana.

Lakini kuhusu suala la Umeme Mbadala Mhe. Spika, serikali jambo hili imelifanyia kazi sana, tayari kuna *study* mbali mbali zimefanywa ili tuweze kuwa na umeme mbadala nchini kwetu. Kamati maalum imeundwa kushughulikia jambo hili na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo angekuwa kapata nafasi angelieleza kwa urefu sana. Kwa sababu nia yetu Mhe. Spika, ni kuwa na umeme mbadala umeme ambao utawasaidia wananchi wetu kwa bei rahisi, wa uhakika, na ikiwezekana kukiwa na ziada tuwauzie wenzetu ndio nia yetu na kadiri utakavyokuwa nafuu ndivyo utakavyoleta maendeleo makubwa katika nchi yetu. Kwa hivyo, jambo hilo ushauri wa Wajumbe tunaupokea lakini kazi imeshafanywa.

Kuhusu ZECO na TANESCO Mhe. Spika, mazungumzo yameendelea vizuri na lile deni lililokuwa na utata mkubwa la shilingi 40 bilioni hili limeondolewa. Sasa mazungumzo yanaendelea katika kuweka bei muwafaka inayostahiki itakayokubalika kati ya TANESCO na ZECO ili ZECO inunue umeme kwa bei ya haki, bei mwafaka na mambo yamekwenda vizuri naamini tutafikia hatua nzuri.

Mhe. Spika, vile vile Waheshimiwa Wajumbe walilalamika suala la hujuma za umeme ule ambao ulitokea kwa bahati mbaya. Mhe. Spika, hakukuwa na hujuma, ule waya wa umeme ulikuwa umechoka umeshafika umri wake, umezeeka haujiwezi tena. Mimi nataka niishukuru sana na niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada walizochukua katika kuhakikisha kwamba waya ule ukatusaidia kutoa umeme mpaka leo ili tuweze kufanya *replacement* ya huu waya mpya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, hakuna hujuma yoyote pale, ni yawa umezeeka, umepitwa na wakati wajibu wake kubadilishwa na kwa maana hiyo nataka niwahakikishie Mhe. Spika, kwamba hali ya sasa tuko katika dakika za mwisho za kurekebisha.

Mhe. Spika, kwa ujumla nataka niseme yafuatayo:

Kwamba serikali inafanya kazi sana inajitahidi, kuhusu suala la mapato Mhe. Spika, mapato ya ZRB hayakupungua bali yameongezeka. Hivi sasa ZRB wanakusanya zaidi ya shilingi 12 bilioni kwa mwezi kwa hivyo ni hatua kubwa sana na jitihada zinaendelea kukusanya zaidi.

Kuhusu ununuzi wa majenereta. Mhe. Spika, Serikali ya Norway kwa kushirikiana na mashirika ya maendeleo ya DFID ya Uingereza na SIDA la Sweden pamoja walikubaliana maombi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupatiwa mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura na mgao ulikuwa kama ifuatavyo:

- Norway walitoa dola milioni nne
- SIDA walitoa dola milioni nne nukta tano
- DFID walitoa dola milioni tatu na
- SMZ walitoa dola milioni moja nukta tano.

Kwa hivyo, fedha zile zilitolewa na wafadhili na ni jambo zuri kuwa na mitambo ya umeme wa dharura. Umeme huu unapotokea *fault* yoyote yale majenereta ndio yatatusaidia mhe. Spika, kwa hivyo yale kuwepo yametusaidia na wingi wake yamefanywa vile kitaalamu. Kwa sababu kama mahitaji ya umeme ukihitajika mdogo unawasha kidogo, kama mahitaji ya umeme yanahitajika kwa wingi ndio yanatoa MW 25 yote yanawashwa. Wakati mwengine kama likitokea *fault* moja basi mengine yafanye kazi kwa ukamilifu wake. Kwa hivyo yale yalivyopangwa yalipangwa kitaalamu na ilikuwa ni jambo la msingi maamuzi yale tunashukuru.

Kwa jumla Mhe. Spika, nataka niseme Serikali imeipokea taarifa hii na itaifanyia kazi kwa umakini mkubwa, kwa uadilifu na kwa haki na bila ya upendeleo. Na kwa msingi huo Mhe. Spika, nataka niwahakikishie kwamba hatua madhubuti zitachukuliwa kadiri serikali itakavyoona inafaa na tutahakikisha kwamba aliyekuwemo yumo hatoki na asiyekuwemo haingii.

Kwa maana hiyo Mhe. Spika, naomba nikushukuru, nishukuru Baraza lako tukufu, niwashukuru Wajumbe wa Kamati, ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe huyo alikuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Nikushukuruni Waheshimiwa Wajumbe kwa michango tangu asubuhi imekwenda vizuri kwa mashirikiano makubwa na sasa niakhirishe kikao hiki hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 2:15 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe
29/01/2013 saa 3:00 asubuhi)